**10 JUNI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 10 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilianzishwa kupitia Sheria Namba 17 ya mwaka 2004...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni hati ya kuwasilisha mezani siyo hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi juu ya Azimio la Bunge kuhusu pendekezo la kuridhiwa Mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kwa

lengo la kuanzisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii katika uendelezaji wa maeneo ya bandari nchini la mwaka 2023.

Spika: Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Pamoja ambayo ilihusisha Kamati mbili; Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na Kamati ya Miundomibu kwa niaba yao Mheshimiwa Augustino Holle Vuma ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa *PAC*.

**MHE. VUMA A. HOLLE – Kn.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA PAMOJA:**

Maoni ya Kamati ya Pamoja kuhusu Azimio la Bunge kuhusu pendekezo la kuridhiwa Mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kwa lengo la kuanzisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii katika uendelezaji wa maeneo ya bandari nchini.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO LA BUNGE KUHUSU PENDEKEZO LA KURIDHIWA MKATABA BAINA YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA SERIKALI YA DUBAI KWA LENGO LA KUANZISHA USHIRIKIANO WA KIUCHUMI NA KIJAMII KATIKA UENDELEZAJI WA MAENEO YA BANDARI NCHINI

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge nimuite Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi aje awasilishe hoja kuhusu Azimio la Bunge kuhusu pendekezo la kuridhiwa Mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai.

Mheshimiwa Waziri Profesa Makame Mnyaa Mbarawa.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilianzishwa kupitia Sheria Namba 17 ya mwaka 2004. Mamlaka hii iliridhia na kuchukua majukumu ya yaliyokuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania *(Tanzania Harbors Authority)* iliyoanzishwa kupitia Sheria ya Mamlaka ya Bandari namba 12 ya mwaka 2012 ya mwaka 1977 baada ya kuvunjika ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupewa majukumu zaidi ya kumiliki, kuendesha na kuendeleza bandari zilizopo Pwani ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Spika, Sheria hiyo ya Bandari Namba 17 mwaka 2014 inaipa *TPA* majukumu ya kumiliki, kusimamia, kuendesha na kuendeleza maeneo yote ya Bandari Tanzania Bara. Madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa *TPA* yameainishwa katika kifungu namba tano cha sheria hiyo ambayo ni kuhakikisha Tanzania inaendelea kunufaika na faida ya kijiografia ikiwemo kuchagiza usimamizi bora na ufunganishaji wa tija wa bandari zilizoko Pwani ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu, kuhakikisha kunakuwa na tija katika huduma zinazotolewa za upakiaji na ushushaji wa mizigo pamoja na abiria, kuendeleza, kuboresha na kusimamia miundombinu ya kibandari, kusimamia usalama wa bandari na kuingia mikataba au makubaliano na mtu yeyote au taasisi yoyote kwa ajili ya utoaji wa huduma za bandari.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwekeza kwenye bandari zake kwa vipindi tofauti tofauti kwa kutumia vyanzo vyake na fedha za mikopo katika kutekeleza mikakati kwa lengo la kuboresha sekta ya bandari nchini. Mikakati iliyochukuliwa hivi karibuni ni utekelezaji wa mradi mkubwa wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam *(Dar es Salaam Maritime Gateway Project)* ambao umehusisha kwanza, uimarishaji na uongezaji wa kina cha Gati Namba 01 mpaka Namba 07; ujenzi wa Gati jipya la kuhudumia magari na uongezaji wa kina cha lango cha kuingia Bandari ya Dar es Salaam. Uzoefu umeonesha kuwa uwekezaji wa namna hii una faida kubwa kwa nchi iwapo bandari itaendeshwa kwa tija na ufanisi mkubwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchukua hatua mbalimbali za maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam bado ufanisi katika utoaji huduma za bandari haujafikia viwango vinavyofikiwa kimataifa. Hali ya sasa ya utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam imeendelea kuwa kiwango cha chini ukilinganishwa na bandari shindani kikanda. Kwa mfano, wastani wa meli kusubiri nangani kwa Bandari ya Dar es Salaam ni siku tano, ikilinganishwa na siku 1.25 kwa Bandari ya Mombasa na siku 1.6 kwa Bandari ya Durban. Ufanisi mdogo wa Bandari ya Dar es Salaam umetokana na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Kukosekana kwa mifumo ya kisasa ya TEHAMA;

(ii) Kutokuweko kwa maeneo ya kutosha ndani na nje ya bandari kwa ajili ya kuhifadhia shehena pamoja ya maegesho ya meli; na

(iii) Kukosekana kwa mktambo ya kutosha na ya kisasa kuhudumia shehena ambayo teknolojia yake inabadilika mara kwa mara na ina gharama kubwa ya uwekezaji na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, athari za kutokuwa na ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na meli kusubiri muda mrefu nangani ambako kunasababiisha kuongezeka kwa gharama ya kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Kwa mfano, gharama za meli kusubiri nangani kwa siku moja ni takribani dola za Kimarekani 25,000 sawa na takribani shilingi za Kitanzania 58,000,000 kwa siku; meli kutumia muda mrefu kupakia na kupakia shehena gatini kwa wastani wa siku tano ikilinganishwa na siku moja inayokubalika kimataifa; na meli kubwa kutokuja katika Bandari ya Dar es Salaam kutokana na kuchukua muda mrefu kuhudumiwa. Hali hii husababisha bandari yetu kuwa siyo bandari inayolisha shehena na bandari zingine *(feeded port)* na hivyo kuongeza gharama ya kutumia bandari hiyo na kuikosesha nchi mapato ambayo yangeweza kutumika katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati nchini ambayo ingesaidia kukuza uchumi na kuboresha huduma za wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pia kuongezea gharama katika mnyororo mzima wa uzalishaji *(total route costs)* kutoka nje ya nchi, kupitia bandari yetu kwenda nchi za Jirani zinazotumia bandari yetu ya Dar es Salaam. Kwa mfano, gharama kusafirisjhia kasha moja kutoka nje ya nchi *(on transit)* kwenda nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo inafikia takkribani dola za Kimarekani 8,500 hadi 12,000. Hii ni gharama kubwa sana ikilinganishwa na bandari za nchi jirani au nchi shindani.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa Serikali pekee haitoweza kutatua changamoto zilizopo kwenye Bandari ya Dar es Salaam, kuanzia miaka ya 2000 Serikali ya Awamu ya Tatu iliingia Mkataba wa Upangaji na Uendeshaji *(Lease and Concession Agreement)* na kampuni ya kimataifa ya uendeshaji wa Vitengo vya Makasha *Hutchson* ya Hong Kong huko nchini China. Mkataba huo ulidumu kwa takribani miaka 22 kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2022 na uliipa haki ya kipekee kampuni hiyo kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuhudumia makasha katika Gati Namba 08 hadi Namba 11 za Bandari ya Dar es Salaam. Wakati huo huo *TPA* ikiendesha na kuhudumia maeneo mengine ya bandari hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto za bandari zilizopo na kwa kuzingatia dhima ya Serikali ya kuboresha sekta ya bandari nchini, ili kuongeza ufanisi na sekta ya bandari katika mapato ya nchi, ajira na kuchagiza sekta nyingine za kiuchumi, Serikali ilifanya maamuzi ya kutafuta wawekezaji wapya wanaoendena na dhima ya Serikali. Hatua hizo zilihusisha kupokea mapendekezo ya wawekezaji mbalimbali wakiwemo Makampuni ya *Hutchson* ya Hong Kong huko China, *PSA International* kutoka Hong Kong, *DP World* ya kutoka huko Dubai, Abu Dhabi *Ports* ya kutoka huko Abu Dhabi *UAE*, *Adani Ports and Logistics* kutoka Mundra-India, Kampuni ya *CMA - CGM* kutoka Ufaransa pamoja na kampuni ya *EPMA* Maersk kutoka huko Denmark.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu ni kufungua masoko ya kimkakati katika eneo la bidhaa na biashara ya usafirishaji ndani ya nchi na kanda zinazotuzunguka. Katika kupitia mawasilisho ya

kampuni hizo pamoja na sifa zao za kimataifa, Serikali imeamua kuanzisha majadiliano na Kampuni ya *DP World* kwa kuzingatia uzoefu wake katika uendeshaji wa shughuli za bandari Barani Afrika, Asia, Ulaya na Maerkani ya Kaskazini ya Kusini. Kampuni hii ina uzoefu na utaalam wa kuchagiza myororo mzima wa usafirishaji *(end to end total logistics chain solution)* kutoka maeneo ambayo bidhaa zinatoka mpaka kufikia kwa walaji.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa maeneo maalum ya kiuchumi *(special economic zones)* karibu na bandari, usafirishaji wa baharini na nchi kavu kupitia njia ya reli; uwekezaji mkubwa katika maeneo mbalimbali ambayo imewekeza na pamoja kuajiri wazawa katika maeneo haya. Aidha, kwa upande wa mamlaka au makampuni mengine ambayo *TPA* ilipokea mapendekezo yao yalionesha nia ya kuwekeza bandarini peke yake na siyo kuchagiza mnyororo mzima wa usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, pia baadhi ya makampuni hayo hayana uwezo wa kuendesha shughuli za bandarini Barani Afrika wakati Kampuni ya *DP World* inaendesha bandari sita Barani Afrika na bandari zaidi ya 30 duniani kote kwa ufanisi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia nia ya Serikali kuvutia uwekezaji nchini wakati wa Maonesho ya *Dubai Expo* 2020 tarehe 28 Februari, 2022 hati ya makubaliano takribani 30 ilisainiwa baina ya taasisi za Serikali za Tanzania na sekta binafsi za Tanzania na taasisi za Serikali na sekta binafsi za huko Dubai kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini ili kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya makubaliano hayo ni baina ya *TPA* na *DP World* iliyolenga kuanzisha ushirikiano wa uboreshaji, uendeshaji na uendelezaji wa maeneo ya bandari nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa hati ya makubaliano hayo, Serikali iliteua timu ya wataalam ambayo ilipewa jukumu la kufanya majadiliano na wataalam wa Serikali ya Dubai na kufanikisha kuandaliwa na kusainiwa kwa

makubaliano baina ya Serikali na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kwa mujibu wa taratibu zilizopo. Makubaliano hayo ni kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamiii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lengo la makubaliano haya ni kuweka msingi wa makubalino *(framework agreement)* baina ya nchi na nchi ili kuwezesha kuanza kufanyika kwa majadiliano na kuingiwa kwa mikataba mbalimbali kama vile mikataba ya nchi mwenyeji, upangishaji na uendeshaji kwa ajili ya uwekezaji na uendeshaji wa maeneo ya bandari nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa masharti ya makubaliano hayo unapaswa kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ili utekelezaji wake uweze kuanza. Hivyo Serikali kupitia Wizara ya ujenzi na uchukuzi imeanzisha mchakato wa kupata ridhaa ya Serikali ya kuwasilisha makubaliano hayo hapa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi kuhusu mkataba wa makubaliano hayo; kwa mujibu wa ibara ya pili ya makubaliano, lengo ni kuweka msingi wa ushirikiano baina ya Serikali mbili kwa maeneo mahususi yaliyoainishwa ndani ya makubaliano husika, rejea *appendix* namba moja ya makubaliano hayo ambayo utekelezaji wake utafanywa kupitia mikataba mahususi baina ya taasisi zilizoidhinishwa katika makubaliano kama taasisi tekelezi ambazo ni *TPA* na *DP World*. Hivyo makubaliano haya hayana masharti yanayoifunga Serikali kuhusu maeneo ya ushirikiano yaliyoainishwa pasipokuwa na mikataba mahususi ya utekelezaji wa miradi inayojadiliwa na kukubaliwa na pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawanda ya utekelezaji chini ya makubaliano haya yatahusisha uendelezaji na uendeshaji wa baadhi ya maeneo ya bandari na siyo bandari yote kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Aidha, uendelezaji na uendeshaji huo utafanyika kupitia mikataba mahususi ya miradi *(project agreements)* ambayo itajadiliwa na kuingiwa kwa kila eneo la ushirikiano na itahusisha matumizi ya ardhi pekee na siyo umiliki wa ardhi ikiwa ni pamoja na Serikali kuhakikisha kuwa sheria, kanuni na taratibu za nchi zinalinda umiliki wa ardhi ya Watanzania zinazingatiwa na kusimamiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makubaliano haya yameainishwa awamu mbili za maeneo ya ushirikiano; awamu ya kwanza itajumuisha kusimamia, kuendesha na kuendeleza baadhi ya magati katika Bandari ya Dar es Salaam, maboresho ya gati la majahazi na gati la abiria katika Bandari ya Dar es Salaam ili kuvutia vyombo vikubwa Zaidi na meli za kitalii kutia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam, kuwekeza katika maeneo yaliyotengwa katika bandari kavu, kufanya uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya TEHEMA ya kuendesha shughuli za kibandari ili kuongeza ufanisi wa bandari kuwa shindani na kuwajengea uwezo watumishi wa *TPA* kutekeleza shughuli za bandari kwa ufanisi katika maeneo mengine ya bandari nchini. Msisitizo wa Serikali ni kuhakikisha maeneo yote ya nchi yanabaki chini ya umiliki wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya pili ya miradi yaani *phase two* majadiliano haya yatafanyika kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kuongeza thamani ya bidhaa, maeneo ya viwanda na miundombinu mingine itakayoongeza ufanisi katika usafirishaji wa bidhaa kwenda na kutoka nchi zinazotuzunguka, kuwekeza katika bandari zingine za bahari na maziwa kama itavyopendekezwa na Serikali kupitia *TPA* kwa kuzingatia ulinzi na maslahi mapana ya Taifa, na kuwekeza katika vyombo vya usafirishaji wa shehena yaani matishari katika maziwa makuu ili kuunganisha bandari za maziwa makuu na bandari za nchi za jirani kama itavyopendekezwa na *TPA* na kukubaliana na mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa fursa kwa wawekezaji wengine kuwekeza katika maeneo mengine ya bandari nchini kwa lengo la kuleta ushindani, tija na ufanisi, uwekezaji tarajiwa chini ya

mkataba huu hautahusisha maeneo ya Gati Namba 8 hadi 11, yaani Kitengo cha Pili cha Makasha, Gati la Mafuta Kurasini Namba 1 *(KOJ 1),* Gati la Mafuta Kurasini Namba 2 *(KOJ 2),* Boya la Kupokelea Mafuta *(SDM)* na Gati la Kuhudumia Magari katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na maeneo yote ya awamu ya kwanza na ya pili ambayo hayatafikia muafaka katika majadiliano yatakayofanyika baada ya kuridhiwa kwa makubaliano haya. Uwekezaji huo pia hautahusisha Bandari ya Tanga na Bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makubaliano hayo yatatoa haki ya upekee ya kufanya majadiliano kwa awamu ya miradi iliyoainishwa kwenye makubaliano hayo kwa kipindi kisichozidi miezi 12. Msingi wa kutoa haki hii ya kipekee ni kuwezesha pande mbili kufanya majadiliano na kumpa uhakika mwekezaji kujadiliana katika maeneo pasipokuwepo na majadiliano na mwekezaji mwingine katika maeneo hayo hayo. Hivyo, iwapo kipindi hicho kitakwisha bila kufikia makubaliano *TPA* ina uwezo wa kuanzisha majadiliano na wawekezaji wengine katika maeneo hayo pasipo kuwepo kwa mgogoro wowote chini ya makubaliano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda; makubaliano haya yatakuwa hai mpaka pale ambapo shughuli za miradi zitasitishwa au kwisha kwa muda wa mikataba ya nchi mwenyeji na mikataba ya miradi. Msingi wa makubaliano hayo kuendana na mikataba ya miradi ni kutokana na kwamba unaweka msingi unaowezesha kuingia na kutekelezwa kwa mikataba hiyo nchini. Iwapo makubaliano hayo yatakuwa na ukomo kabla ya kuisha mikataba ya miradi iliyo chini ya makubaliano haya utekelezaji wa mikataba ya miradi baada ya kuisha kwa makubaliano hayo itakuwa batili.

Mheshimiwa Spika, vilevile uhai wa makubaliano haya utawezesha kuingiwa kwa mikataba mbalimbali yenye masharti na muda wa ukomo tofauti na ambayo yote inategemea msingi wa uhai wa makubaliano haya. Hivyo, endapo upande mmoja wa makubaliano haya utajitoa athari yake ni kufa au kuvunjika

kwa utekelezaji wa mikataba yote ya miradi iliyoanzishwa chini ya makubaliano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu la ulinzi na usalama katika Bandari ya Dar es Salaam litaendelea kusimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama ambavyo vipo katika maeneo yote ya bandari kwa kuzingatia sheria za nchi na mikataba ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili limezingatiwa pia katika makubaliano haya na kuwekwa bayana kwamba masuala ya ulinzi na usalama hayatakiukwa kwa namna yoyote wakati wa utekelezaji wa shughuli za uwekezaji. Vilevile taasisi zote za Serikali ambazo zinahusika katika shughuli za bandari zitaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ndani ya eneo la bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwepo wa sekta binafsi kutoa huduma katika maeneo ya bandari umeendelea kuwepo na kusimamiwa na Serikali kwa miongo tofauti tofauti. Aidha, katika kipindi chote ambacho sekta binafsi imejihusisha katika uendeshaji wa bandari hakujawahi kujitokeza tukio la kuhatarisha usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwataarifu kwamba, uwepo wa ajira za Watanzania hususan watumishi wa Bandari ya Dar es Salaam ni kipaumbele kikubwa cha Serikali sio tu katika azimio hili, bali kila aina ya uwekezaji ambayo nchi itaufanya. Ibara ya 13 ya makubaliano inaitaka *DP World* kuendeleza ajira za watumishi wote waliopo, kuajiri Watanzania pamoja na kuwaendeleza kitaaluma. *(Makofi)*

Vilevile makubaliano haya yameweka wazi bayana masharti ya Kampuni ya *DP World* kutumia wakandarasi wa ndani katika manunuzi ya huduma na bidhaa pamoja na kusaidia vyuo vya mafunzo vya nchini katika masuala ya elimu ya usafirishaji majini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kueleza manufaa ambayo yanatarajiwa kupatikana iwapo Bunge lako tukufu litaridhia azimio hili la kuwezesha Serikali kuendelea na hatua zinazofuata za majadiliano na Serikali ya Dubai. Baadhi ya manufaa hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Kupunguza muda wa meli kukaa nangani kutoka siku tano kwa sasa mpaka saa 24. Hii itapunguza gharama za utumiaji wa bandari yetu, matokeo yake itaongeza idadi ya meli zitakazokuja Bandari ya Dar es Salaam kutoka meli 1,569 zilizohudumiwa mwaka 2021/2022 mpaka kufikia takribani meli 2,950 itakapofika mwaka 2032/2033. *(Makofi)*

ii. Kupunguza muda wa ushushaji wa makasha kutoka siku 4.5 mpaka siku mbili.

iii. Kupunguza muda wa uondoshaji wa mizigo kutoka saa 12 mpaka saa moja kutokana na uboreshaji wa huduma za mifumo.

iv. Kupunguza gharama ya usafirishaji wa mizigo kutoka nchi za jirani, kutoka nje kwenda nchi za jirani. Kwa mfano, kutoka dola 12,000 mpaka kufikia dola 6,000 au 7,000 kwa kasha moja linalikwenda nchi ya Malawi, Zambia au Kongo. Hii italeta watumiaji wengi sana kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

v. Pia kutakuwa na kuongezeka kwa shehena inayohudumiwa kutoka tani milioni 18.1 za mwaka 2021/2022 hadi kufikia tani milioni 47.57 mwaka 2032/2033 sawa na ongezeko la asilimia 158.

vi. Kuongezeka kwa mapato ya Serikali yanayotokana na kodi ya forodha inayokusanywa kupitia shehena inayopitishwa bandarini kutoka shilingi trilioni 7.76 za mwaka 2021/2022 hadi kufikia shilingi trilioni 26.7 za mwaka 2032/2033 sawa na ongezeko la asilimia 244.

vii. Kuongezeka kwa ajira zinazotokana na shughuli za bandari kutoka 28,990 mwaka 2021/2022 hadi kufikia ajira 71,907 ifikapo mwaka 2032/33 sawa na ongezeko la 178.

viii. Pia kutakuwa na maboresho ya maeneo ya kuhudumia shehena za makasha na kueka mitambo yenye teknolojia ya kisasa.

ix. Pia kuendeleza maeneo ya kuhifadhia mizigo ya bandari kavu kwa kuweka miundombinu ya kisasa ya kuhudumia aina zote za shehena.

x. Pia kutakuwa na maboresho ya magati ya kuhudumia majahazi na abiria, ikiwa ni pamoja na kushawishi uingizaji wa meli kubwa za kitalii zitakazoongeza idadi ya watalii nchini na kuongeza pato la Taifa.

xi. Pia kusimika mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya shughuli za bandari na kuwaunganisha wadau wote. Pia kutakuwa na mafunzo na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa *TPA* katika bandari zote na pia kutakuwa na uanzishwaji wa maeneo maalum ya kiuchumi na viwanda.

xii. Pia kutakuwa na uchocheaji wa ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi zikiwemo sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuchagiza shughuli za viwanda na biashara, kuchagiza ukuaji wa sekta ndogo za usafirishaji kwa njia ya reli na barabara. Watanzania pia, watanufaika na teknolojia na ujuzi wa uendeshaji wa bandari za kisasa na kujenga mahusiano mazuri ya kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, iwapo Bunge lako tukufu litaridhia makubaliano hayo, Serikali itahakikisha wakati wa kuandaa mikataba ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya makubaliano haya masuala muhimu yafuatayo yatazingatiwa:-

i. Mikataba iyakayoandaliwa itawekwa bayana kipindi cha utekelezaji wake na ukomo wake. *(Makofi)*
Mikataba hiyo, itawekewa muda wa marejeo na viashiria muhimu vya ufanisi wa kiutendaji *(key performance indicator)* vitawekwa vizuri. *(Makofi)*

ii. Uandaaji wa mikataba ya miradi utafanywa chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa.

iii. Mikataba itakayoandaliwa italinda ajira za wafanyakazi wazawa na kuwajengea uwezo. *(Makofi)*

iv. Mifumo yote ya TEHAMA itakayosimikwa na *DP World* itasomana na mifumo yote mikuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee tena hapo.

iv. Mifumo yote ya TEHAMA itakayosimkwa na *DP World* itasomana na mifumo mikuu ya Serikali. *(Makofi)*

v. Taasisi mahususi za Serikali zitaendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika maeneo yote ya bandari nchini. *(Makofi)*

vi. Kuhakikisha *DP World* inachukua hatua stahili za masuala ya utafutaji wa masoko ya Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya awali naomba sasa niwasilishe Azimio la Kuridhia Mkataba Baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikiano wa Kimataifa na kijamii wa uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dhima ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuboresha sekta ya bandari nchini ili kuongeza ufanisi na mchango wa sekta hiyo katika mapato ya nchi, ajira na kuchagiza ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi

imeonekena upo umuhimu wa kuendelea kushirikisha sekta binafsi katika shughuli za bandari nchini.

Na kwa kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* tayari ilishasirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za bandari ambao ulikuwa na tija, Serikali imeona ni vyema kuendelea kutafuta wawekezaji wapya wenye uwezo wa kuongeza tija na ufanisi wa bandari zetu ili ziendelee kushindana kikanda katika uhudumiaji wa shehena na kuongeza mchango katika mapato ya Serikali na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Na kwa kuwa kwa vipindi tofauti *TPA* ilipokea na kuchambua mapendekezo ya wawekezaji mbalimbali waliooneshа nia ya kuwekeza katika maeneo ya bandari nchini, iliamua kuingia makubaliano ya awali na kampuni ya *DP World* inayomilikiwa na Serikali ya Dubai mnamo tarehe 28 Februari, 2022 baada ya kudhihirika kwa tija iliyoipata Serikali ya Dubai kupitia Kampuni hiyo ya *DP World* na kusababisha huduma za uchukuzi kupitia bandari kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye pato la Serikali ya Dubai.

Na kwa kuwa makubaliano hayo yalikuwa na lengo la kubainisha maeneo mahususi ya ushirikiano, ili kuboresha uendeshaji wa maeneo ya bandari nchini, kuwekeza katika maeneo yaliyotengwa katika bandari kavu, utunzaji wa mizigo *(logistic park)* na maeneo ya kanda za kibiashara.

Na kwa kuwa Serikali iliona tija ya kuishirikisha kampuni ya *DP World* inayomilikiwa na Serikali ya Dubai kwa asilimia 100 ilianzisha najadiliano na Serikali ya Dubai na kufanikisha kuandaliwa na kuingiwa kwa makubaliano baina ya nchi kwa nchi kwa ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na utendaji wa utendaji kazi wa maeneo ya bandari nchini na ambao ulisainiwa na pande zote mbili tarehe 25 Oktoba, 2022.

Na kwa kuwa Kampuni ya *DP World* ina uzoefu mkubwa katika uendeshaji wa shughuli za bandari Barani Afrika, Asia, Ulaya na Marekani ya Kaskazini na Kusini, kampuni hii pia ina uzoefu na

utaalamu wa kuchagiza mnyororo mzima wa usafisirishaji *(end to end total logistics chain solution)* kutoka maeneo ambayo bidhaa zinatoka mpaka kufika kwa walaji.

Na kwa kuwa kampuni hiyo ina uwezo wa uendeshaji wa maeneo maalum ya kiuchumi karibu na bandari pamoja na usafirishaji bahari na nchi kavu kupitia njia ya reli, uwekezaji katika mitambo na mifumo ya kisasa, uendeshaji wa shughuli za kibandari; pia ina uwezo wa kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya bandari zikiwemo kuwekeza katika mitambo na mifumo ya kisasa ya uendeshaji wa shughuli za kibandari na hivyo kuleta ufanisi; kuwekeza katika mnyororo wa usafirishaji ili kuongeza ufanisi wa bandari; kuwekeza katika vichocheo vya shughuli za kibandari ya zikiwemo maeneo huru ya bandari, maeneo ya kuhifadhia shehena nje ya bandari, miundombinu ya uunganishi wa usafirishaji, kuwekeza katika miundiombinu wezeshi wa bidhaa zinazoharibika na kuwekeza katika kutafuta masoko kutoka nchi zisizo na bandari na kuziunganisha na bandari.

Na kwa kuwa lengo la mkataba huu ni kuweka msingi, kuanzisha majadiliano baina ya Serikali na mwekezaji ili kuwezesha kukubaliana maeneo mahususi ya ushirikiano na kuingia mikataba ya nchi mwenyeji ambayo baada ya kusainiwa itaiwezesha *TPA* kuanza majadiliano na mwekezaji katika maeneo mahususi yatakayokuwa yamekubaliwa katika mikataba ya nchi mwenyeji.

Na kwa kuwa mkataba unalengwa kuridhiwa na unabainisha vipengele muhimu ikiwa ni pamoja:-

i. Ibara ya 2 - Malengo ya Mkataba; Ibara hii inaelekeza kuwa lengo la mkataba huu ni kuweka taratibu wa kisheria wa maeneo ya mashirikiano kwa ajili ya kuendeleza, kuboresha na kuendesha Bandari za Bahari na Maziwa, miundombinu inayoendana na shughuli za bandari kama inavyopendekezwa na Serikali kupitia *TPA* kwa kuzingatia ulinzi na maslahi mapana ya Taifa. Pia maeneo ya mashirikiano yanajumuisha kujengea uwezo, kuhamisha ujuzi,

teknolojia na utaalum, kuimarisha vyuo vya mafunzo na intelijensia ya masoko.

ii. Ibara ya 3 – Usirikiano; Ibara hii inaelekeza kuwa, nchi zitashirikiana kwa lengo la kuanzisha na kuendeleza mazingira muhimu na bora kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za uwekezaji unaolengwa na kuwa wawakilishi wa nchi zetu watakutana kwa lengo la kujadili na kuingia mikataba kwa namna itakavyoonekana inafaa, ili kuwezesha kuanza utekelezaji wa miradi inayokusudiwa. Ibara hii pia inaanzisha Kamati ya Ushauri ambayo ina jukumu la kuratibu shughuli za utekelezaji wa makubaliano husika na kuhakikisha kunakuwepo na utaratibu wa kubadilishana taarifa kuhusu malengo ya uwekezaji unaokusudiwa.

iii. Ibara ya 4 - Mawanda ya Ushirikiano na Taasisi za Utekelezaji; Ibara hii inafafanua kuwa mawanda ya makubaliano haya ni kuwezesha utekelezaji wa ushirikiano kama ilivyoainishwa katika kiambatanisho cha kwanza cha mkataba. Kiambatanisho hicho kimeainisha maeneo ya ushirikiano yatakayotekelezwa kwa awamu mbili, Serikali ya Tanzania inasisitiza kuwa *TPA* ndio yenye jukumu la kutekeleza maeneo ya ushirikiano kuhusu makubaliano haya na kwa upande wa Serikali ya Dubai, *DP World* na washirika wake ndio zitakuwa taasisi za utekelezaji.

Pamoja na ushirikiano huo nchi yetu itakuwa na haki ya kuitaarifu Serikali ya Dubai kuhusu fursa nyingine za uwekezaji katika maeneo ya bandari, maeneo huru, ili kuwezesha taasisi za Dubai kuwasilisha mapendekezo ya uwekezaji katika maeneo hayo.

Kuhusu uwekezaji huu, *DP World* na washirika wake ndio watakuwa na jukumu la kutafuta fedha kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za uwekezaji.

iv. Ibara ya 5 - Haki za Kuendeleza, Kusimamia na Kuendesha; Ibara hii inaeleza kuwa *DP World* itapewa jukumu la kuendeleza, kusimamia na kuendesha maeneo ya kipaumbele ya uwekezaji kama itakavyokubaliwa kupitia mikataba mahususi ya nchi mwenyeji. Jukumu hili ni kwa kipindi mahususi cha miezi 12 kuanzia tarehe ya kusainiwa kwa mkataba huu yaani tarehe 25 Oktoba, 2022 na baada ya kuisha kipindi hicho *TPA* itakuwa na haki ya kuwasikiliza wawekezaji wengine katika maeneo ya uwekezaji wa kipaumbele.

v. Ibara ya 8 - Haki ya Ardhi; Ibara hii inaitaka Serikali ya Tanzania kuhakikisha hatua muhimu zinachukuliwa ili kuwezesha *DP World* kupata haki ya matumizi ya ardhi na sio umiliki wa ardhi kwa lengo la kutekeleza miradi itakayokubaliwa kupitiwa mikataba ya nchi mwenyeji. Serikali italinda haki za usalama wa umiliki wa ardhi na kubaki katika mikono ya Watanzania kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi za kutoa na kutumia ardhi kwa wawekezaji na kuhakikisha haki hizo zinabaki hai katika kipindi cha utekelezaji wa miradi tu.

Aidha, katika kutekeleza haki za ardhi Serikali itahakikisha haki hizo zinatambulika, zinasajiliwa, hazina madai yoyote na zinatolewa kwa kampuni itakayotekeleza mradi kwa kuzingatia taratibu na sheria za nchi kwa kipindi cha upangishaji au utekelezaji wa mradi husika tu.

vi. Ibara ya 9 - Motisha za Uwekezaji; Ibara hii inaelekeza kuwa uwekezaji wa *DP World* utakuwa mkubwa na utaleta manufaa ya kiuchumi na kijamii, hivyo utahitaji kutolewa motisha za uwekezaji. Hivyo, pande mbili zilikubaliana kutoa motisha za uwekezaji kwa kuzingatia sheria za nchi na taratibu mahususi za Tanzania, kama itakavyoainishwa zaidi katika mikataba ya nchi mwenyeji.

vii. Ibara ya 12 - Ulinzi na Usalama; Ibara hii inaelekeza kuwa utekelezaji wa shughuli za miradi hautaathiri au kukiuka masuala ya ulinzi na usalama ikiwemo ardhi ya mradi, mifumo ya miundombinu ya juu na ya chini ya eneo la bandari, mitambo iliyosimikwa pamoja na masuala mengine ya usalama ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama atakavyokubaliwa chini ya mkataba wa nchi mwenyeji.

viii. Ibara ya 13 - Ushiriki wa wazawa, ajira na majukumu kwa jamii; Ibara hii inaelekeza kuwa mikataba itakayosainiwa ya utekelezaji wa miradi ni lazima iainishe mpango wa ushirikishaji wa wazawa katika utekelezaji wa miradi husika, majukumu kwa jamii, uendelezaji wa ajira zilizopo, kutoa ajira mpya kwa Watanzania na kuwapatia mafunzo kuhusiana na utekelezaji wa miradi husika. *(Makofi)*

ix. Ibara ya 18 - Kodi, tozo na ushuru nyinginezo; Ibara hii inaelekeza kuwa kodi, ushuru na tozo nyinginezo zitakusanywa katika utekelezaji wa mradi kwa kuzingatia sheria za kodi zilizopo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia Ibara hii inaelekeza kuwa motisha za uwekezaji, misamaha ya kodi ama tozo nyingine zitatolewa kwa kuzingatia msingi wa sheria za kodi zilizopo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama itakavyokubaliwa katika mkataba wa nchi mwenyeji na mikataba ya utekelezaji wa miradi kwa kuzingatia sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

x. Ibara ya 19 - Kurithiwa kwa nchi; Ibara hii inaelekeza kuwa iwapo nchi itabadilika ama kuungana na nchi nyingine au zingine, nchi ambayo itarithi majukumu itachukuliwa kuwa ni sehemu ya makubaliano haya kutokea tarehe ya kurithiwa kwa nchi husika au kwa kuzingatia kuwa nchi inayorithi majukumu itatoa taarifa

kwa upande mwingine kuhusu nia yake ya kuwa sehemu ya makubaliano haya.

xi. Ibara ya 20 - Utatuzi wa migogoro; Ibara hii inaelekeza kuwa utaratibu wa utatuzi wa migogoro uliopendekezwa chini ya makubaliano haya ni kuanza kutumika kwa makubaliano *(amicable settlement)* kupitia njia za kidiplomasia au kupitia kamati ya ushauri ya makubaliano hayo, na kama mgogoro hautatatuliwa ndani ya siku 90, upande usioridhishwa unaweza kutangaza kuwepo mgogoro *(to declare dispute)*. Pale ambapo kutakuwa na mgogoro, utaratibu wa usuluhishi ni kupitia Baraza la Usuluhishi chini ya Kanuni ya Usuluhishi za Kimataifa. Sehemu iliyokubaliwa kuwa mgogoro utasikilizwa ni Johannesburg, Afrika Kusini na lugha ya usuluhishi ni ya Kiingereza.

xii. Ibara ya 21 - Sheria zinazosimamia mkataba; Ibara hii imeweka msisitizo kuwa sheria itakayosimamia mkataba wa nchi mwenyeji na mikataba ya utekelezaji wa miradi zitakuwa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

xiii. Ibara ya 22 - Marekebisho ya makubaliano; Ibara hii inafafanua kuwa makubaliano haya yanaweza kurekebishwa muda wowote kwa upande mmoja kuwasilisha nia ya kurekebisha masharti ya makubaliano kwa upande mwingine kwa njia ya maandishi na kukubaliwa kwa marekebisho hayo kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

xiv. Ibara ya 23 - Muda wa makubaliano na usitishwaji; Ibara hii inaeleza kuwa makubaliano haya yatakuwa hai mpaka itakapotokea moja ya masuala mawili; kwanza, usitishwaji wa shughuli za uwekezaji au kumalizika kwa muda wa mkataba wa nchi mwenyeji.

Pale ambapo moja ya mkataba wa nchi mwenyeji itakapositishwa kabla ya kipindi chake kumalizika, makubaliano haya yataendelea kuwa hai. Aidha, haki na wajibu wa pande mbili za makubaliano haya zitatambuliwa kwa mujibu wa makubaliano husika.

xv. Ibara ya 25 - Kuanza kutumika kwa makubaliano haya; Ibara hii inaeleza kuwa mara baada ya kusainiwa kwa makubaliano haya pasipo kujali majukumu mengine, pande mbili za makubaliano haya zitachukua hatua stahili kuhakikisha shughuli za awali za miradi zinaanza kutekelezwa kwa mujibu wa sheria za nchi.
Pia ndani ya siku 30 kutoka tarehe ya kusainiwa kwa makubaliano haya, nchi washiriki zitaanzisha mchakato wa kuridhiwa na mamlaka husika ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya nchi katika makubaliano haya kwa mujibu wa sheria za kimataifa. Pia makubaliano haya yataanza kutekelezwa baada ya kubadilishana kwa hati za uridhiaji kwa mujibu wa sheria za nchi husika.

xvi. Ibara ya 30 - Mazingira ya kisheria kutokubadilika; Ibara hii inaelekeza kuwa mfumo wa sheria na mazingira yake kuhusu miradi yatakuwa tulivu katika hali ambayo inaridhisha kwa pande zote. Utulivu huo utaanza tarehe ya kusainiwa kwa makubaliano haya. Pia katika ibara hii, Tanzania imetakiwa kuchukua hatua stahili ili kuwezesha makubaliano haya yaweze kutekeleza mikataba ya miradi na mikataba ya nchi mwenyeji.

xvii. Ibara ya 31 - Kubadilisha hati za uridhiaji; Ibara hii inaelekeza kuwa makubaliano na hati za uridhiaji zitabadilishwa ndani ya pande mbili za makubaliano. Na kwa kuwa mkataba huu una manufaa mbalimbali ambayo ni pamoja na kama ifuatavyo: -

(i) Kupunguza muda wa meli kukaa nangani kutoka siku tano kwa sasa mpaka saa 24. Hii itapunguza gharama za utumiaji wa bandari yetu, matokeo

yake itaongeza idadi za meli zitakazokuja ndani ya Bandari ya Dar es Salaam kutoka 1,569 zinaohudumiwa mwaka 2021/2022 mpaka kufikiwa takribani meli 2,950 ifikapo mwaka 2032/2033. *(Makofi)*

(ii) Kupunguza muda wa ushushaji wa makontena kutoka siku 4.5 mpaka kufikia siku tatu.

(iii) Kupunguza muda wa uondoshaji mizigo kutoka saa 12 za sasa mpaka kufikia saa moja kutokana na uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA.

(iv) Kupunguza gharama ya usafirishaji wa shehena kutoka nchi za nje kwenda nchi za jirani, kwa mfano kutoka dola 12,000 mpaka kufikia dola 6,000 na 7,000 kwa kasha moja linalokwenda nchi ya Malawi, Zambia au Congo. Hii italeta watumiaji wengi sana kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam.

(v) Kuongezeka kwa shehena inayohudumiwa kutoka tani milioni 18.41 za mwaka 2021/2022 hadi kufikia tani 47.57 mwaka 2032/2033 sawa na ongezeko la asilimia 158.

(vi) Kuongezeka kwa mapato ya Serikali yanayotokana na kodi ya forodha inayokusanywa katika shehena inayopitishwa bandarini kutoka shilingi trilioni 7.76 za mwaka 2021/2022 hadi kufikia shilingi trilioni 26.70 za mwaka 2032/2033 sawa na ongezeko la asilimia 244. *(Makofi)*

(vii) Kuongezeka kwa ajira zinazotokana na shughuli za bandari kutoka 27,999 mwaka 2021/2022 hadi kufikia ajira 71,907 ifikapo mwaka 2032/2033 sawa na ongezeko la asilimia 148.

(viii) Kuwepo na maboresho ya magati ya kuhudia majahazi na abira ikiwa ni pamoja na kushawishi uingiaji wa meli kubwa za kitalii zitakazoongeza idadi ya watalii nchini na kuongeza Pato la Taifa.

(ix) Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa *TPA* katika bandari zote hapa nchini. *(Makofi)*

(x) Uanzishwaji wa maeneo huru ya kiuchumi na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi zikiwemo sekta za kilimo, mifugo na uvuvi; utalii, viwanda na biashara.

(xi) Mwisho, kuchagiza ukuaji wa sekta ndogo za usafirishaji kwa njia ya reli na barabara na kujenga mahusiano mazuri ya kidiplomasia.

Hivyo basi, kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itayapata kutokana na makubaliano haya, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi katika Bandari za Tanzania *(The Inter-Governmental Agreement between The United Republic of Tanzania and The Emirate of Dubai concerning economic and social partnership for the development and improving performance of sea and lake ports in Tanzania)*.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**10 JUNI, 2023**

## MAELEZO YA AWALI KUHUSU MAPENDEKEZO YA KURIDHIA MKATABA BAINA YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA SERIKALI YA DUBAI KUHUSU USHIRIKIANO WA KIUCHUMI NA KIJAMII KWA AJILI YA UENDELEZAJI NA UBORESHAJI WA UTENDAJI KAZI WA BANDARI TANZANIA - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

### A: UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) ilianzishwa kupitia Sheria Na. 17 ya mwaka 2004. Mamlaka hii ilirithi na kuchukua majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania (Tanzania Harbors Authority-THA) iliyoanzishwa kupitia Sheria ya Mamlaka ya Bandari Na. 12 ya mwaka 1977 baada ya kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupewa majukumu zaidi ya kumiliki, kuendesha na kuendeleza bandari zilizopo pwani ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria hiyo ya Bandari Na. 17 ya Mwaka 2004 inaipa TPA majukumu ya kumiliki, kusimamia, kuendesha na kuendeleza maeneo yote ya bandari Tanzania Bara. Madhumuni makuu ya kuanzishwa kwa TPA yameainishwa katika Kifungu cha (5) cha Sheria hiyo ambayo ni kuhakikisha Tanzania inaendelea kunufaika na faida ya kijiografia ikiwemo: kuchagiza usimamizi bora na ufungamanishaji wa tija wa bandari zilizopo pwani ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu; kuhakikisha kunakuwa na tija katika huduma zinazotolewa za upakiaji na ushushaji wa mizigo pamoja na abiria; kuendeleza, kuboresha na kusimamia miundombinu ya kibandari; kusimamia usalama wa bandari; na kuingia mikataba au makubaliano na mtu au taasisi yoyote kwa ajili ya utoaji wa huduma za bandari.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwekeza kwenye bandari zake kwa vipindi tofauti kwa kutumia vyanzo vyake na fedha za mikopo katika kutekeleza mikakati kwa lengo la kuboresha sekta ya bandari nchini. Mkakati uliochukuliwa hivi karibuni ni utekelezaji wa Mradi mkubwa wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam *(Dar es Salaam Maritime Gateway*

*Project – DMGP)* ambao umehusisha: uimarishaji na uongezaji wa kina cha Gati Na. 1-7; ujenzi wa gati jipya la kuhudumia magari; na uongezaji wa kina cha lango la kuingia bandarini. Uzoefu umeonesha kuwa uwekezaji wa namna hii una faida kubwa kwa nchi iwapo bandari itaendeshwa kwa tija na ufanisi mkubwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuchukua hatua mbalimbali za maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam, bado ufanisi katika utoaji huduma za bandari haujafikia viwango vinavyotakiwa kimataifa. Hali ya sasa ya utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam imeendelea kuwa ya kiwango cha chini ikilinganishwa na bandari shindani kikanda. Kwa mfano, wastani wa meli kusubiri nangani kwa Bandari ya Dar es salaam ni siku 5 ikilinganishwa na siku 1.25 kwa Bandari ya Mombasa na siku 1.6 kwa Bandari ya Durban. Ufanisi mdogo wa Bandari ya Dar es Salaam umetokana na changamoto mbalimbali zikiwemo: kukosekana kwa mifumo ya kisasa ya TEHAMA; kutokuwepo kwa maeneo ya kutosha ndani na nje ya bandari kwa ajili ya kuhifadhia shehena pamoja na maegesho ya meli; na kukosekana kwa mitambo ya kutosha na ya kisasa ya kuhudumia shehena ambayo teknolojia yake inabadilika mara kwa mara na ina gharama kubwa ya uwekezaji na uendeshaji.

5. ***Mheshimiwa Spika***, athari za kutokuwa na ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na: meli kusubiri muda mrefu nangani ambako kunasababisha kuongezeka kwa gharama ya kutumia bandari ya Dar es Salaam, kwa mfano gharama za meli kusubiri nangani kwa siku moja ni takriban Dola za Marekani 25,000, sawa na takriban Shilingi milioni 58 kwa siku; meli kutumia muda mrefu kupakia na kupakua shehena gatini kwa wastani wa siku 5 ikilinganishwa na siku 1 inayokubalika kimataifa; meli kubwa kutokuja katika bandari ya Dar es Salaam kutokana na kuchukua muda mrefu kuhudumiwa. Hali hii husababisha bandari yetu kuwa bandari inayolishwa shehena na bandari zingine (feeded port) na hivyo kuongeza gharama ya kutumia bandari hiyo na kuikosesha nchi mapato ambayo yangeweza kutumika katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati nchini ambayo

ingesaidia kukuza uchumi na kuboresha huduma za wananchi. Pia, kunaongeza gharama katika mnyororo mzima wa usafirishaji *(total route costs)* kutoka nje ya nchi, kupitia katika bandari yetu kwenda nchi za jirani zinazotumia bandari hiyo. Kwa mfano, gharama ya kusafirisha kasha moja kutoka nje ya nchi (on transit) kwenda nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zinafikia takriban Dola za Marekani kati ya 8,500 hadi 12,000. Hii ni gharama kubwa sana ikilinganishwa na Bandari shindani.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua kuwa Serikali pekee haitaweza *kutatua* changamoto zilizopo kwenye Bandari ya Dar es salaam, kuanzia miaka ya 2000, Serikali ya Awamu ya Tatu kupitia Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) iliingia mkataba wa upangaji na uendeshaji *(lease and concession agreement)* na Kampuni ya Kimataifa ya Uendeshaji wa Vitengo vya Makasha, Hutchison ya Hong-Kong China. Mkataba huo ulidumu kwa miaka ishirini na mbili (22) kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2022 na uliipa haki ya kipekee Kampuni hiyo kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuhudumia makasha katika gati namba 8 hadi 11 za Bandari ya Dar es Salaam. Wakati huo huo TPA ikiendesha na kuhudumia maeneo mengine ya Bandari hiyo.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutatua changamoto za Bandari zilizopo na kwa kuzingatia dhima ya Serikali ya kuboresha Sekta ya Bandari nchini ili kuongeza ufanisi na mchango wa Sekta ya Bandari katika mapato ya nchi, ajira na kuchagiza sekta nyingine za kiuchumi, Serikali ilifanya maamuzi ya kutafuta Wawekezaji wapya wanao endana na dhima ya Serikali. Hatua hizo zilihusisha kupokea mapendekezo ya Wawekezaji mbalimbali wakiwemo kampuni ya Hutchson (Hong Kong), Antewerp/Brugge (Belgium), PSA International (Singapore), DP World (Dubai), Abu Dhabi Ports (Abu Dhabi), Adani Ports and Logistics (Mundra-India), Kampuni ya CMA-CGM (France) pamoja na Kampuni ya Maersk (Denmark). Lengo kuu ni kufungua masoko ya kimkakati katika eneo la bidhaa na biashara ya usafirishaji ndani ya nchi na kanda zinazotuzunguka.

8. ***Mheshimiwa Spika***, katika kupitia mawasilisho ya kampuni hizo pamoja na sifa zao kimataifa, Serikali iliamua kuanzisha majadiliano na kampuni ya DP World kwa kuzingatia uzoefu wake katika uendeshaji wa shughuli za bandari barani Afrika, Asia, Ulaya na Amerika ya Kaskazini na Kusini. Kampuni hii ina uzoefu na utaalamu wa kuchagiza mnyororo mzima wa usafirishaji *(end to end total logistics chain solution)* kutoka maeneo ambayo bidhaa zinatoka mpaka kufika kwa Walaji. Uendeshaji wa maeneo maalum ya kiuchumi (special economic zones) karibu na bandari, usafirishaji baharini na nchi kavu (kupitia njia ya reli), uwekezaji mkubwa katika maeneo mbalimbali ambayo imewekeza na pamoja kuajiri Wazawa katika maeneo hayo. Aidha, kwa upande wa makampuni mengine ambayo TPA ilipokea mapendekezo yao, yalionesha nia ya kuwekeza bandarini pekee na sio kuchagiza mnyororo mzima wa usafirishaji. Pia, baadhi ya makampuni hayo hayana uzoefu wa kuendesha shughuli za bandari barani Afrika wakati Kampuni ya DP World inaendesha takriban bandari sita (6) barani Afrika na bandari zaidi ya 30 duniani kote kwa ufanisi mkubwa.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia nia ya Serikali kuvutia uwekezaji nchini, wakati wa maonesho ya Dubai Expo 2020 tarehe 28 Februari, 2022 Hati za Makubaliano takriban 30 zilisainiwa baina ya Taasisi za Serikali ya Tanzania na Sekta binafsi na Taasisi za Serikali za Dubai kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini ili kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Moja kati ya Hati ya Makubaliano hayo ni baina ya TPA na DP World iliyolenga kuanzisha ushirikiano wa uboreshaji, uendeshaji na uendelezaji wa maeneo ya bandari nchini.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufanikisha utekelezaji wa Hati ya Makubaliano hayo, Serikali iliteua Timu ya Wataalam ambayo ilipewa jukumu la kufanya majadiliano na Wataalam wa Serikali ya Dubai na kufanikisha kuandaliwa na kusainiwa kwa Mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kwa mujibu wa taratibu zilizopo. Mkataba huo ni kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa

ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa bandari Tanzania.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la Mkataba huu ni kuweka msingi wa makubaliano (framework agreement) baina ya nchi na nchi ili kuwezesha kuanza kufanyika kwa majadiliano na kuingiwa kwa mikataba mbalimbali (Mikataba ya Nchi Mwenyeji, Upangishaji na Uendeshaji) ya uwekezaji na uendeshaji wa maeneo ya bandari nchini.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa masharti ya Mkataba huo unapaswa kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ili utekelezaji wake uweze kuanza. Hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilianzisha mchakato wa kupata ridhaa ya Serikali ya kuwasilisha Mkataba huu Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa.

**B: UFAFANUZI KUHUSU MKATABA WA IGA**

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mujibu wa Ibara ya 2 ya Mkataba wa IGA, lengo lake ni kuweka msingi wa ushirikiano baina ya Serikali mbili kwa maeneo mahsusi yaliyoainishwa ndani ya Mkataba husika (Rejea Appendix 1 ya Mkataba) ambayo utekelezaji wake utafanyika kupitia Mikataba Mahsusi baina ya taasisi zilizoainishwa katika Mkataba wa IGA kama taasisi tekelezi ambazo ni TPA na DP World. Hivyo, Mkataba huu hauna masharti yanayoifunga Serikali kuhusu maeneo ya ushirikiano yaliyoanishwa pasipo uwepo wa Mikataba Mahsusi wa utekelezaji wa miradi itayojadiliwa na kukubaliwa na pande mbili.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Mawanda ya uwekezaji chini ya Mkataba huu yatahusisha uendelezaji na uendeshaji wa baadhi ya maeneo ya Bandari na sio bandari yote kwa ujumla wake. Aidha, uendelezaji na uendeshaji huo utafanyika kupitia Mikataba Mahsusi ya Miradi *(Project Agreements)* ambayo itajadiliwa na kuingiwa kwa kila eneo la ushirikiano na

itahusisha matumizi ya ardhi pekee na sio umiliki wa ardhi ikiwa ni pamoja na Serikali kuhakikisha kuwa Sheria, kanuni na taratibu za nchi zinazolinda umiliki ya ardhi ya Watanzania zinazingatiwa na kusimamiwa ipasavyo.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkataba huu umeainisha **Awamu kuu mbili** za maeneo ya ushirikiano. **Awamu ya kwanza** itajumuisha: kusimamia, kuendesha na kuendeleza baadhi ya Magati katika Bandari ya Dar es Salaam; kuboresha Gati la Majahazi na Gati la Abiria katika Bandari ya Dar es Salaam ili kuvutia vyombo vikubwa zaidi na meli za kitalii kutia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam; kuwekeza katika maeneo yaliyotengwa katika Bandari Kavu; kufanya uwekezaji katika Mifumo ya Kisasa ya TEHAMA ya kuendeshea shughuli za kibandari ili kuongeza ufanisi wa Bandari kuwa shindani; na kuwajengea uwezo Watumishi wa TPA ili waweze kutekeleza shughuli za Bandari kwa ufanisi katika maeneo mengine ya Bandari Nchini. Msisitizo wa Serikali ni kuhakikisha maeneo yote ya nchi yanabaki chini ya umiliki wa Serikali.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Awamu ya Pili ya Miradi (Phase II), majadiliano yatafanyika kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo: kuongeza thamani ya bidhaa; maeneo ya viwanda na miundombinu mingine itakayoongeza ufanisi katika usafirishaji wa bidhaa kwenda na kutoka nchi zinazotuzunguka; kuwekeza katika Bandari zingine za Bahari na Maziwa kama itavyopendekezwa na Serikali kupitia TPA kwa kuzingatia ulinzi na maslahi mapana ya Taifa; na kuwekeza katika vyombo vya usafirishaji wa shehena (matishari) katika maziwa makuu ili kuunganisha bandari za Maziwa Makuu na bandari za nchi jirani kama itakavyopendekezwa na TPA na kukubaliana na Mwekezaji.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kutoa fursa kwa Wawekezaji wengine kuwekeza katika maeneo mengine ya bandari nchini kwa lengo la kuleta ushindani, tija na ufanisi, uwekezaji tarajiwa chini ya Mkataba huu hautahusisha maeneo ya Gati namba 8 hadi 11 (Kitengo Na. 2 cha Makasha), Gati la Mafuta Kurasini Na. 1 (KOJ 1), Gati la Mafuta Kurasini Na. 2 (KOJ2), Boya la

Kupokelea Mafuta (SBM) na Gati la Kuhudumia Magari katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na maeneo yote ya Awamu ya Kwanza na Pili ambayo hayatafikia muafaka katika majadiliano yatakayofanyika baada ya kuridhiwa kwa IGA. Uwekezaji huo pia, hautahusisha Bandari ya Tanga na Mtwara.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkataba huu unatoa haki ya upekee ya kufanya majadiliano kwa Awamu ya Miradi iliyoanishwa kwenye Mkataba huo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili (12). Msingi wa kutoa haki hii ya kipekee ni kuwezesha pande mbili kufanya majadiliano na kumpa uhakika Mwekezaji kujadiliana katika maeneo pasipo kuwepo kwa majadiliano na Mwekezaji mwingine katika maeneo hayo hayo. Hivyo, iwapo kipindi hicho kitakwisha bila kufikia makubaliano, TPA inaweza kuanzisha majadiliano na Wawekezaji wengine katika maeneo hayo pasipo kuwepo kwa mgogoro wowote chini ya Mkataba huo.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Kuhusu muda, Mkataba huu utakuwa hai mpaka pale ambapo shughuli za miradi zitasitishwa au kuisha kwa muda wa mikataba ya nchi mwenyeji na mikataba ya miradi. Msingi wa Mkataba huu kuendana na mikataba ya miradi ni kutokana na kwamba unaweka msingi unaowezesha kuingia na kutekelezwa kwa mikataba hiyo nchini. Iwapo Mkataba huu utakuwa na ukomo kabla ya kuisha mikataba ya miradi iliyo chini ya Mkataba huu, utekelezaji wa mikataba ya miradi baada ya kuisha kwa mkataba huu itakuwa batili. Vile vile, uhai wa Mkataba huu utawezesha kuingiwa kwa mikataba mbalimbali yenye masharti na muda wa ukomo tofauti na ambayo yote inategemea msingi wa uhai wa mkataba huu. Hivyo, endapo upande mmoja wa mkataba huu utajitoa, athari yake ni kufa au kuvunjika kwa utekelezaji wa mikataba yote ya miradi iliyoanzishwa chini ya Mkataba huu.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu la Ulinzi na Usalama katika Bandari ya Dar es Salaam litaendela kusimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia vyombo vyake vya Ulinzi na Usalama ambavyo vipo katika maeneo yote ya Bandari kwa

kuzingatia Sheria za nchi na mikataba ya kimataifa. Suala hili limezingatiwa pia katika Mkataba wa IGA na kuwekwa bayana kwamba masuala ya Ulinzi na Usalama hayatakiukwa kwa namna yeyote wakati wa utekelezaji shughuli za uwekezaji. Vilevile, taasisi zote za Serikali ambazo zinahusika katika shughuli za bandarin zitaendelea kutekeleza majukumu yao kwa mujibu Sheria ndani ya eneo la bandari. Uwepo wa sekta binafsi kutoa huduma katika maeneo ya bandari umeendelea kuwepo na kusimamiwa na Serikali kwa miongo tofauti tofauti. Aidha, katika kipindi chote ambacho Sekta Binafsi imehusishwa katika uendeshaji wa bandari, hakujawahi kujitokeza tukio la kuhatarisha usalama wa nchi.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuwataarifu kwamba, uwepo wa ajira za Watanzania hususan watumishi wa bandari ya Dar es Salaam ni kipaumbele kikubwa cha Serikali sio tu katika Azimio hili bali katika kila aina ya uwekezaji ambao nchi itaufanya. Ibara ya 13 ya Mkataba huu inaitaka DP World kuendeleza ajira za Watumishi wote waliopo, kuwaajiri Watanzania pamoja kuwaendeleza kitaaluma. Vilevile, Mkataba huu umeweka bayana sharti kwa Kampuni ya DP World kutumia Wakandarasi wa ndani katika manunuzi ya huduma na bidhaa pamoja na kusaidia Vyuo vya mafunzo vya Tanzania katika masuala ya elimu ya usafirishaji majini.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuchukua fursa hii kuelezea manufaa ambayo yanatarajiwa kupatikana iwapo Bunge letu Tukufu litaridhia Azimio hili na kuwezesha Serikali kuendelea na hatua zinazofuata za majadiliano na Serikali ya Dubai. Baadhi ya manufaa yatakayopatikana ni pamoja na:

i. Kupunguza muda wa meli kukaa nangani kutoka siku 5 kwa sasa mpaka masaa 24. Hii itapunguza gharama za utumiaji wa Bandari yetu. Matokeo yake itaongeza idadi ya meli zitazokuja Bandari ya Dar es Salaam kutoka meli 1,569 zilizohudumiwa mwaka 2021/22 mpaka kufikia takriban meli 2,950 ifikapo mwaka 2032/33;

ii. Kupunguza muda wa ushushaji wa makontena kutoka siku 4.5 mpaka siku 2;

iii. Kupunguza muda wa uondoshaji mizigo kutoka masaa 12 mpaka saa 1 kutokana na uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA;

iv. Kupunguza gharama ya usafirishaji wa mizigo kutoka nchi za nje kwenda nchi za Jirani, kwa mfano kutoka US$ 12,000 mpaka kati ya US$6,000 na US$7,000 kwa kasha linalokwenda nchi ya Malawi, Zambia au DRC. Hii italeta Watumiaji wengi kwenye Bandari ya Dar es Salaam;

v. Kuongezeka kwa shehena inayohudumiwa kutoka tani milioni 18.41 za mwaka 2021/22 hadi kufikia tani milioni 47.57 mwaka 2032/33, sawa na ongezeko la asilimia 158;

vi. Kuongezeka kwa Mapato ya Serikali yatokanayo na Kodi ya Forodha inayokusanywa katika shehena inayopitishwa bandarini kutoka Shilingi Trilioni 7.76 za mwaka 2021/22 hadi Shilingi Trilioni 26.7 za mwaka 2032/33, sawa na ongezeko la asilimia 244;

vii. Kuongezeka kwa ajira zinazotokana na shughuli za bandari kutoka 28,990 mwaka 2021/22 hadi ajira 71,907 ifikapo mwaka 2032/33, sawa na ongezeko la asilimia 148;

vii. Maboresho ya maeneo ya kuhudumia shehena ya makasha na kuweka mitambo yenye Teknolojia ya kisasa;

viii. Kuendeleza eneo la kuhifadhia mizigo la Bandari Kavu kwa kuweka miundombinu ya kisasa ya kuhudumia aina zote za shehena;

ix. Maboresho ya magati ya kuhudumia Majahazi na Abiria ikiwa ni pamoja na kushawishi uingiaji wa meli kubwa za kitalii zitakazo ongeza idadi ya Watalii nchini na kuongeza pato la Taifa;

x. Kusimika Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya shughuli za bandari na kuwaunganisha wadau wake;

xi. Mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa TPA katika Bandari zote (knowledge and skills transfer);

xii. Uanzishwaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi/Viwanda; na

xiii. Kuchochea ukuaji wa sekta zingine za kiuchumi zikiwemo Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; kuchagiza shughuli za Viwanda na Biashara; kuchagiza ukuaji wa sekta ndogo za usafirishaji kwa njia ya reli (SGR, TAZARA na MGR) na barabara; Watanzania kunufaika na teknolojia na ujuzi wa uendeshaji wa bandari kisasa; na kujenga mahusiano ya kidiplomasia.

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, iwapo Bunge lako litaridhia Mkataba huu, Serikali itahakikisha wakati wa kuandaa Mikataba ya Utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mkataba huu masuala muhimu yafuatayo yatazingatiwa:

i. Mikataba itakayoandaliwa itaweka bayana kipindi cha utekelezaji wake na ukomo, muda wa marejeo na viasharia muhimu vya ufanisi wa kiutendaji (key performance indicators);

ii. Uandaaji wa mikataba ya miradi utafanywa chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa;

iii. Mikataba itakayoandaliwa italinda ajira za Wafanyakazi Wazawa na kuwajengea uwezo; iv.

Mifumo yote ya TEHAMA itakayosimikwa na DP World inasomana na Mifumo ya Serikali;

iv. Taasisi mahsusi za Serikali zitaendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika maeneo yote ya bandari; na

v. Kuhakikisha DP World anachukua hatua stahiki za masuala ya utafutaji wa masoko ya Bandari ya Dar es Salaam.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo haya ya awali naomba sasa niwasilishe Azimio la kuridhia Kuridhia Mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu Ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii ya Uendelezaji na Uboreshaji wa Utendaji Kazi wa Bandari Tanzania.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa nimuite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambaye anakuja kuwasilishwa kwa niaba ya Kamati ya Pamoja, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU K.n.y. KAMATI YA PAMOJA:** Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya Kamati ya Pamoja kuhusu Azimio la Bunge kuridhia makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa Bandari Tanzania wa mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Pamoja kuhusu Azimio la Bunge kuridhia makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa

Bandari Tanzania la mwaka 2023. Maoni haya yanawasilishwa Bungeni kufuatia uamuzi wako wa busara wa kuunda Kamati ya Pamoja itokanayo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kwa mujibu wa Kanuni 143(1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba uamuzi wa kuunda Kamati ya Pamoja ni mwendelezo wa jitihada zako za dhati za kuhakikisha kwamba masuala muhimu ya Kitaifa yanayogusa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge…

Mheshimiwa Mwenyekiti, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe sana, azimio hili limeletwa na Serikali, sasa yanasomwa maoni ya Kamati zetu ambazo zimefanya kazi kwa niaba yetu. Sasa sijajua mtakuwa mnachangia nini kama hamumsikilizi Mwenyekiti na ninyi hamkuwa Wajumbe wa Kamati hii, ndiyo mtaanza kuleta hapa michango ya kutoka huko mitandaoni badala ya ambayo Kamati imefanyia kazi. *(Makofi)*

Niwaombe sana, kama ni lazima kuzungumza kwa sauti ya juu, milango iko mingi, toka nje, nenda kazungumze, waache wanaotaka kusikiliza na kuchangia ambayo Kamati iansema wasikilize. Tupunguze sauti, kama ni lazima uzungumze kwa sauti kubwa nenda nje, milango iko mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU K.n.y. KAMATI YA PAMOJA:** Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba uamuzi wa kuunda Kamati ya Pamoja ni mwendelezo wa jitihada zako za kuhakikisha kwamba masuala muhimu ya Kitaifa ambayo yanagusa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu yanapewa uzito unaostahili na kufanyiwa uchambuzi wa kina ili Bunge liweze kutoa uamuzi sahihi na wenye manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wako huu ni mwendelezo wa jitihada zako za kuhakikisha kwamba Bunge kwa niaba ya wananchi linatekeleza wajibu wake ipasavyo wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Pamoja naomba nitumie fursa hii kukupongeza kwa dhati kabisa kwa namna ambavyo umelisimamia jambo hili katika mchakato wake wote hadi kufikia hatua hii ambapo Taarifa ya Kamati ya Pamoja inawasilishwa ili Bunge lako tukufu lifanye uamuzi kwa hoja iliyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyofanya kazi; baada ya kupokea maelekezo ya kulishughulikia jambo hili kwa mujibu wa Kanuni ya 108(1) na (2), Kamati ya Pamoja ilianza kazi yake mara moja na kufanya yafuatayo: -

a) Kufanya uchambuzi wa awali na baadae kupokea Maelezo ya Serikali kuhusu Mapendekezo ya Azimio la kuridhia makubaliano husika siku ya Jumatatu tarehe 05 Juni, 2023;

b) Kupokea na kuchambua maoni ya wadau yaliyowasilishwa mbele ya Kamati siku ya Jumanne tarehe 06 Juni, 2023. Aidha, Kamati ilipokea maoni yaliyowasilishwa kwa njia ya mtandao ambapo mpaka wakati Kamati inakamilisha kazi yake ilipokea maoni kutoka kwa wadau 72. *(Makofi)*

c) Kufanya uchambuzi wa kina wa makubaliano husika kwa kuzingatia uchambuzi wa awali, maelezo ya Serikali pamoja na maoni ya wadau yaliyowasilishwa kwa njia tofauti. Kazi hii ya uchambuzi ilifanyika kuanzia tarehe 07 - 09 Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Kamati hii ilifanya tathimini kwa kuzingatia Kanuni ya 107(2)(f) na (g) ili kupima iwapo kuna manufaa au athari ambazo Tanzania itapata

kutokana na mapendekezo ya Serikali kwa Bunge kuridhia makubaliano husika.

Mheshimiwa Spika, tathimini iliyofanyika ilikuwa na lengo la kujihakikishia kwamba makubaliano ambayo Serikali imeingia na inapendekeza Bunge kuridhia unakuwa na manufaa kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chimbuko la makubaliano; mnamo tarehe 28 Februari, 2022 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(Tanzania Ports Authority [TPA])* iliingia makubaliano ya awali *(Memorandum of Understanding)* na Kampuni ya *DP World* inayomilikiwa na Serikali ya Dubai *(Government of Dubai)*. Kamati ilitaarifiwa kwamba makubaliano hayo yalikuwa na lengo la kubainisha maeneo mahsusi ya ushirikiano ili kuendeleza na kuboresha uendeshaji wa miundombinu ya kimkakati ya bandari za bahari na maziwa makuu, maeneo maalum ya kiuchumi *(special economic zones),* maeneo ya maegesho na utunzaji mizigo *(logistics parks)* na maeneo ya kanda za kibiashara *(trade corridors)* nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, tarehe 25 Oktoba, 2022 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai zilisaini rasmi Makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa bandari za bahari na maziwa Tanzania *(The Inter-Governmental Agreement between The United Republic of Tanzania and The Emirate Of Dubai concerning economic and social partnership for the development and improving performance of sea and lake ports in Tanzania)*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, uchambuzi wa Kamati; msingi wa uchambuzi; hoja iliyowasilishwa na Serikali inapendekeza kwamba Bunge lako tukufu liridhie makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa bandari Tanzania kwa lengo la kutimiza masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Bunge kujadili hoja ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa umeainishwa katika Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambapo pamoja na masuala mengine utaratibu huo umeweka bayana kwamba Serikali ina wajibu wa kuwasilisha hoja yake Bungeni pamoja na makubaliano yanayokusudiwa kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, mawanda ya uchambuzi; napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba Kamati ilifanya uchambuzi kwa kupitia Ibara zote za makubaliano pamoja na viambatisho vyake ili kupata uelewa wa kutosha kuhusu masharti yaliyomo pamoja na maudhui ya masharti hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya uchambuzi wa makubaliano hayo, Kamati ilizingatia pia masuala ya msingi kulingana na masharti ya Kanuni ya 107(2) yakiwemo yafuatayo: -

a) Wajibu wa nchi baada ya kusaini makubaliano;

b) Kiwango ambacho Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imezingatiwa katika makubaliano;

c) Manufaa ambayo Tanzania itapata kutokana na makubaliano hayo;

d) Iwapo kutakuwa na athari zozote kutokana na makubaliano; na

e) Jambo lingine lolote lenye tija kwa Taifa kutokana na makubaliano husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati, maelezo ya Serikali pamoja na maoni yaliyowasilishwa na Wadau mbalimbali, yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza mawanda ya uchambuzi wa Kamati ili kulishauri Bunge kufanya uamuzi kwa mujibu Kanuni ya 111(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, masuala ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati katika uchambuzi; aina ya makubaliano; moja kati ya jambo la msingi ambalo Kamati ilizingatia katika uchambuzi wake, ni kutaka kufahamu na kujiridhisha kwamba nchi yetu imeingia makubaliano ya aina gani na Serikali ya Dubai. Baada ya kuihoji Serikali kuhusu suala hili ili kujiridhisha kikamilifu, Kamati imebaini kwamba makubaliano yaliyopo ni baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai juu ya kuweka misingi wa kisheria *(legal framework)* wa uendelezaji wa bandari. Aidha, aina ya ubia, kiasi/kiwango cha ubia na maeneo ya ubia yataidhinishwa kwenye Mikataba ya Utekelezaji *(Host Government Agreements* na *Individual Project Agreements)* itakayokuja kuingiwa iwapo Bunge litaridhia Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, lengo la makubaliano; katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba lengo la makubaliano yanayopendekezwa kuridhiwa *(objective of the agreement)*, kwa mujibu wa Ibara ya 2 ya makubaliano hayo, ni kuweka msingi wa kisheria katika maeneo ya ushirikiano ili kuendeleza na kuboresha uendeshaji wa miundombinu ya kimkakati ya bandari za bahari na maziwa makuu, maeneo maalum ya kiuchumi (*special economic zones)*, maeneo ya maegesho na utunzaji wa mizigo *(logistics parks)* na maeneo ya kanda za kibiashara *(trade corridors)*. Aidha, maeneo mengine ya ushirikiano ni katika kujenga uwezo *(capacity building)*, kuhaulisha maarifa, ujuzi na teknolojia *(transfer of knowledge, skills and technology)*, kuimarisha taasisi za elimu na kusaidia upatikanaji wa masoko.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza hapo juu, makubaliano haya yanaweka msingi wa kisheria baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na Serikali ya Dubai na si mkataba wa mradi wowote wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie eneo hili, kama tulivyoeleza hapo juu, makubaliano haya yanaweka msingi wa kisheria baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na Serikali ya Dubai na si mkataba wa mradi wowote wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi yote itakayotekelezwa itatatekelezwa kwa mikataba ya utekelezaji itakayotaja mawanda, faida na kufafanua kwa kina masuala ya kiutekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nimelazimika kuyarudia haya kwa sababu ni maeneo ambayo Watanzania walio wengi wamepotoshwa katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uendeshaji wa bandari, ni sehemu ya jitihada ambazo nchi yetu inapaswa kuziunga mkono ili kuongeza ufanisi na utendaji wa kazi wa bandari zetu. Hata hivyo, ni vyema Serikali ikahakikisha kwamba katika kutafuta wawekezaji wa sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu na uendelevu wa biashara baina yetu na mataifa mengine, kunakuwepo na umakini, weledi na uwazi bila kuathiri maslahi mapana ya nchi katika kuongeza pato la Taifa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mawanda ya utekelezaji wa makubaliano; Wajumbe walihoji ili kupata ufafanuzi kwa Serikali iwapo utekelezaji wa makubaliano husika utahusisha taasisi zipi na iwapo utazigusa bandari zote nchini, au ni kwa Bandari ya Dar es Salaam peke yake. Msingi wa hoja hii ni kutaka kujua kiwango cha utekelezaji wa ubia katika uendeshaji wa bandari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* ndio yenye jukumu la kutekeleza maeneo ya ushirikiano kuhusu Makubaliano haya kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa upande wa Serikali ya Dubai, Kampuni ya *DP World* na washirika wake ndio zitakuwa taasisi za utekelezaji. Utekelezaji huo utafanyika kupitia Mikataba ya Utekelezaji *(Host Government Agreements* na *Individual Project Agreements)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilitaarifiwa kuwa pamoja na ushirikiano huo, nchi yetu itakuwa na haki ya kuitaarifu Serikali ya Dubai kuhusu fursa nyingine za uwekezaji katika maeneo ya bandari, maeneo huru ili kuwezesha taasisi za Dubai kuwasilisha

mapendekezo ya uwekezaji katika maeneo hayo. Kuhusu uwekezaji husika, *DP World* na washirika wake ndio watakuwa na jukumu la kutafuta fedha za uwekezaji kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya makubaliano kwa nchi; kwa mujibu wa mapendekezo ya kuridhia makubaliano haya yaliyowasilishwa na Serikali, kuridhiwa kwa makubaliano haya kutakuwa na manufaa yafuatayo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: -

i. Kuongeza fursa za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kutokana na uwekezaji mkubwa na ongezeko la shehena ya mizigo itakayopitia Bandari ya Dar es Salaam. Aidha, maeneo mengine ya ushirikiano ni katika kujenga uwezo *(capacity building),* kuhaulisha maarifa, ujuzi na teknolojia *(transfer of knowledge, skills and technology),* kuimarisha taasisi za elimu na kusaidia upatikanaji wa masoko.

ii. Kuongezeka kwa ufanisi katika uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi na kuleta tija stahiki.

iii. Kuongezeka kwa Pato la Taifa kutokana na uboreshaji wa shughuli za kibandari.

iv. Kuongezeka tija na kuwezesha mwendelezo wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo imekuwa ikijengwa na Serikali kama vile: -

    a. Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa *(Standard Gauge Railway - SGR)*

    b. Ujenzi wa meli za mizigo katika maziwa makuu; na

    c. Mradi wa Lango la Bahari la Bandari ya Dar es Salaam *(Dar es Salaam Maritime Gateway Project - DMGP)*.

v. Kuchagiza na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi zikiwemo kilimo, utalii, viwanda, mifugo, uvuvi, biashara na usafirishaji na hivyo kuboresha ustawi wa Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa suala la uwekezaji wowote wa kimkakati unafanywa na Serikali kwa lengo la kuchangia kukua kwa sekta mtambuka kama ilivyo kwa ujenzi wa reli, mradi wa kuzalisha umeme, maeneo ya kilimo na kukuza utalii, Bunge hili lina wajibu wa msingi wa kuunga mkono jitihada hizo, sambamba na kutimiza wajibu wake wa kuishauri na kuisimamia Serikali ipasavyo. Kwa muktadha huo, uwekezaji wowote ambao una lengo la kuongeza ufanisi wa bandari zetu, manufaa yake yako bayana.

Mheshimiwa Spika, suala la kutoyumbishwa kwa makubaliano; Ibara ya 30 ya makubaliano haya inaweka masharti ya kuwa na uthabiti, uimara na uhakika wa kutoyumbisha makubaliano. Serikali za nchi husika zinakubaliana kuwa, mazingira ya kisheria na kimakubaliano kuhusu uwekezaji huu yatakuwa ya uthabiti na ya kuridhisha kwa Serikali zote mbili. Taarifa zote kuhusu uthabiti wa makubaliano zitakubaliwa kati ya Kampuni ya *DP World* na Kampuni husika ya mradi na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*.

Aidha, masharti ya uthabiti wa makubaliano yatawekwa katika mikataba ya utekelezaji *(Host Government Agreements and Individual Projects Agreements)* itakayoingiwa kati ya Tanzania na kampuni ya mradi husika. Katika tarehe ya kusainiwa makubaliano haya, itatumika kama rejea ya tarehe ya uthabiti katika kufanya mabadiliko yoyote ya kisheria au mabadiliko ya kikodi yanayoweza kuathiri miradi husika.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya masharti haya ni utaratibu wa kimkakati baina ya pande za makubaliano kuhakikisha kwamba maslahi ya pande zote mbili yanalindwa kikamilifu kulingana na mazingira ya kiushindani na ni utaratibu wa kawaida katika mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, suala la ukomo wa muda/uhai wa makubaliano; Ibara ya 23(1) hadi (4) ya makubaliano haya inazungumzia kuhusu taratibu za kusitisha makubaliano. Kamati imefanya uchambuzi wa Ibara ya 23 na kubaini kwamba iwapo Serikali itakuwa makini na usimamizi wa makubaliano haya, bado kuna nafasi kubwa ya kusitisha makubaliano wakati wowote ule iwapo kutatokea mgogoro baina ya pande zote mbili za makubaliano haya na mikataba ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba nirudie tena eneo hili kwa sababu nako kumetafsiriwa vibaya huko nje ya Bunge letu. Ibara ya 23(1) hadi (4) ya makubaliano haya inazungumzia kuhusu taratibu za kusitisha makubaliano. Kamati imefanya uchambuzi wa Ibara ya 23 na kubaini kwamba iwapo Serikali itakuwa makini na usimamizi wa makubaliano haya, bado kuna nafasi kubwa ya kusitisha makubaliano wakati wowote ule iwapo kutatokea mgogoro baina ya pande zote mbili za makubaliano haya ya kimkataba kwenye eneo la utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, maoni na ushauri wa Kamati; Kamati imefanya na kukamilisha uchambuzi wake, na hivyo kuwasilisha Bungeni ili Bunge liweze kufanya kazi yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) na kuiwezesha Serikali kuendelea na taratibu nyingine. Hata hivyo Kamati imeona ni muhimu Serikali ikayazingatia kwa lengo la kuweka mazingira mazuri kwenye uandaaji wa mikataba ya utekelezaji *(Host Government Agreements* na *Individual Project Agreements)* ili kuwa na tija na kukidhi matakwa ya wananchi kama ifuatavyo: -

Moja, kwa kuwa Kamati imebaini kwamba makubaliano yanayopendekezwa kuridhiwa na Bunge yataweka msingi *(framework)* ili sasa Serikali iende hatua nyingine ya kusaini mikataba ya utekelezaji, Kamati inashauri kwamba mikataba yote itakayofuata katika kutekeleza masharti ya makubaliano haya iwe na tija na yenye kulinda maslahi mapana ya nchi ya Tanzania na watu wake. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba mikataba hiyo inajumuisha maoni ya wadau muhimu katika sekta mtambuka ili kuhakikisha kwamba, masuala ya msingi

yanazingatiwa katika kuboresha mawanda ya utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili nalo tumeweka uzito kwa sababu tumechukua na maoni yote ambayo yaliyoletwa kupitia Kamati hii tumezingatia.

Mheshimiwa Spika, ukomo wa mikataba na masharti ya tathimini; Kamati inasisitiza kwamba uhai wa mikataba ya utekelezaji itakayosainiwa itaje muda maalum wa utekelezaji wa miradi ambao utazingatia maslahi mapana ya nchi. Vilevile mikataba hiyo iwe na kipengele kinachoelekeza wabia kufanya tathimini ya utekelezaji wa miradi ya uwekezaji na kuvunja makubaliano iwapo utekelezaji huo hautafanyika kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhakika wa ajira na fursa kwa Watanzania; kwa kuwa makubaliano yanayopendekezwa kuridhiwa na yana sura ya ubia, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali: -

i. Kuhakikisha kwamba ajira za Watanzania zinalindwa na kuweka mfumo thabiti wa mgawanyo wa ajira baina ya nchi na wabia;

ii. Kunakuwepo na utaratibu wa kuwajengea uwezo wafanyakazi wa bandari kwa lengo la kuhaulisha ujuzi, maarifa na teknolojia; na

iii. Kushirikisha makampuni ya Kitanzania katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, menejimenti ya uwekezaji; kwa kuwa utekelezaji wa makubaliano unakusudia kuweka ushirikiano kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* na *DP World*, na kwa kuwa bado *TPA* atakuwa msimamizi wa karibu wa miradi ya uwekezaji wa bandari kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, hivyo basi Kamati inashauri yafuatayo: -

i. Mikataba ya ubia kati ya *TPA, DP World* na makampuni mengine izingatie maslahi ya nchi;

ii. Serikali iendelee kusimamia usalama kwa kuzingatia kwamba bandari ni sehemu nyeti;

iii. Serikali iendelee kukaribisha wawekezaji wengine katika maeneo ambayo hayajapata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya mwisho; naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati kabisa wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati hii ushirikiano na maelekezo, ushauri na busara zako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii bila kuingilia uhuru wa majadiliano, mwenendo na maamuzi yaliyofikiwa na Kamati hii. Kwa hakika, umeonesha dira, ukomavu wa kisiasa na kiuongozi ili kukuza demokrasia ndani ya Kamati, Bunge na nchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati kabisa, Wajumbe wa Kamati ya Pamoja ambao pamoja na kutofautiana kimawazo, kimtazamo na kiitikadi, lakini bado wamekuwa wavumilivu, kuheshimu mawazo ya wengine, na hatimaye kufikia makubaliano ya pamoja ili kulishauri Bunge hatua ya kuchukua. Kwa kutambua mchango wao katika kujadili hoja hii, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyoandikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inamshukuru mtoa hoja, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) pamoja na Naibu Waziri (Sekta ya Uchukuzi) Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete (Mb) kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Azimio la Kuridhia Makubaliano huu. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa ushirikiano walioipatia Kamati ya Pamoja na kutoa ufafanuzi pale walipohitajika kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa umma wa Watanzania na watu wote wenye nia njema na nchi hii, ambao walitenga muda wao kuitikia wito wa Kamati na kufika kutoa maoni yao mbele ya Kamati na pia kwa kuwasilisha maoni yao kwa maandishi kwa njia za kielektroniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa uratibu wa shughuli za Kamati na kutoa ushauri wa kitaalam wakati wa uchambuzi wa mapendekezo ya kuridhia makubaliano hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka ambayo Bunge limepewa kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, naomba sasa lijadili na kuridhia makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa Bandari Tanzania, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, amemaliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, lakini pia Mwenyekiti wetu ameshasoma taarifa yetu ya Kamati ya Pamoja. Sasa mtakumbuka kuwa ratiba tuliyokuwa tumewagawia baada ya marekebisho tuliyoyafanya leo siku ya Jumamosi ilikuwa tuwe pia na maazimio mengine mawili kwa maana ya Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mipaka ya Hifadhi ya Taifa Ruaha, lakini pia Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mipaka ya Hifadhi ya Taifa Kigosi. Maazimio haya bado yanafanyiwa kazi na Kamati na yatakapokuwa tayari yataletwa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile ninalo tangazo hapa la wageni na tangazo lingine la kazi.

Tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa ambaye ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, hawa ni Dkt. Ally Possi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu - Sekta ya Uchukuzi, yupo ndugu Hamza Johari Mkurugenzi Mkuu wa Usafiri wa Anga. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Mussa Mbura ambaye Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, yuko pia Mhandisi Juma Kijavara ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, yuko pia Ndugu Maseke Mabiki – Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, na yupo pia Ndugu Redemptus Bugomola ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Idara ya Usalama na Mazingira, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Silvatus Kapandila - Mhasibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi, yupo pia Ndugu Devota Gabriel - Mkurugenzi Msaidizi Sekta ya Ufuatiliaji na Tathmini, na yupo pia Ndugu Leonard Lwiza - Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA, karibu sana.

Yupo pia Ndugu Richard Malya - Mkurugenzi wa Ununuzi na Ugavi Sekta ya Uchukuzi, yupo pia Mhandisi Nandaro Hezron-Kaimu Mkurugezni Miuondombinu ya Uchukuzi Sekta ya Uchukuzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wapo pia wageni wetu Wabunge; wapo wageni watano wa Mheshimiwa Jerry William Silaa ambao ni wafanyabiashara kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa John Pallangyo kutoka Arumeru Mashariki, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Asha Abdullah Juma ambae ni mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu Chwaka Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, viongozi 100 kutoka Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha *St. John* cha Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 91 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosoma Kozi ya Uchumi, karibuni sana Bungeni wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge anawakumbusha kuwa ile semina ambayo mlitangaziwa inayoletwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na Mafunzo mnakumbushwa kwamba semina hii itakuwa siku ya kesho saa 4.00 asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, mnatarajiwa kuhudhuria semina hii kwa wingi ili muweze kutoa mawazo yenu katika hatua hzi mbalimbali ambazo Serikali inazichukua.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza mchango wetu, Kanuni zetu za Bunge Kanuni ya 107 na Kanuni ya 111 zinatuongoza katika kazi yetu hii.

Kanuni ya 107 Sehemu ya Kwanza kwa maana ya fasili ya kwanza; "Endapo Jamhuri ya Muungano inaingia Mkataba wa Kimataifa ambao kwa masharti yake unahitaji kuridhiwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba, Waziri husika au Mwanasheria Mkuu wa Serikali atawasilisha kwa Katibu hoja ya kuridhia Mkataba akiambatisha nakala ya Mkataba unaokusudiwa kuridhiwa."

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu haya mambo yamekwishakuwa mengi sana huko nje, ni lazima Serikali iwe imeshaingia Mkataba ndio uletwe Bungeni, sio kwamba unaletwa kabla kwa sababu kabla unakuwa sio Mkataba, na sisi mamlaka yetu ya Kikatiba hayo yamefafanuliwa pia kwenye Kanuni ya 111 kile ambacho ndicho tunakifanya hapa leo.

Kanuni ya 111(1); "Majadiliano wakati wa kujadili hoja ya kuridhia Mkataba yatahusu masharti ya Mkataba husika."

Fasili ya (2); "Baada ya majadiliano kukamilika, Spika atamwita mtoa hoja kuhitimisha hoja yake kabla hajalihoji Bunge kupata uamuzi wake."

Fasili ya (3); "Uamuzi wa Bunge unaweza kuwa ni Azimio la: -

(a) Kuridhia masharti yote ya Mkataba;

(b) Kuridhia baadhi ya masharti ya Mkataba iwapo Mkataba unaruhusu kufanya hivyo; au

(c) Kukataa kuridhia Mkataba husika.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili tunalokaa sasa hapa kazi yetu iko katika Kanuni ya 113. *(Makofi)*

Haya hapa mbele nimeletewa vikaratasi vingi vya Wabunge wanaotaka kuchangia. Tutazama na muda wetu unavyokwenda lakini tutajitahidi wengi wenu wapate nafasi.

Kwa kusema hayo, naanza na wale waliotangulia kuleta vikaratasi, kwa hiyo, tutakwenda kwa mtindo huo. Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia tena wa kwanza, muda ukiniruhusu nitakuwa na maeneo matano.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni suala la msingi wa kisera; Chama cha Mapinduzi kilibadili mwelekeo wa kisera za kiuchumi na kisiasa miaka ya 1990 na mabadiliko mojawapo yaliyokuwa kwenye sera za kiuchumi ni kwamba tuliachana na sera za Serikali kuhodhi nyenzo za uchumi kama ilivyokuwa kabla.

Mheshimiwa Spika, miaka 20 ya CCM ilifanya tathimini kuhusu utekelezaji wa sera zake na mwaka huo ikatoa tafsiri ya ubinafsishaji na inasomeka hivi; "Ubinafsishaji hauna maana ya Serikali kukabidhi mali ya umma kwa watu au taasisi binafsi. Ubinafsishsji maana yake ni mambo matatu yafuatayo:-

(i) Kuanza ama kuuza baadhi ya hisa za kampuni za umma kwa wawekezaji binafsi; ama

(ii) Kuingia ubia na makampuni binafsi au watu binafsi wa ndani au nje ya nchi;

(iii) Kukodisha kampuni ya umma kwa taasisi au watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, hii ndio misingi ya sera ya ubinafsishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkutano Mkuu wa CCM wa Nne uliweka mazingatio mawili katika Sera ya Ubinafsishaji; kwanza, ni Serikali kuchagua taasisi au mtu binafsi kwa uangalifu ili awe mtu au tassisi yenye uwezo wa fedha na teknolojia, ujuzi wa biashara wa soko linalohusika na manufaa kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, Mkutano Mkuu ulielekeza kwamba mashirika na rasilimali muhimu ambao ni msingi na nyeti kwa maendeleo ya Taifa yanaendelewa kumilikiwa na dola. Mkutano Mkuu ukataja mashirika hayo na rasilimali hizo kwamba ni pamoja na Bandari, Reli, Posta na Simu na Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu hii mpaka leo *TANESCO* inamilikiwa na Serikali asilimia 100, ni kwa sababu hii Reli inamilikwa na Serikali, ni kwa sababu hii Bandari, Posta na Simu kwa maana ya *TTCL* inamilikiwa na Serikali. Kwa maelezo hayo azimio lililopo mezani lipo ndani ya sera za msingi za kiuchumi za CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, azimio hili lililopo mezani halihusu Bandari kuuzwa, azimio lililopo mezani linahusu uendelezaji na

uboreshaji wa utendaji wa bandari. Chama cha Mapinduzi kisingeruhusu Serikali yake kuingiza azimio hapo la kuuza bandari kwa sababu ni mali ya Serikali, lakini Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM kamwe asingeruhusu kuingiza humu azimio ambalo linauza bandari kwa sababu ni kinyume na sera yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Wabunge hawa walioko hapa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wala wasingepokea azimio la namna hiyo. Kwa hiyo tuwatoe wasiwasi Watanzania tunachojadili hapa kipo ndani ya misingi ya kisera za kiuchumi za CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni hofu ambayo imejitokeza; kwa unyeti wa bandari mara baada ya kusikia taarifa hizi za kubinafsisha bandari, wananchi wengi waliingia hofu na kusema kweli sisi kama Wabunge lazima tuzipokee, kuzielewa na kuzishughulikia hofu na hisia za watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sisi tunafanya mambo yetu hapa na kuzingatia mambo mengine ambayo ni matakwa ya wananchi wetu. Kwa hiyo, hizo hofu ni lazima tuzishughulikie na ninaamini baada ya Bunge hili tutakuwa tumefanya kazi kubwa ya kutoa hofu za wananchi wetu kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kimsingi tangu tuanze ubinafsishsji hakuna jambo ambalo limewahi kupokelewa bila hofu. Mtakumbuka wakati tunabinafsisha *NBC* kulikuwa na hofu kubwa na mjadala ulikuwa ni mkubwa sana. Mtakumbuka mpaka *TBL* na *TCC* hiki kiwanda cha Sigara ilikuwa ni mjadala mkubwa. Mimi nakumbuka nilikuwa chuo kikuu mwaka 2005/2006 tuliamua ku-*beggar* eneo kwa ajili ya kujenga *Mlimani City*, tuliambiwa Chuo Kikuu kimeuzwa, lakini tulisimama imara, Rais Kikwete akatusimamia. Sidhani kama leo kuna Mtanzania atalalamika kuhusu *Mlimani City*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hofu ya pili inayoeleweka lazima tukubali kwamba hatuna historia nzuri sana kwenye ubinafsishaji. Kutokana na historia ya baadhi ya mambo wananchi waliingia

hofu kwa sababu katika baadhi maeneo tulipigwa kwa kweli lazima tukiri, na kwa sababu hiyo hofu zinaeleweka na hofu hii Mheshimiwa Mkapa aliwahi kuieleza wakati wa *NBC*. Baada ya kelele kubwa sana za *NBC* Rais Mkapa alitulia akauliza tatizo ni nini? Ndipo akarekebisha wakati wa *NMB*. Ndio maana akauliza nifanyeje, akashauriwa kwamba *NMB* Serikali iwe na ubia, lakini vilevile ili ipate mtaji, watumishi wako wote wa Serikali na wengine wapitishie mtaji *NMB*. Ndio maana unaona leo *NMB* ni taasisi imara na inafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika mchakato wa ubinafsishaji Serikali imekuwa ikirekebisha pale panapohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, sitaki kulizungumzia sana kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri wamekwishaeleza kwamba azimio linahusu nini. Azimio hili kama alivyosema Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri tunazungumzia kuanzisha mahusiano ya kiuchumi na kijamii kati ya nchi mbili Serikali yetu na Serikali ya Dubai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo tukisharidhia Serikali inakwenda kufanya kazi yake ya kawaida ya kuingia kwenye mikataba. Kwa hiyo, hapa tulipo waheshimwa wananchi hatuna mkataba wa *TPA* na *DP World,* wala hiyo sio kazi ya Bunge hili hiyo ni kazi ya Serikali. Kwa hiyo, hilo jambo lieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma Mkataba huu kama alivyosoma Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri *appendix I* inazungumzia maeneo tutakayoingia kwenye miradi ni Bandari ya Dar es Salaam, akifanya vizuri Serikali inaweza kumwalika ndivyo mkataba unavyosema aende kwenye maeneo mengine. *So, it is not automatic* tunazungumzia Bandari ya Dar es salaam na baadhi ya maeneo*, Berth Zero, Berth Four, Berth One to Four, Berth Five to Seven,* kwa hiyo, ipo wazi jambo hili lieleweke.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Wabunge tuna jukumu pale ambapo kunakuwa na upungufu kwa kuzingatia hisia za watu na hofu zao na

mapendekezo yao kurekebisha pale ambapo inahitajika kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kupendekeza kwa kuzingatia Ibara ya 22 kwa sababu watu pia wanasema Mkataba huu hauna namna ya kurekebisha. Mkataba unarekebishika kwa Ibara ya 22 imeweka wazi kwamba inawezekana kurekebeshika, kwa sababu kengele imelia nitaachia hapo, lakini nataka kupendekeza maeneo ya kurekebisha ikafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, moja ni suala la *timeframe;* hili limezungumzwa sana na wananchi kwamba mkataba hauna *timeframe* na wataalamu wetu wametoa maelezo kwamba mikataba ya namna hii kimataifa ni kawaida kutokuwa na *timeframe*. Hata hivyo, waende wakaangalie sisi ni Bunge la Taifa wala sisi sio Bunge la Kimataifa, kama hizo ndizo hisia a wananchi na ndio matakwa ya wananchi, angalieni uwezekano wa kurekebisha hata mkisema *not exceeding 25 years that is fine* ili kutoa hiyo hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Ibara ya 23(4) kile kipengele kingeweza kuondoka kile ambacho kinaaeleza kwamba mkataba hauvunjiki. Kimsingi Mkataba unavunjika mle mle ndani. Kwa hiyo, waangalie lugha iliyotumika ili kuwaaminisha wananchi wa Tanzania kwamba inawezkana kuvunja Mkataba.

Mheshimiwa Spika, jambo la tano na mwisho, ni mambo ya kuzingatia kwenye mikataba ijayo kwa wataalamu wetu, yapo mengi lakini la kwanza, kwenye ile bandari yetu pale kwenye *appendix I,* kimsingi ni maeneo ambayo tumekwishafanya uwekezaji. Kwa hiyo, tunatarajia mkataba ambao mtakaoingia uta–*focus* zaidi kwenye eneo la uendeshaji kuliko uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa maoni yangu ni maeneo ya mifumo ya TEHAMA; hili ni eneo *sensitive* linahusu usalama wa nchi, tuombe sana watu watu wa *TCRA* na *e-Government* wawepo, asiachiwe mwekezaji peke yake. Lazima watu wetu wahusike kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kila nchi kuna nchi zimebahatika kuwa na waasisi, nyingine hazina. Sisi ni moja ya nchi ambazo tuna waasisi kama ilivyo Marekani wana George Washngton - Rais wao wa kwanza aliwaachia misingi. Msingi mkubwa ambao Marekani wanaulinda kwa wivu mkubwa ni *liberty* kwa sababu ndio walioachiwa kwa maana ya uhuru wa watu wao.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna waasisi nchi hii, Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Karume ndio waasisi wa Taifa hili, na walituachia misingi kama ambavyo ilivyo kwa Marekani tunapaswa tusiiguse. Msingi mama wa Taifa hili mwalimu alisema; "silaha na sifa yetu kubwa ni umoja." *(Makofi)*

Kwa hiyo, nchi yetu ni mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, bila shaka tutatofautiana kimtazamo kuhusu sera na mikakati, lakini kamwe tofauti zetu zisiende kugusa misingi mama ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi Kitila Mkumbo natoka Kijiji cha Mgela, Kata ya Mtoa, Tarafa ya Ishedede Wilaya ya Iramba - Singida lakini mimi ni Mbunge wa Jimbo la Ubungo - Dar es Salaam, hilo limewezekana kwa sababu ya umoja wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna nchi ambazo Wabunge wao ni Wabunge wa makabila sio Tanzania, tunataka na tunatamani huko tuendako watoto wangu, watoto wa wajukuu zangu mimi atoke Iramba akagombee Ubunge Pemba, atoke Pemba akagombee Ubunge Bukoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuwaombe na tuwasihi wanasiasa na sisi viongozi tuepuke kauli na ambazo zinagusa misingi mama, tutofautiane kisera, hiyo inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa dakika moja tu naomba nitoe wito kwa wataalamu wetu. Wataalamu wetu mmesikia hofu, hisia na matamanio ya Watanzania. Watanzania hawapingi ubinafsishaji wa bandari wanataka mikataba iwe mizuri, kwa hiyo wataalamu wetu hilo lizingatiwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo nilikuwa nakusikiliza mchango wako. Samahani hapa mwishoni hapa badala ya hili neno ubinafsishaji linaweza tena kutuma ujumbe mwingine. Nadhani kuna tofauti ya uwekezaji na ubinafsishaji. Hitimisha hoja yako kwa sekunde thelathini.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wataalamu wetu mzingatie hilo ili uwekezaji uwe mzuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho tuliombe Bunge lako la kuanza nalo katika mikataba itakayoingiwa tuombe ije hapa kwa mujibu wa sheria tuliyonayo kwa sababu ni nyeti na ni muhimu mikataba hii ije tuipitie kama ambavyo sheria inasema itakuwa ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimekwisha mtaja Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuwa mchangiaji wa pili katika hoja hii muhimu sana iliyoko mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niishukuru sana Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya kuendelea kupambana kutafuta majibu ya maswali magumu yanayosumbua uchumi na ukuaji wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bandari ni moja kati ya masuala magumu ambayo yana umuhimu mkubwa katika uchumi wa nchi yetu, kwa hiyo kitendo cha kuendelea kuhangaika kutafuta ufumbuzi juu ya suala hili ni jambo ambalo tunapaswa kuliunga mkono na kulipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo muwasilishaji hoja pamoja na mchangiaji aliyetangulia alivyosema hoja hii imekuja mbele ya Bunge lako chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge lako hili mwaka 2017 lilishapitisha mwongozo wa jinsi ya kujadili ambao umezingatiwa, Kamati imefanya kazi yake vizuri na tumeona taarifa yake na tunaipongeza kwa taarifa nzuri katika hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili kama alivyozungumza mchangiaji wa kwanza suala hili limeleta taharuki, limeleta hofu katika jamii yetu ya Tanzania moja kwa mambo ambayo pengine ni ya kisiasa yanayoenezwa na watu mbalimbali lakini hofu nyingine tu ni hofu ya kawaida ya hofu ya kitu kipya, hofu ya kitu usichokijua *(fear of unknown)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inatokana tu na kwamba tumekaa na bandari yetu kwa miaka 60 tumekuwa tukiitumia wenyewe, tunapanda, tunashuka, tunakwenda, tunarudi miaka 60 siyo muda mchache, sasa ghafla unaposikia kwamba uendelezaji wake unachukua mfumo mwingine lazima kunakuwa na hofu ambayo sisi kama Wabunge tunalo jukumu la kuelewa na kuwaelewesha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitaangalia zaidi maeneo ambayo huwa yanahojiwa kwenye mkataba. Ukipewa mkataba uuchambue au utoe *opinion* mojawapo ya mambo ya kwanza kwanza kabisa kujiuliza ni wahusika wa mkataba *(parties)* kwamba hivi ni nani hawa wanaosaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu uko wazi kwamba umesainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo hiyo hatuna hofu yoyote ya kuifahamu kwa sababu tunaijua ni Serikali yetu, lakini pia pale kwenye *preamble* imesainiwa na nchi inaitwa *The Emirates of Dubai*. Sasa the *Emirates of Dubai* ni sehemu ya Umoja wa Falme ya Nchi za Kiarabu au *UAE United Arabs Emirates* ambayo ni dola ya Kifalme inayoongozwa na Katiba, *it is the constitutional monarchy.*

Mheshimiwa Spika, Katiba yake ya mwaka 1971 kama ambavyo imerekebishwa mara nyingi mpka 2004 ndio toleo ambalo lipo sasa hivi inaunda shirikisho lenye hizi Emirates lenye hizi nchi saba ambayo ni Dubai tunayoizungumzia Sharjah, Abu Dhabi, Dubai, Ajman, Umm Al-Quwain, kuna Ras Al Khaimah na Fujairah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hizi nchi ambazo zinaunda hili shirikisho, shirikisho lina bendera linaundwa Taifa, lakini hizi nchi shiriki zinazounda hili shirikisho pia zina bendera zake na mamlaka yake. Ibara ya 120 ya Katiba ya *UAE* inataja masuala ya Muungano *(union matters)* za *UAE,* inataja masuala ya Muungano ambayo yako 19 katika masuala hayo suala la uwekezaji si sehemu ya masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji ni sehemu ya mamlaka ambayo imeachiwa hizi nchi moja moja hizi Emirates. Kwa hiyo, Mkataba wetu huu umesainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwakilishwa na Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wetu wa Miundombinu kwa idhini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na upande wa *The Emirates of Dubai* imesainiwa kwa idhini ya Mfalme wa Dubai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende mbali kidogo, Dubai ni *absolute monarchy* yaani ni nchi ya Kifalme *per see* ambapo Mfalme akishasaini *under seal* chini ya ile lakiri yao huo ni mkataba ambao ni halali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimelizungumza hili kwa sababu mojawapo ya hofu zinazoendelea ni kwamba mbona hapa Rais wetu amesaini na Waziri lakini kule amesaini mkuu wa ile *port* ni kwa sababu ile ni *absolute monarchy* na tayari Mfalme yule ameshasaini pale kwenye ule mkataba, ameshatoa idhini yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndivyo ambavyo wenzetu hawa wamekuwa wakiishi mpaka wakageuza jangwa likawa sehemu ambayo dunia nzima inaitamani. Wamenaishi hivyo na

wameweza kufikia hatua hiyo katika nchi hiyo katika nchi hii *I mean* katika dunia hii. Kwa hiyo uwekezaji haupo chini ya yale mambo ya Muungano isipokuwa *article 117* ya Katiba hiyo ya *UAE* inatoa mamlaka kwa kila nchi kushughulikia mambo ya ukuaji wa uchumi na biashara wa nchi zao ili waweze kuchangia kule kwenye *union* yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa niendelee tu kusema kwamba haya ni makubaliano, makubaliano pia unaweza ukayaita mkataba, lakini haya ninayosema ni makubaliano ya uendelezaji wa bandari zetu chini ya Ibara ya 5(3) cha Mkataba huu, hizi taasisi mbili maana kama ilivyosema Tanzania inamiliki *TPA* na Dubai inamiliki *DP World* na hakuna mahali kwenye mkataba huu ambapo *DP World* imesaini ni hizi Serikali mbili zimesaini ili kujenga mazingira sasa ya haya makampuni yake mawili kushirikiana na chini ya ile Ibara ya 5(3) ya mkataba huu kila panapokuwa na *project* ambayo *TPA* na *DP World* wataingia mkataba kutakuwa na *presentation* na uwasilishi ambao utaletwa na *DP World, TPA* italipitia na kulijadili na kusaini mkataba tofauti kwa kila mradi ambao utakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha kushauri tu kama ambavyo mwenzangu Profesa Mkumbo alizungumza ni kwamba tunahitaji umakini mkubwa tu wakati wa kusaini hii mikataba mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa Waziri akieleza mambo ambayo Serikali ime-*undertake* kuzingatia wakati wa kusaini huo mkataba. Mimi nakubaliana na yale mambo ambayo ameyaorodhesha ikiwa ni pamoja na suala la *land right* ambalo lipo huku, kwamba kama ambavyio mkataba huu unazungumzia kwamba *land right* ni juu *possession* na *access* na siyo *ownership* basi hilo liendelee kuzingatiwa hivyo hivyo kama ambavyo mkataba huu kubwa umeweza kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba huu unaruhusu marekebisho yaani *amendment*, unaruhusu *termination* na Ibara ya 21 inaruhusu matumizi ya sheria za Tanzania katika ile mikataba mmoja mmoja ambayo tutakwenda kuingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja, na ninawashawishi Wabunge wenzangu tuuridhie mkataba huu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niwe miongoni mwa Wabunge ambao wamepata fursa hii adhimu ya kuzungumza kuhusu azimio hili ambalo tunakwenda kulipitisha, azimio ambalo limepata kuzungumzwa na Watanzania wengi sana huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuwaomba Watanzania kwamba shughuli ya leo tunayoifanya tunaifanya kwa niaba yao Kikatiba, hofu waliyokuwa nayo na sisi mwanzoni tulikuwa na hofu hiyo hiyo, lakini baada ya kujiridhisha kwa kupitishwa na wataalamu wetu kwenye jambo hili hofu yetu imeondoka, na nataka niseme kuanzia sasa tutaendelea kuwapa elimu wenzetu walioko nje ya Bunge hili na tukitoka hapa tukirudi majimboni tutakwenda kuifanya kazi hiyo vizuri pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makubaliano haya ya ujumla sehemu zote ambazo Watanzania wana hofu tutakwenda kuzikazia zaidi kwenye mkataba mmoja mmoja kwenye miradi inayokwenda kuingiwa, na sisi hapa hatupo kwa ajili ya kuyashauri hayo ambayo wao wana hofu nayo na sisi tunaona kwamba ni ya msingi na kwamba Serikali inapokwenda kuingia mkataba mmoja mmoja ikayakazie. Mambo hayo ni pamoja na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Serikali baada ya azimio hili kupita waende wakafanye *valuation* ya Bandari yetu ya Dar es Salaam, na ambao kwa kweli kwenye *appendix I* ndipo ambapo mwekezaji au wenzetu wamechagua kwamba tukashirikiane nao. Kwa hiyo, ni muhimu sana kufanya *valuation* ya bandari ili tujue *asset* tulizonazo kwenye bandari yetu, tujue *reliability* zilizopo

kwenye bandari yetu na kwa ujumla tuujue mtaji wetu uliopo kwenye bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni muhimu sana kufanyika kwa sababu tunakaribisha mwekezaji mwingine na anaondoka mwekezaji mwingine *TICTS* aliyekuwepo pale. Kwa hiyo ni muhimu tukafanya *valuation,* tujue mtaji, lakini vilevile tujue *future earnings,* lakini vilevile tujue *market value* ya *asset* zetu, ni muhimu sana jambo hili lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ni la muhimu sana kufanyika ni *feasibility study*. Tufanye *feasibility study* ya miradi yote ambayo tunafikiri kwamba au ambayo tutakwenda kukubaliana na mwekezaji anayekuja kabla ya kuingia mikataba naye tufanye *feasibility study*. Kwa nini nasema *feasibility study? Feasibility study* itatuambia kwamba katika bandari ambazo mwekezaji ameonesha nia na katika maeneo ambayo mwekezaji ameonesha nia anatutoa pale kwa uwekezaji wake kutupeleka wapi? Kwa mfano mpaka sasa bandari zote 86 zinazohudumiwa na *TPA* zinapokea meli 4,686; *feasibility study* itatuonesha kwamba kwa uwekezaji anaoenda kufanya atatupeleka kwenye kupokea meli ngapi kutoka hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili mpaka sasa tunapokea tani za mizigo milioni 20.709 uwekezaji huu unaokuja *feasibility study* itatuonesha kwamba ukifanyika tutafikia *level* ipi? Katika hizo tani milioni 20 tunazopokea za mizigo milioni 18 zote ni za Bandari ya Dar es Salaam ambalo ndio eneo kwa *phase* ya kwanza mwekezaji ameonesha *interest*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine *feasibility study* ikatuoneshe kwamba kutoka kwenye makontena 823,404 ambayo tunayapokea kwa sasa, uwekezaji huu utatupeleka kwenye makontena mangapi? Kwamba baada ya uwekezaji na baada ya bandari kwenda kwenye *full swing* tutakuwa na uwezo wa kupokea kontena ngapi?

Ndugu zangu Watanzania na ndugu Wabunge wenzangu hivi ndio vipimo ambavyo kwenye mikataba inayoenda kufanyika

mbele lazima tuwe navyo ili miaka kadhaa baadae tuweze kujitathmini kwamba uwekezaji huu tulioupokea na tunaouridhia umetusaidia au umeturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huu unaofanyika tukafanye *feasibility study* ili tujue kwa sasa tuna magari 200,938 hayajahudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam, tunatarajia mzigo uongezeke kwa uwekezaji unaokuja na magari yanayohudumiwa waongezeke ajira za Watanzania ziwepo na *chain* yote ya uchumi ionekane kwa uwekezaji unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bandari yetu na katika vitu kwa kweli ambavyo tunahamasika na tunakubalina sote kwamba tunamhitaji mwekezaji ni ili kuongeza mzigo ambao bandari inahudumia wa nchi jirani. Hivi sasa bandari yetu inahudumia mzigo kutoka nchi jirani tani milioni 7.7 tunatarajia baada ya uwekezaji kufanyika na mikataba tunayokwenda kuingia mmoja mmoja ikatuwezeshe kututoa hapa kwenye kupokea tani milioni saba peke yake kwa maana ya mizigo ya Zambia iongezeke, mizigo ya Kongo ikaongezeke, mizigo ya Burundi ikaongezeke, mizigo ya Rwanda ikaongezeke na Malawi ikaongezeke, Uganda ikaongezeke na nchi zingine kama vile Msumbiji, Sudan, Kenya, Comoro, Angola na Zimbambwe, uwekezaji utusaidie kufika hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili watu wengi wamelizungumzia huko nje, wapo waliolipotoshwa, lakini wapo waliokwenda mbali zaidi ya kuzungumza yale ambayo ni hatari kwa umoja wa nchi yetu na mshikamano wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwakumbushe wakati nchi yetu ilipopita kipindi kukubwa cha *Covid-19,* wakati dunia yote ilikuwa imejifungia ndani haikuzalisha, Watanzania tulikuwa tunatembea mitaani na tulikuwa tunafanya shughuli zetu. Makamu wa Rais wa nchi hii alikuwa ni Dkt. Samia Suluhu ndio alikuwa Mshauri Mkuu wa Rais aliyekuwepo. Tulivuka salama na hatukumtilia mashaka kama ni Mtanzania au siyo Mtanzania. Jambo hili hatupaswi kuliendekeza, yanapokuja mambo ya msingi ya hoja tutofautiane kwa hoja na si kwa kubaguana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawakumbusha Watanzania, miaka miwili iliyopita shughuli za kisiasa hazikuwa zinaruhusiwa kufanyika, hapakuwa na mikutano wa chama cha siasa wala hapakuwa na *press conference* za kwenye vyombo vya habari, ni Rais huyu huyu ndio alikuja akafungua hiyo minyororo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini wakati ule na yale yalikuwa ni mambo ya kitaifa ni mambo ya kikatiba kama ambavyo tunafanya hili la leo, kwa nini wakati ule hamkuhoji kwamba huyu ni Mzanzibar amekuja kufungulia vyombo vya habari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza miaka miwili iliyopita kulikuwa na magazeti zaidi ya manne yamefungiwa *online tvs, online media* karibu vyombo zaidi ya 30, 40 vimefungiwa. Hivi ninavyozungumza ni Rais huyu huyu aliyepo amefungulia vyombo vyote vilivyokuwa vimefungiwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ilishagonga, ahsante sana.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, mpaka sasa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa kwa kuwa umeshaomba, sekunde 30 malizia.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, mpaka sasa hakuna kesi mahakamani ya chombo chochote cha habari wala mwandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema tangu awali majina ninayo mengi sana hapa mbele, kwa hiyo, niwaombe na ninyi mnisaidie na msaidiane na ninyi wenyewe kila mtu asipotumia muda wake maana yake kuna watu hawatapata nafasi. Kwa hiyo niwaombe sana nikisema

muda wako umekwisha basi ujitahidi ili na mwenzio naye apate nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Ali Hassan Omar King atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mheshimiwa Jerry William Silaa, ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutupa uhai na uzima kusimama leo hapa kuja kujadili jambo lenye maslahi na uchumi na jamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi kwa sababu kama ulivyosema walioomba kuchangia ni wengi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka niseme msemo mmoja ambao msemo tunautumia; *maa filbidhi ilaldaras;* kwenye weupe ukisugua utatia doa, kwenye weupe ukisugua utaweka doa. Maana ukisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambaye leo hajaruhusu kusema kwamba maelezo haya yaende kwenye *Hansard.* Watanzania huko nje wamemsikia Mheshimiwa Waziri amesema jambo moja baada ya lingine, ametaja maslahi ya Mkataba huu, ametaja chanzo au chimbuko la Mkataba huu, ameusema na Mkataba wenyewe, amechambua, amesema na faida tofauti tofauti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Watanzania tunawaomba acheni kusikia yale maneno ya watu wengine kule, hebu sikilizeni ile hotuba ambayo imesomwa na Mheshimiwa Waziri hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mwenyekiti wa Kamati alimaliza ndio maana nikasema kwenye weupe ukisugua utatia doa; amesema kwa niaba ya Bunge lako hili tukufu na ameishauri Serikali na ameunga mkono hili azimio kwa sababu yale aliyoyaeleza sisi sote tunayakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niseme kuna kitu kimoja, kwa nini watu wamezungumza yale huko nje? Kwa sababau kuna mazingira ya ushindani wa bandari yetu na kuna mazingira ya

hawa wawekezaji katika bandari. Kuna ushindani wa wawekezaji katika hii bandari, sasa wengine ukisikia wanachangia huko nje wanachangia, lakini akili zao hazijasalimika. Hili neno naomba liwe *noted*. Kweli wametoa maoni, lakini wametoa wakati akili zao hazijasalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanatoa maoni haya akili zao ndani kuna vifurushi vya nongwa, wengine wanatoa maoni katika mkataba huu lakini akili zao kuna vifurushi vya tamaa kwamba kwa nini amepata mtu mwingine, wengine wanatoa maoni lakini ndani ya akili zao kuna kifurushi cha ubaguzi. *(Makofi)*

Sasa huwezi ukawa akili yako haiko salama ukajadili jambo likaenda salama kwa Watanzania. Naomba Watanzania wamesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kitila Mkumbo alisema nchi hii ina sera, ubinafsishaji umeanzishwa zamani, uwekezaji na sera zake upo toka enzi ya Rais Mkapa umewekwa, lakini Chama cha Mapinduzi tunayo sera hiyo. Kwa hiyo, Rais huyu huyu angetokea sehemu yoyote ya Tanzania hii angefuata sera za uwekezaji angefuata na sera za Chama cha Mapinduzi na ndicho ambacho kinachosema na ndicho kinachoongoza kusema hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hakufanya Rais huyu kwa sababu ya Uzanzibari, hakufanya Waziri, hakusaini kwa sababu ya Utanzania na sera yetu, mageuzi yetu ndio yaliyoturuhusu tufanye haya na tumefanya tumejirekebisha kama walivyozungumza wazungumzaji wengine na ndipo tukafika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hebu kila mmoja avute akili yake atizame kuna kikatuni kimoja kilikuwa kinaitwa cha nipashe, kinakuwa kina mdomo mrefu na masikio makubwa kinampasha mtu, halafu chukueni ile sura ya kile kikatuni mlinganisheni kuna mtu fulani alikuwa anazungumza maneno hayo utapata. Sasa sisi hatuwezi kusikiliza umbea kama huu ambao wao walikuwa wakiuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Pamoja ambayo imeshughulikia alisema haya ni makubaliano na makubaliano haya yanaweka msingi wa kitu kitakachokuja kufanyika, hiyo mikataba itakayokuja kujengwa huko mbele. Huu sio mkataba wameshazungumza watu, huu sio mkataba, tunawatoa hofu Watanzania wayasikilize hayo maelezo vizuri, lakini mikataba itakuja mmoja mmoja katika eneo moja moja.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika mkataba huu kuna *appendix I* ambayo kuna mambo ambayo *phase one project* zitakazofanyika. Kwa hiyo, ndani ya *project* zile zitakapofanyika ndipo kutakuwa kuna hiyo mikataba midogo midogo na mimi nilitoe hofu Bunge hili na wananchi wa Tanzania sio kwamba kila kilichotajwa kwamba kitafanyika kwa yote. Ukisikia kutafanyika *development*, ukisikia kutafanyika *improvement* ukisikia kutafanyika *management*, ukisikia kutafanyika *operations*, kuna miradi au kuna *phase* au kuna *project* ziko katika hatua tofauti tofauti. Ziko nyingine tutaanza kweli ku–*develop* kwa sababu ni kitu kipya, lakini kuna vingine vinatakiwa kufanyiwa *management,* lakini kuna vingine vitafanyiwa *operation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukitazama kuanzia hiyo gati *zero* mpaka gati *number seven* utakuja kuona kwamba ni kweli, ukiijua ile bandari kwamba kuna maeneo kutafanyika *operation* na kuna maeneo mengine wao wata-*improve* lakini wataachiwa bandari wenyewe waendeleze. Sasa na mimi na *stick* pale pale kwenye ushauri wa Kamati kwamba ni lazima tuhakikishe hiyo mikataba sasa iwe ina tija kwa Watanzania. Tuhakikishe hiyo mikataba wanashirikishwa wadau husika tutakapoingia hiyo mikataba mmoja mmoja, lakini pia mikataba hiyo ni lazima itoe ukomo au itaje ukomo kama wananvyosema wengine na maoni mwengine ambayo Mwenyekiti ameshauri na Wajumbe wengine Wabunge wengine wameshauri.

Mheshimiwa Spika, lakini hofu nyingine kwamba huu mkataba hauna ukomo, mkataba huu unao ukomo nao umetajwa, sisi kama Wabunge wa Bunge lako hili tukufu tumekaa hapa kwamba tunaelewa nini kinaendelea, sasa tuwaombe

Watanzania kile kifurushi walichochanganyiwa kule nje sicho, vifurushi vile vinatokana na mambo tofauti tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwenye ajira za Watanzania ndani ya mkataba huu cha kwanza ni kulinda ajira zilizokuwepo, lakini kutokana na faida na utanuzi ina maana zitapatikana na ajira nyingine. Sasa hapa ndipo tutakapojua kwamba tulikuwa tukipotoshwa ajira haziendi kutolewa, haziendi kuondolewa, tunaenda kuongeza ajira katika mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye manufaa tumeambiwa kwamba siku za kuteremsha makasha zitatoka kuanzia 4.5 mpaka siku mbili, ina maana hiyo ni tija, lakini pia meli kutoka siku tano mpaka saa 24 ni tija hiyo, lakini fedha ambazo zitakusanywa kutoka trilioni 7.7 mpaka trilioni 26.7; haya ni maendeleo makubwa kutokana na haya mageuzi. Sasa sisi kama Wabunge ndio tukasema kwamba hili azimio tunaiunga mkono Serikali kwa sababu tuko katika masuala ya kiuchumi na bandari zetu zina ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *DP World* yeye ana *market* nyingi sana, lakini isitoshe anataka kutuunga mkono ili reli yetu ambayo tumeianzisha ya *Standard Gauge* ipate mzigo, sasa tushaanzisha reli ipate mzigo halafu tuna ufinyu wa kushusha bandarani unafikirri tutaendelea wapi. Reli itakuja kuwa ya abiria... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nashukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian atafuatiwa na Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza Kiongozi wetu

Mkuu na Jemedari Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuifanya Tanzania isonge mbele na ipate maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nimshukuru Waziri Mkuu na kumpongeza kulifanya jambo hili kama msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali kuweza kulifikisha hapa lilipo, namna ambavyo amelisimamia na kuweza kushauri wataalamu wote kwa ujumla pamoja na Rais wetu ametutendea haki kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii ya kipekee kuishukuru timu nzima iliyoweza kuishauri Serikali hususan wanasheria wetu kutoka Wizara na kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa mara ya kwanza nikiwa ndani ya Bunge lako tukufu nikishuhudia mkataba huu ukija kwa uwazi zaidi. Ifikie wakati kama Watanzania tutambue wapi tunatoka na tunakwenda wapi. Namna ambavyo mkataba huu umeletwa ndani ya Bunge ni makubaliano ya wazi yasiyojificha na kuna muda tuchukue kuwapongeza watu ambao wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Waziri umefanya kazi vizuri, umeweka uzalendo mbele, umelitendea haki Taifa la Tanzania, timu yako tumefanya nayo kazi kwa kuuliza swali moja moja. Mimi binafsi nimemtafuta kati ya timu, mtu mmoja ambaye alikuwemo kuhusika na hili nikajiridhisha menyewe na hichi kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamefanya kazi kwa uchambuzi wa kina, hoja zote za Watanzania wamezizingatia hata zilizokuwa zikipita ndani ya mitandao. Hata na mimi kama Mbunge ambaye ni mwakilishi wa wananchi nadni ya Bunge hili kuna maeneo na vipengele nilikuwa navihisi kwamba haviko sawa, lakini nichukue fursa hii kuwaambia wananchi wa Tanzania waondoshe hofu, Serikali yao iko makini, viongozi wao wako makini, Bunge liko makini, Waziri Mkuu yuko makini, Spika yuko makini. Imefanywa kazi hii kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi ripoti zote zimepitiwa kupitia Kamati zako za Bunge. Kamati zimejiridhisha na sisi tuliokuwa hatupo ndani ya Kamati tumeyatafuta na tumejiridhisha kuona

makubaliano haya hayana chembe ya shaka. Kuna maneno yanayozungumza kwamba huu ni mkataba, Watanzania ifike wakati tuamke, tujue hizi kelele zinatoka wapi. Hakuna vita vikubwa duniani kama vita vya uchumi, hakuna kitu kikubwa duniani kama kitu cha kupiga hatua ya maendeleo. Siku zote hata maendeleo ya mtu binafsi yeye mwenyewe lazima apate vita, atapata vita kwa marafiki zake, atapata vita kwa majirani zake, atapata vita kwa watu waliomzunguka. Hii vita tuliyokuwa nayo ni Tanzania ya kusonga mbele ifike wakati Watanzania mjue kwamba maamuzi yanayotolewa ni maamuzi ambayo ni kwa maslahi ya nchi na si kwa maslahi ya mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani zaidi ya Wabunge 300 na tuko ndani ya Bunge tuone kwamba kitu hiki kinachoenda kufanyika kama ni cha hovyo tukakiridhia, hicho kitu hakiwezekani abadani, na mimi niliesimama hapa ni Mbunge wa CCM nitasema kweli daima kwenye hili wamefanya haki, wametutendea haki wanasheria wametutendea haki katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vipengele zaidi ya vipengele nane ndani ya makubaliano haya, Watanzania wanavizungumza. Hofu yao ni jambo ambalo linatufanya sisi tufanye utekelezaji wa kina, Watanzania tunawapongeza, hofu yenu imetufanya tuwe na bidii na kufanya kazi hii kwa kina na uaminifu. Hofu yenu imetujengea uimara wa kufanya kazi hii kwa uangalifu mkubwa, tuwaahidi kama mlivyotupa ridhaa ya kuwawakilisheni ndani ya nyumba hii tunahakikisha tutawatendea haki. Ondoeni hofu kazi hii inaenda kufanyika kwa uweledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la ubaguzi; wakati huu tuliokuwa nao ukimuona Mtanzania hususan mwenye uongozi anayeongoza watu, anatamka kauli ya ubaguzi tunamshangaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilyesimama hapa naitwa Tauhida Gallos Nyimbo; Nyimbo ni mtu wa Songea baba yangu ni mtu wa Songea, mama yangu ni Mzaramu. Mimi nimezaliwa Zanzibar na

Mbunge kutoka Zanzibar, leo tukisimama Watanzania tunaanza kubaguana hatutofika na dhambi ya ubaguzi ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kiongozi ndani ya Tanzania utakuja na hoja za msingi, Serikali yetu haikatai kukosolewa, makosa ambayo tunayakosoa inafanya uboreshaji zaidi. Nilitegemea kumuona kiongozi anayeongoza watu anahubiri amani, umoja na mshikamo pale ambapo anapoona kuna makosa anapaswa kurekebisha hayo makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ninajishangaa, kiongozi wa siasa anapoleta ubaguzi ndani ya chama chake, Naibu Katibu Mkuu anatoka Zanzibar, ninajiuliza anajifikiria vipi? Ana sehemu hata ya kuchangia kapata maamuzi ndani ya hivyo vikao vyao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Zanzibar katika sehemu ambayo ilikuwa kwa muda mrefu inakusanya mapato *ZRB* msimamizi wake anatoka Bara, hakuna kelele, hakuna zogo na mapato yanakusanywa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya utawala wa *ZBC* Zanzibar Mkurugenzi mmoja anatoka Bara, alishawahi kuwa *NEC* katika nafasi ya Chama cha Mapinduzi, sasa hivi ni Mkurugenzi *ZBC*, tunataka Tanzania hiyo ya kutoka Songea mpaka Makunduchi, hii ni Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka Wabunge tufike wakati tutamani kumuona mtu anayetoka hapa ndani ya jengo hili anakuwa pia ni Rais wa Zanzibar kutoka Bara. Tuipelekeni Tanzania huko, tuioneshenì Katiba yetu na kuiboresha, tuhakikishe Tanzania inakuwa moja watu wa Tanzania wanakuwa wamoja, itikadi za kisiasa tusiivunje Tanzania, itakadi ya kisiasa isimvunje mama Tanzania, upendo wetu ndio umoja wetu. *(Makofi)*

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja azimio hili asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi/ Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Jerry William Silaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mheshimiwa Joseph George Kakunda ajiandae.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa kuomba kumpongeza Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye mambo mawili; jambo la kwanza, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye uongozi wake anafanya mambo kwa uwazi na kushirikisha Watanzania wote na Bunge lako hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bandari Sura ya 166 ya mwaka 2004 kifungu cha 12(1)(b) na kifungu cha 5(e) kinaipa mamlaka Mamlaka ya Bandari kuingia kwenye mikataba ya upangishaji na uendeshaji. Kama Serikali ingeamua kufanya matakwa ya kisheria leo azimio hili lisingekuja Bungeni, lakini Mheshimiwa Rais kwa busara yake na kwa uongozi wake wa uwazi ameamua kuchukua njia ambayo inaonekana ni ndefu, lakini ni njia shirikishi leo tuko hapa tunajadali mkataba ama makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai juu ya uwekezaji wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili amesema Mheshimiwa Reuben Kwagilwa ni uhuru wa kujieleza kwenye Taifa letu. Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa uhuru mpana sana wa kujieleza. Watu wanasema mpaka

wanavuka mipaka, lakini nikuthibitishie wanayosema maneno hayo ni wananchi wetu na sisi ni viongozi wa watu lazima tuwasikilize katika kuelekea kwenye maamuzi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya azimio hili kuletwa Bungeni na wewe kuilete kwenye Kamati ya Pamoja inayoundwa na Kamati zetu mbili, mijadala imekuwa ni mingi. Mijadala ni afya kwa Taifa letu lakini lazima tuseme, wako watu ambao walikuwa wana nia njema ya kutaka kuelemishwa, lakini lazima tuseme vilevile wako watu wanaopotosha jitihada nzuri ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuleta maendeleo ya uchumi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze wanasiasa wakubwa wa nchi hii wakiwemo wa upinzani ambao walitoa maoni yao ya haki na hawakutumia fursa ya kupotosha umma juu ya azimio la makubaliano haya yalioko Bungeni. Maneno mengi yaliyosemwa amesema hapa Mwenyekiti Mheshimiwa Kakoso ambao sisi kwenye Kamati yetu ya Pamoja tumepokea maoni ya wananchi wengi, pamoja na yale maoni yalitoka kwenye maeneo ya mitandao ya kijamii yalionyesha kuna hofu kubwa baina ya Watanzania. Hofu yao iko kwenye maeneo mengi, yakiwemo watu wana hofu ya ajira za Watanzania, wananchi wana hofu ya ardhi yetu, wananchi wana hofu ya mapato, wananchi wana hofu ya ukomo, wananchi wana hofu ya usalama wa bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu, azimio lililoko mezani mbele yetu ni makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai na si mkataba wa aina yoyote wa uwekezaji, uendeshaji wala ubia wa bandari. Naomba niseme hili na kaka yangu Kitila Mkumbo naomba na yeye vilevile nimshauri, ni ngumu sana na kwa nia njema kabisa kwa mtu asiyekuwa na taaluma ya sheria kutofautisha baina ya *a contract and an agreement.* Kwa lugha ya Kiingereza cha kawaida inaonekana ni nyaraka zinazofanana, lakini kilichopo mbele yetu ni makubaliano yanayojenga msingi wa Serikali kwenda kutengeneza mikataba ambayo ndio itakuwa na utaratibu wa uwekezaji baina ya *Host Government Agreement* na *concession agreement za project* moja moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wengine elimu zetu za kwanza hazikuwa sheria, mimi nilisoma *Electronic Science and Communication,* nilienda kuongeza ujuzi huo tu katika nia ya kujaribu kufahamu nyaraka hizi unapozisoma kwa lugha ya kawaida inawezekana ikakupotosha ama mtu akakupotosha kwa makusudi. Zipo *clip* zinatembea za mwanasheria mmoja ukisikiliza lafudhi yake utajua nchi anayotokea, nchi ambayo tunashindana nayo kwenye shughuli hizi za bandari na ukisikiliza kwa makini hata usomaji wake anasoma kipengele kwa kukikatisha kipande ambacho anajua anaweza akapotosha umma kwa wale ambao hawajui *legal interpretation* ya kifungu kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme Kamati imetoa maoni na Wabunge wengi waliochangia wametoa maoni; Serikali inapoenda kutengeneza *Host Government Agreements* na inakwenda kutengeneza mikataba ya mradi mmoja mmoja itazingatia maeneo yote ya hofu za wananchi mliyoyataja pale juu kama Kamati ilivyopendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko eneo naomba niseme na niwathibitishie Watanzania katika kipindi Bunge lina Spika mbobevu wa sheria ni kipindi hiki. Spika Dkt. Tulia Ackson Mwansasu ni Mwanasheria mbobevu. Wale wasiofuata historia amewahi kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndiyo kipindi pekee usingeweza kuleta jambo lenye matatizo likaingia kwenye *floor* ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naliomba Bunge kazi iliyoko mbele yetu ya azimio la makubaliano haya, ni kazi uliyoitaja kwa mujibu wa kanuni fasili ya 107 na fasili ya 111 kama inavyotohoa ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia makubaliano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai ili kutengeneza msingi wa Serikali kwenda kutengeneza mikataba ya *Host Government Agreements* na *Concession Agreements* ambazo ndiyo zitajenga msingi mzima wa aina ya uwekezaji. Hapa hatuna ubia, hapa hatuna *partnership,* hapa hatuna uendeshaji, yote hayo yataelekezwa kwenye mikataba ile ambayo Serikali itaenda kuandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili ambalo nataka kulisema kwenye sheria niwaombe Waheshimiwa Wabunge na utatuongoza. Bunge linafanya kazi yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tusijiingize kwenye kazi ya Serikali ya kuwa waandishi wa mikataba tutajiondolea wajibu wetu wa kuisimamia Serikali pale ambapo Serikali itakuwa imekosea. Najua ni matamanio na ni mihemko ya kuona kwamba Bunge hili kila kinachofanywa na Serikali, kila mkataba uletwe, siyo utaratibu wa kikatiba na wewe utatuongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwaambia umma wa Watanzania maana matatizo yote ya bandari yameelezwa na wengi, wapo wanaochangia ambao hawalitakii mema Taifa letu. Mchakato wa maendeleo siyo mchakato rahisi, amesema Mheshimiwa Tauhida hata maendeleo yako binafsi ametaja marafiki, ametaja majirani hata ndugu zako wenyewe wanaweza wakawa wanapinga maendeleo yako binafsi, lakini wako washindani wetu wa kiuchumi, wako washindani wa wenzetu tunaoingia nao kwenye makubaliano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wako wengine ni *clout chasers* tu kwenye mitandao; *clout chasers* ni mtu anayetaka kupata na umaarufu, yuko mtu mmoja anaheshimika sana anaandika maandiko mengi juzi ameandika haiwezekani ukampa mtu bandari zote hiyo ni *sole proprietorship*. Hivi jamani hata ku-*google* tunashindwa? Maana ya *sole proprietorship* ni kumpa mtu bandari zote? Lakini ni mtu anaandika kwa kutafuta *fame* na watu wanamfuata wakimsikiliza. Lazima Bunge hili litoe uongozi na litoe ufafanuzi wa maeneo haya ili wananchi wetu wafahamu kabisa tuko hapa kwa ridhaa ya Watanzania. Tunaanza vikao vyetu kwa dua, tumeapa hapa kwa imani za dini zetu. Tunayoyafanya hapa yanahesabu kwa wananchi, lakini yanahesabu kwa Mungu wetu huko mbele ya haki. Tunafanya kwa uadilifu wa hali ya juu na wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nina maombi matatu; ombil la kwanza,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia kengele imeshalia.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, ombi la kwanza niliombe Bunge lako liendelee kumuunga mkono Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye mipango yake mema ya kujenga uchumi imara wa nchi yetu. *(Makofi)*

Ombi la pili, kuwaomba wananchi kuendelea kutuamini kwamba Wabunge wao wataendelea kusimamia maslahi yao kwenye maeneo yote katika kuishauri na kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi la tatu Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma ili kuondoa hofu na izingatie maoni ya Kamati na maoni ya Wabunge katika kutengeneza mikataba mizuri yenye tija kwa Taifa letu na kulinda maslahi ya Taifa hili na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kuna jambo nimeletewa taarifa hapa kwamba linazunguka huko kwenye mtandao, Mbunge yeyote ambaye amepokea bahasha hapa ndani hebu aifungue ina nini humo ndani? Yeyote tu. Hebu fungua bahasha yako halafu simama mmoja tu.

*(Hapa baadhi wa Wabunge walinyoosha juu bahasha walizogaiwa)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa hebu tusomee humo ndani kuna nini kwenye hiyo bahasha? Kamera zielekee kule kwa Mheshimiwa Vita Kawawa. Hebu tusomee kuna nini hapo maana tunaelekea sehemu mbaya sasa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, tumeletewa barua hizi kutoka *Kingdom Leadership Network Tanzania* ambayo ni ya *Invitation for the Sixth Tanzania National Prayers Breakfast on*

*24th June, 2023 Dodoma Convention Center (Jakaya Kikwete Convention Center)* ambayo hii inaelezea. Naweza nikaendelea?

**SPIKA:** Hiyo inatosha.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, inatosha ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa taarifa hapa kwamba Wabunge wanagawiwa pesa kwenye bahasha. Nadhani Watanzania waheshimuni wawakilishi wenu. Waheshimuni wawakilishi wenu. Eeh, waheshimuni wawakilishi wenu. Mmeshasomewa huko kwenye bahasha kuna nini maana sasa naona tunakoelekea siyo kuzuri kabisa.

Haya nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa nafasi ya kuchangia na ninaomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa maono yake na harakati anazozifanya kwa ajili ya maendeleo ya mama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa makubaliano zaidi ya 17 ambayo ameingia kwa maslahi ya Taifa letu. Mheshimiwa Rais anafahamu umuhimu wa sekta binafsi na ndiyo maana yeye mwenyewe amekuwa kipaumbele katika kuja na makubaliano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, duniani kote, duniani kote na siyo maneno yangu ni maneno ya takwimu kwa sababu wanasema *no research, no right to speak,* siyo maneno yangu mimi. Duniani kote uwekezaji wa sekta binafsi ndiyo mhimili wa maendeleo ya Taifa lolote duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu za *International Finance Corporation* zinasema; kazi zote na ajira zote takribani 90% duniani

kote zinachagizwa na zinaletwa na sekta binafsi. Shirika hili linasema 60% ya pato la Taifa kwa nchi zote duniani zinachagizwa na sekta binafsi. Benki ya Dunia inakadiria kwamba 90% ya kazi zote duniani katika mataifa yanayoendelea zinaletwa na sekta binafsi na sisi hata Watanzania hapa ni mashahidi kwa sababu kazi nyingi na ajira nyingi zipo kwenye sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile sekta binafsi ndiyo ambayo kwa takwimu inachagiza zaidi kwenye upatikanaji wa kodi na mapato kwa Serikali duniani kote na hayo siyo maneno yangu. Mataifa makubwa ama mashirika makubwa ya kitaifa ambayo tumeyakasimu madaraka kwa mfano *Economic Cooperation and Development* yamethibitisha, kwa mfano kodi ya makampuni ambayo hata sisi tunaitegemea kwa kiasi kikubwa kwenye kuendesha Serikali yetu duniani kote inaletwa zaidi na sekta binafsi. Kwa hiyo ni masuala ambayo kwa kweli yamejiweka wazi na yamejitanabaisha wazi kwenye umuhimu wa sekta binafsi na ndiyo maana makubaliano yoyote yanayoingiwa yanachagiza zaidi ushirikishwaji wa sekta binafsi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia 75 ya miundombinu yote duniani kwenye uwekezaji mkubwa wowote duniani unamilikiwa na sekta binafsi na ndiyo sekta ambayo imetusaidia kukidhi changamoto za miundombinu ambayo nchi yoyote duniani inayo kwa sababu sekta binafsi ndiyo ambayo inaweza kuwekeza zaidi kwenye teknolojia, ujasiriamali kwa sababu ndiyo ambayo inaweza kukidhi ushindani kuliko uwekezaji ambao unaweza kufanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo ushindani unaokua kwa kasi sana kutokana na maendeleo ya teknolojia huwezi kuacha kushirikisha sekta binafsi ili kukabiliana nao. Kila siku tunasimama hapa na tunasema jamani teknolojia haipigwi ngumi. Ukipiga ngumi teknolojia kwa zama hizi za sayansi na teknolojia umeenda na maji. Huwezi kuacha ku-*involve* sekta binafsi ili iwekeze kwenye teknolojia iweze kutusaidia sisi kusonga mbele kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu Tanzania ni nchi ya 141 kati ya nchi 177 kwenye uwekezaji wa biashara na mojawapo ya changamoto kubwa zinazotufanya tuwe nyuma ni changamoto za uendeshaji wa bandari kwa sababu ndiyo eneo ambalo lilipaswa kutuingizia mapato makubwa kama Taifa na ili tuweze kutoka kwenye 141 na tuende kwenye nafasi ambazo zinatufanya kama Taifa tuweze kushindana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kazi yetu kama Bunge ni kushauri na kwenye makubaliano haya kwa kweli tutasimama kidedea. Baada ya miaka 60 ya Uhuru hatuwezi kuendesha nchi yetu *conventional,* hilo ni jambo ambalo haliwezekani. Ni lazima tukubali Tanzania siyo kijiji. Ni lazima tukubali sisi tupo kwenye ushindani. Haiwezekani meli zichukue siku 4.5 mapaka tano kushushwa bandarini, wakati jirani yetu anatumia siku moja kushusha mzigo wake. Kwa akili ya kibiashara wafanyabiashara wote hawawezi kuja kwako kwa ajili ya biashara. Kwa hiyo, lazima tukubaliane wote tunasemaga hapa Serikali haiwezi kuwekeza yenyewe kwa sababu ya namna ambavyo Serikali zetu zinajiendesha, kwa hiyo ni lazima tu-*involve* sekta binafsi kwa sababu ndiyo sekta ambayo kwanza inafanya *research* kwa haraka sana na pia inaweza ku-*adapt* kwa sababu ya sera ya sekta binafsi inaweza ku-*adapt* mazingira kwa haraka sana, kwa hiyo hata teknolojia ina *adapt* kwa haraka mno. Kwa hiyo, ni lazima tu-*involve* sekta binafsi katika kuhakikisha maendeleo ya Taifa letu tunapiga hatua kwa kasi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, humu ndani hakuna Mbunge ambaye siyo Mtanzania, wote sisi ni Watanzania na hakuna Mbunge ambaye hana uzalendo kwa mama Tanzania, kila Mbunge humu ndani ana uzalendo wa hali ya juu sana kwa mama Tanzaniam kwa hiyo hakuna Mbunge ambaye anaweza kuidhinisha mkataba unaoenda kuuza rasilimali kubwa kama ya bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nielezee kuhusiana na mkataba; mkataba ule hakuna Mbunge humu ambaye ni mangungu wa Msovero hajui kusoma, wala hajui maslahi ambayo sisi kama Taifa tunaingia. Ule mkataba ni kwa sababu baadhi ya watu

wanapenda kuwasomea wenzao baadhi tu ya vifungu labda nusu kingine hamalizii, lakini nitakupa mifano miwili tu ya umakini wa ule mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tukienda kwenye ku-*solve* migogoro inayohusiana na mashirikiano kati ya sisi na makampuni ya kimataifa tulikuwa tunatumia sheria za wengine katika kutatua migogoro yetu sisi wenyewe, lakini mkataba huu umesema; migogoro yoyote itakayohusika na uendeshaji wa bandari kwenye mikataba ya *HGA* hata kama tutaenda kutumia usuluhishaji kwenye *platform* za kimataifa, tutatumia sheria zetu za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria ya Uingereza ambayo inasemwa itatumika ni ile kwenye mkataba wa nchi kwa nchi kwa sababu sisi wote ni *independent states,* hatuwezi kutumia sheria ya Tanzania ama sheria ya Dubai kwa sababu lazima twende kwenye *neutral point*. Kwa hiyo, mikataba ya uendeshaji wa bandari itakuwa *determined* migogoro yake kwa kutumia sheria zetu za Tanzania hata kama tukienda *ICSID* ambako ndiyo migogoro mingi inaenda kutatuliwa hata kama tukikaa *South Africa* sheria ambayo itatumika kwanza ni Sheria ya Tanzania. Kwa hiyo, ni mkataba ambao unaangalia maslahi ya Watanzania kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye suala la ukomo; mkataba huu hauwezi kuweka ukomo kwa sababu tutakuwa hatujitendei haki kama Watanzania. Mkataba wa uendeshaji wa bandari ndiyo ambao utaweka ukomo, ukiweka miaka 15 ukomo ina maana mkataba huu miaka 15 ikiisha na mkataba huu utaisha. Sasa leo tuweke miaka 40 uendeshaji wa bandari tunaenda kuweka miaka 25, sasa inakuwaje tujifunge sisi wenyewe? Kwa hiyo, ndiyo maana nasema umakini umefanyika kwenye mkataba huu ili kuhakikisha kwamba maslahi ya Taifa yanalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho Watanzania wana hofu kwa sababu uwekezaji huko nyuma kuna baadhi ya watu wasio waaminifu wamewahi kutuingiza hasara Taifa letu. Kwa hiyo, sasa lazima vilevile tushauri na tutoe angalizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Bunge ni tunaisimamia Serikali na kuishauri, hatuwezi kuhusika kwenye kutunga mkataba halafu baadaye pia tukaja kuusimamia huo mkataba husika, lakini tunataka tuwaambie watendaji ambao wamekasimiwa haya madaraka, huko nyuma kama Taifa tumeingia hasara sana, safari hii tutatoa macho kweli kweli, hatutakubali. Tutahakikisha mikataba yote inayopitiwa na inayopitishwa ina maslahi kwa mama Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo tutahakikisha tunatoa macho, tunasimamia na kama kuna mtendaji ambaye ataweka masuala yoyote ambayo yana maslahi binafsi au kwa kikundi cha watu kwa kweli tutahakikisha wanawajibishwa kulingana na sheria yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph George Kakunda atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kuwa kutoa mfano rahisi, kama ambavyo tunafahamu kwamba Kariakoo ni kitovu cha biashara cha Tanzania nzima na hivyo hivyo Dubai ni kitovu cha biashara cha dunia kwa sasa; kwa sababu gani? Wamefikaje hapo wenzetu? Wamefika hapo kwa sababu ya umahiri na weledi katika sekta ya usafiri na usafirishaji. Leo ndiyo maana utatoka hapa Tanzania utaunganisha ndege Dubai, utafanya *shopping* Dubai, utafanya mambo mengi Dubai. Wamefika hapo kwa sababu ya weledi na umahiri wao na eneo la bandari ni eneo mojawapo la umahiri na ndiyo maana wameweza kuongoza bandari zaidi ya 50 duniani maana yake wana uwezo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kuchangia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa

kwenda Dubai mwaka jana kuhudhuria *Dubai Expo* na msingi wa kuhudhuria *Dubai Expo* ndiyo ukamfanya apate nafasi ya kuzungumza na mtawala wa Dubai mambo mbalimbali ya ushirikiano kati ya nchi zetu mbili ambayo mazungumzo hayo ndiyo yaliweka msingi wa hati ya makubaliano *(MoU)* iliyosainiwa mwezi wa pili mwaka jana na baadaye mazungumzo yakafanyika kati ya wataalamu wa nchi zetu mbili ambao wamekuja sasa na haya makubaliano kati ya nchi mbili ya *IGA* ambayo tunayaridhia leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kama asingeeda Dubai mwaka jana inawezekana pengine leo tusingekuwa tunajadili namna ya kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, katika mkataba huu baada ya kuwa nimeusoma na kusikiliza maelezo mengi ya wanasheria nimeuelewa vizuri katika maeneo mawili makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza la kiutawala; mkataba huu kiutawala ni mkataba kati ya nchi mbili; Tanzania na Dubai na ni mkataba ambao unatoa mwongozo kwa mikataba rasmi, mikataba mahususi ya miradi ambayo itatekelezwa baadaye. Kuna upotoshaji ambao ulifanyika uonekane kama vile mkataba huu tayari ni mkataba wa kazi. Huu siyo mkataba wa utekelezaji, huu ni mkataba ambao unatoa mwongozo wa jumla kwa miradi yote ambayo Kampuni au Shirika la Bandari na hii Kampuni ya *DP World* wataingia baadaye katika maeneo mbalimbali na mikataba hiyo ambayo itaingiwa baadaye ndiyo itakuwa na muda maalum wa utekelezaji. Inaweza ikawa miaka 10 kufanya kazi hii, miaka mitano kufanya kazi hii, miaka 15 kufanya kazi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakimaliza *phase one* ile ndiyo wataingia sasa kutokana na matakwa ya bandari yetu, Shirika la Bandari letu litakavyopendekeza ndiyo wanaweza wakaenda kwenye maeneo mengine kutoka kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala hili kumekuwa na upotoshaji mwingi sana wa makusudi na wengine siyo wa makusudi kwenye mitandao ya kijamii, na mimi napenda nizungumze mambo mawili makubwa ambayo yamekuwa yanapotoshwa. Wanasema mkataba huu huu haurekebishiki lakini ukisoma kifungu hapa kimesomwa, Waziri kasoma na wewe mwenyewe kila mtu hapa amesoma kifungu cha 22 kinaruhusu marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba huu hauvunjiki, kifungu cha 23 kinaruhusu unaweza ukavunjika lakini kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwenye kifungu cha 20 na kifungu cha 20 kimeweka umakini kwamba huwezi kuamka tu asubuhi unavunja mkataba, haiwezekani. Tutumie kwanza njia za kidiplomasia na diplomasia ya uchumi tumeanza kuizungumza zaidi ya miaka 20 iliyopita itatumika. Tukishindwa kwenye diplomasia twende kwenye Kamati yetu ya Pamoja kati ya Tanzania na Dubai. Kamati ya wataalamu wakae pamoja wajadiliane kwa undani, ikishindikana kabisa ndiyo tutakwenda kwenye usuluhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hawa wenzetu, kwa kweli ukisoma baadhi ya maoni ya wenzetu nadhani walikuwa wanapotosha wengine ni wanasheria kabisa walikuwa wanapotosha tu kwa makusudi, mwingine anasoma kifungu hakisomi mpaka mwisho, mwingine anasoma kifungu kimoja kinachofuatia hasomi, halafu anajaribu kupotosha umma wa Watanzania, hilo lilikuwa ni kwa upande wa kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuichumi mkataba huu unapata uhalali wa kiuchumi *(economic justification)* kwa sababu kuu tatu; kwanza mkataba huu kama mwongozo unaweka nidhamu katika usimamizi wa fursa za uwekezaji na kusimamia viwango vya utendaji. Mkataba huu kama mwongozo unalazimisha taasisi zitakapokuwa za utekelezaji kuwa na weledi, umahiri na uzalendo katika utendaji wa kazi wao. Kwa hiyo, sisi kama Wabunge tukisharidhia mkataba huu tunaipa Serikali *mandate* sasa ya kwenda kuingia mikataba midogo midogo ambayo watazingatia viwango, watazingatia umahiri, watazingatia weledi katika utendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hii ndio ilitumiwa na wenzetu wale tunaita *Eastern Tigers* Singapore, Indonesia, Korea ya Kusini na Malaysia walipiga hatua kutokana na mwenendo kama huu na huko nyuma tulifanya makosa, tulikuwa tunaingia mikataba wakati mwingine moja kwa moja bila kuwa na mkataba wa mwongozo kama huu, matokeo yake tukawa tunapata shida mbalimbali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali imeona kwamba ili turekebishe shida ambayo tulikuwa tunazipata tuwe na mwongozo wa jumla ambao utakuwa ni kama *reference* kwa mtu yeyote ambaye atakuwa anafanya makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wawekezaji duniani kote wanahitaji mambo manne makubwa; kwanza wanahitaji umeme wa uhakika, na ndio maana Serikali inawekeza matrilioni kwenye uzalishaji wa umeme; tuwe na uhakika, waje hapa wakijenga viwanda na wanahitaji umeme, wapate umeme wa uhakika wazalishe bidhaa. Vitapita wapi? Vitapita humu kwenye njia za usafi na usafirishaji. Wanahitaji gharama nafuu za usafiri na usafirishaji ndio maana tunaboresha bandari, tunaboresha viwanja vya ndege, tunaboresha barabara, tunaboresha reli ya *SGR,* yote hii tunafanya kuweka matrilioni huko ili kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu wanahitaji malighafi ya uhakika sekta ya kilimo na sekta za uzalishaji. Lingine ambalo tunafanya vizuri Tanzania wawekezaji wanahitaji nguvu kazi yenye ujuzi na ndio maana tunawekeza kwenye *VETA* kila Wilaya, kila Mkoa ili nguvu kazi iweze kupatikana. Kama wawekezaji watawekeza kila mahali, lakini bandari yetu bado inafanya kazi kwa kusuasua kama ambavyo ilivyo sasa hivi tutakuwa uwekezaji kwenye sekta nyingine huu tunafanya kama bure. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ili tupate faida nzuri kabisa kwenye hizi sekta nyingine zote ni muhimu sana tuboreshe bandari kama ambavyo Serikali inajitahidi sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadri jambo zuri, kila mtu ukimsikiliza anakwambia ni jambo zuri. Upinzani unatoka wapi? Ni maeneo manne; kuna watu wanafaidika na hali iliyopo sasa hivi, changamoto za bandarini pale kuna watu wanafaidika, hao lazima wapige vita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna watu wengine wanapinga ni washindani wa bandari yetu wa pande zetu, wengine majirani zetu, kwa hiyo lazima wapinge. Kuna watu wengine ni wapinzani wa hii kampuni ya *DP World* na wapinzani wa Dubai, lazima wapinge. Lakini hivi mimi najiuliza ingekuwa Serikali imeleta mwekezaji anatoka Canada au anatoka Ulaya au Marekani hivi angepingwa kiasi hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kwa sababu sasa tumegeukia kupata fursa mpya za uwekezaji ndio maana upinzania umekuwa umezidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, la mwisho kuna wivu wa kisiasa kwamba sasa kumbe chama hiki kiko madarakani kinaanza kufanya vizuri zaidi wanaanza kukosa fursa, nashukuru sana naunga mkono hoja, tuwe makini, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge niwaombe wale mnaoendelea kuleta vikaratasi vya kuomba kuchangia hata wale ambao nimeshapokea sitaweza kuwafikia wote. Kwa hiyo, kuanzia sasa hata usihangaike kuleta kwa sababu hata nikikuweka kwenye orodha zitakufikia. Sawa, ahsante sana.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Halima James Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwenye hili nichangie kama ifuatavyo; kwanza ni muhimu ikaeleweka kwamba watu wanaokosoa jambo wana nia njema kuliko watu wanaoona jambo na kulichukulia kama lilivyo, hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili tuna Watanzania wenzetu wako huko nje wana akili nyingi sana, pia inawezekana kutuzidi hata sisi tuliokuwa huku ndani. Kwa hiyo, ni muhimu sana kama Taifa tukajenga utamaduni wa kuheshimu kila mchango wa Mtanzania, vilevile tukauchuja pale ambapo tunaona hauna maslahi mapana kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja hazijibiwi kwa ukali, hoja inajibiwa kwa upole,…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Nani amesimama kwa ajili ya taarifa? Aah Mheshimiwa Halima Mdee kuna taarifa kwa Mheshimiwa Ummy Nderiananga.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa dada yangu Mheshimiwa Mdee kwamba hamna mchango ambao umedharauliwa au kupuuzwa ila ambacho tuna mashaka nacho ni michango ambayo ni ya upotoshaji na tunaendelea kuelimishana katika eneo hilo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati imesema kwamba makubaliano hayo kwa sababu tukipitisha

kama Bunge maana yake yanaenda kuwa makubaliano ya Kimataifa yaani Sheria ya Kimataifa inaenda kuwa *International Law.* Sasa tunaambiwa makubaliano yanaweka msingi wa kisheria na sio mkataba na sisi ndio tunazungumza hapa hapa kwamba kama msingi una mashaka, kama msingi una matobo, kama msingi hauna madhara kitaifa hiyo mikataba mnayosema tutaletewa hapa Bungeni lazima iendane na sheria hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni kama vile hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano hapa, Katiba ni msingi mama wa sheria zote. Haya makubaliano hapa ndugu zangu ndio msingi wa kitakachokuja. Nitatoa mfano *scope* Ibara ya nne inasema; "*Scope of this agreement is to facilitate the implementation of areas of co-operation set out in an Appendix I of this agreement.*"

Mheshimiwa Spika, *Appendix I* ni sehemu pacha ya huu mkataba ama haya makubaliano. *Appendix I* ina *phase* mbili; ina *phase i* na ina *phase II. Phase I* inahusu yale magati ya bandarini ambayo pamoja na mambo mengine yanahusisha magati ambayo Tanzania tulikopa *almost* trilioni moja kuyafanyia maboresho. Ndugu yetu wa *TPA* kwa haya maelezo anapewa *terminal* ya maboti na anapewa na *terminal* ya *passengers* ya abiria, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili *phase II* inahusisha ku-*develop,* ku-*manage* na ku-*operate mind you* kwa sheria ya sasa hivi ya bandari ya 2014 na kama tulivyofanya marekebisho mwaka 2019, majukumu haya ni ya bandari. Kwa hiyo, tunasema kama nia ni njema kwa nini *aspect* ya *PPP* isionekane kwenye makubaliano yanayokuja kuwa sheria ya Kimataifa? Makubaliano haya bandari ni *facilitator* tu wa mazungumzo makubaliano haya hata umiliki wa ardhi, bandari hajulikani yuko wapi. Kwa hiyo nilisema *phase II…*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima subiri muda wako unalindwa, Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema, maana tuko hapa tunataka kujua vifungu vipi vina shida humu ndani. Umeeleza

kuhusu *scope of co-operation and implementing entities* ukasoma kifungu kidogo cha kwanza, hebu kirejee tena.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kidogo cha kwanza si ndio *phase I project?*

**SPIKA:** Ndio ulioisoma, irejee tu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, imesema *development, management and operation of General Cargo Berth one to four in container terminal berth five to six. Development Dhow Wharf Terminal and Passengers Terminal of Dar es Salaam Port to be operated by TPA. This two* ndio anapewa *TPA* ku-*operate* kwa mujibu wa hii hapa.

**SPIKA:** Kwa hiyo, kwa ulivyosoma umeanzia huku *article 4* ukasoma *sub-article one,* ukatupeleka huku kwenye *appendix I.* Umetueleza kwamba Serikali ilishawekeza pesa trilioni zaidi ya moja na hilo eneo ndilo analopewa huyu *DP World.* Hebu nieleweshe mimi hapo anapewa kufanya nini? Kwa vifungu hivi tulivyonavyo mbele yetu anapewa kufanya nini?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba unilindie muda wangu.

**SPIKA:** Unalindwa kabisa usiwe na wasiwasi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nimesema hivi *article 4* ni *scope of co-operation* ambayo *article 4* inaenda sambamba na *appendix I. Appendix I* imeelezea maeneo ya ushirika ambayo katika *appendix I specific* eneo naomba niruhusu…

**SPIKA:** Nakusikiliza, umenisikia nimeongea, nakusikiliza. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *appendix I* katika moja, mbili, tatu mpaka saba kwenye *appendix I TPA* amepewa namba *two,* ndio atakayo…

**SPIKA:** Sawa sasa twende hapo mimi nataka pale kwenye pesa ya Mtanzania ambayo ili…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, pesa ya Mtanzania...

**SPIKA:** Subiri kwanza, mimi si nakusikiliza, tunasikilizana kwa sababu jamani leo sio michango ya kawaida humu ndani, ni michango kwa ajili ya hili azimio hili. *(Makofi)*

Mmi nisaidie jambo moja kwenye lile eneo ambalo pesa zimetumika za Mtanzania, si ndio? Hapa *phase I project* na wewe uko hapo inasema hapo kwenye moja; "*development, management and operation*" hapo. Huku mwanzoni kwenye *article 4* inasema; *"The scope of this agreement is to facilitate the implementation of areas of the co-operation set out in appendix I to this agreement, co-operation between this two entities*" kama hivyo ndivyo na yale maelezo ambayo umeyatoa mwenyewe kwamba Serikali imeshawekeza pale. Kwa nini wewe, mimi nauliza ili nielewe maana tunataka tujue vifungu gani tupitishe, vingine vipi tukatae.

Kwa nini usifikiri lile eneo anaenda kwenye *operation* maana hapa yako mambo matatu, kuna *development, management and operation?*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, mimi siwezi kufikiria kwa niaba ya Serikali kwa sababu hoja…

**SPIKA:** Ehe sasa ngoja hapo hapo umemaliza vizuri.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu hapa…

**SPIKA:** Ngoja niweke sasa vizuri hoja yangu ili nikupe muda uendelee kumalizia. Ndio maana Waheshimiwa Wabunge sasa hivi tunatoa maoni yetu ili Serikali yale ambayo wanaenda kuingia kwenye hiyo mikataba wakayatazame. *(Makofi)*

Huu mkataba haujaweka msingi kwamba kwenye eneo hili la zero mpaka *berth* sijui saba huu mkataba hauwezi kusema anaenda kufanya nini pale, wala hausemi. Unaeleza maeneo ambayo anaweza kupelekwa sio anapelekwa. Kwa nini anaweza kupelekwa? Kwa sababu kifungu cha tano ambacho kimetajwa sana huko nje kimeweka misingi ya hayo ili waweze kukubaliana, lazima wakubaliane kamoja kamoja ambayo hawakubaliani anaweza kupewa mtu mwingine au akaendelea yeye mwenyewe *TPA. (Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Halima nilitaka mimi mwenyewe nielewe vizuri maana leo lazima tuongozane vizuri humu ndani, nje mambo ni mengi. Nilitaka nielewe pale kwenye uwekezaji na maadamu umesema kwamba huwezi kujua Serikali inapeleka wapi, haya endelea na mchango wako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, huu mkataba ni baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai na *DP World* ametajwa hapa *specifically.* Kwa hiyo, hata kama tutazunguka mbuyu kwa kiwango gani tunachozungumza hapa hivi vitu vyote viwe vitatu, kiwe kimoja, viwe viwili lazima apewe. Kwa hiyo, tukipitisha mkataba atapewa hilo ni la kwanza.

**SPIKA:** Lazima apewe unaitoa wapi Mheshimiwa Halima? Maana lazima tukae sawa leo ile lazima apewe yeye umeitoa wapi? *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, unajua kwa nini naitoa kwenye haya makubaliano, wamekubaliana ushirika wa mambo yote yaliyozungumzwa hapa.

**SPIKA:** Hapana twende vizuri, vifungu humu ndani vimetaja mambo mahususi kwamba ni lazima yeye apewe; wapi pamesema?

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa taarifa.

**SPIKA:** Twende tu vizuri mimi na wewe ni mwanasheria, ingawa wengine wote watatutaka sisi wanasheria tukae sawa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru wewe ni Mwanasheria tena mbobevu. Haya makubaliano Bunge leo likipitisha *whether* pameandikwa ni lazima apewe, ama asipewe haya makubaliano yametoa ulazima yakipitishwa kwamba chochote kitakacho…

**SPIKA:** Huo ulazima ndio nataka kujua unapoutoa mwanasheria mwenzangu, huo ulazima unatokea wapi? *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ni hivi labda…

**SPIKA:** Mimi naweza kukuelewa sana ukisema kwamba yaani huu mkataba ama haya makubaliano yanaweka msingi ili umalizie hoja yako kwa maana ya kwamba kwa sababu haya yanaweka msingi, naishauri Serikali inapoenda kuingia mkataba itazame hapa na hapa na hapa. Ukisema inaweka ulazima hilo mimi siwezi kukukubalia kwa sababu sijapaona humu ndani panapoweka ulazima, sijapaona.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, aah *come on* Mheshimiwa …

**SPIKA:** Nani anataka kuzungumza?

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Jerry Silaa.

**SPIKA:** Sasa taarifa unanipa mimi au Mheshimiwa Halima?

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mheshimiwa Halima Mdee.

**SPIKA:** Ngoja tumalize kwanza hoja yetu, kabisa ni uhuru wa maoni ila leo Bunge hili ni la tofauti linatoa maoni na linatoa elimu kwa umma kwa sababu kumekuwa na upotoshaji mkubwa sana. Kwa hiyo, tunajadiliana kwa uhuru kabisa leo lazima tutoke humu ndani sisi wenyewe tukiwa tumeelewana, Mheshimiwa Halima. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa maneno yako mwenyewe kwamba mkataba huu ama makubaliano hayo yakipitishwa yanaweka msingi, na naweka msisitizo yanaweka msingi na huo msingi unatakiwa uzingatiwe kwenye sheria ama mikataba mingine yoyote midogo midogo itakayokuja. *(Makofi)*

Kwa mantiki hiyo kama msingi una matatizo na nashukuru Profesa hapa wakati anazungumza amesema kama kuna matatizo maana yake tunajua kuna matatizo…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, tunapaswa kukubali kwamba…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza, la pili,…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie.

**SPIKA:** Inatokea wapi taarifa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Aah Mheshimiwa Patrobass Katambi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kumkumbusha na kumpa taarifa Mheshimiwa Halima msomi mwenzangu katika kile kwenye suala la msingi ambalo anausema, ni vizuri akajua *all contracts are agreements, but not all agreement are contracts.* Kwa sababu msingi wake ni kwamba ukisoma hayo anayoyaeleza, ukisoma *article one* ya sheria hii ambayo itasomwa pamoja na kifungu cha tano utaangalia pia na huku kwenye *appendix* kwenye *phase I* ndipo utapata tafsiri ya pamoja kwenye hili. Hata kwenye eneo ambalo amezungumza kuhusu ardhi ukienda kwenye *interpretation* inaeleza kwamba *excluding*…

**SPIKA:** Haya ahsante sana kwa sababu taarifa ni moja, umechagua ile ya sehemu ya kwanza, hii ni sehemu ya pili ahsante sana. Mheshimiwa Halima Mdee unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwenye *appendix* hiyo hiyo ambayo inatokana na hiyo *scope phase II* imejumuisha *ports* zingine imejumuisha maziwa na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, nazungumza mawanda…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa bandari ama taarifa ya bandari.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, tuna bandari kadhaa, kama hamtaki tuchangie basi mseme.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane tusikilizane, tusikilizane taarifa hiyo itakuwa ni taarifa ya tatu nafikiri sio, ni taarifa ya tatu na ya mwisho.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, ya pili hujanipa.

**SPIKA:** Sasa siwezi kuwapa wote wawili Mheshimiwa Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, analolizungumza Mheshimiwa Halima la *scope* ya nafasi ya pili maana yake ni kwamba sisi tukishaingia makubaliano Tanzania na Dubai, tukishawapa hawa *DP World* wakifanya, tukijiridhisha, tukatathmini, tukajua wanaweza kufanya vizuri, tuna uwezo wa kuwapa nafasi. Tukiona hawawezi tuna uwezo wa kuwapa kampuni zingine zikafanya kazi hiyo, kwa hiyo asipotoshe, aseme vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, analolisema yeye analisema yeye, halipo hapa. Nimesema *article four* inazungumzia *scope* imerejea *appendix I, appendix I* ina *phase* mbili; *phase* ya kwanza ni hiyo niliyozungumza, *phase* ya pili, *two* inasema; *development, management* and *operation of additional sea and/or lakes ports.*

Mheshimiwa Spika, mawanda yamekuwa mapana kwa bandari ambazo tunazo, Bahari ya Hindi ukiacha hiyo ya Dar es Salaam, kwa sababu hili suala sio la Dar es Salaam, ni Dar es Salaam na bandari nyingine, Bahari ya Hindi tuna bandari 12, Ziwa Victoria tuna bandari 24, Ziwa Tanganyika tuna bandari 19, Ziwa Nyasa tuna bandari 11 hizi ni zile ambazo zimekamilika kisheria. Kwa hiyo, tukisema hili jambo ni la nchi linahusisha bandari, maziwa 66. Kwa hiyo, iko mbele kwa kisheria, ukija ambazo… *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, hayo maeneo yote ni katika huu mkataba, yaani kwa maana ya kwamba Tanzania na Dubai moja?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *Yes,* mkataba huu…

**SPIKA:** Wapi pamesema?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hawaja *mention,* wametoa ruhusa ya jumla...

**SPIKA:** Sasa unaona hiyo ndiyo changamoto? Kama hawajata mbona una *speculate?*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nina *speculate* kwa sababu mimi ninaona mbele. Ninaona mbele kwa sababu gani? *No, no, no* naomba tusikilizane, naomba tusikilizane. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima ngoja, ngoja, ngoja muda ninaozungumza na wewe naulinda usiwe na wasiwasi, muda ninaozungumza na wewe ninaulinda.

Waheshimiwa Wabunge, tuelewane vizuri hili kwa sababu nilishasema mwanzo kwa hiyo nitazungumza nikiwa nimekaa. Kanuni zetu, Kanuni ya 111 inasema hivi; "Majadiliano wakati wa kujadili hoja ya kuridhia mkataba yatahusu masharti ya mkataba husika." *(Makofi)*

Kwa hiyo, hakuna mkataba nje wa haya unaoweza kuzungumziwa kwenye ngazi hii, lakini nimwelewe yeye anasema kwamba anaona mbali. Kwa hiyo, anatoa maoni yake Waheshimiwa muyasikilize upande wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nisikilize, unajua vitu vingine vinachosha. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, mimi niseme tu mkataba huu tofauti na wengi wanavyosema kwanza haufanani kabisa na Mkataba wa *TICTS,* wala usifananishe, kwa sababu wa *TICTS* zilikuwa zinahusu zile *berth* nne, hii ni kubwa na ni pana kuliko *TICTS*. Sasa kama huu mkataba unagusa Mtwara, unagusa Dar es Salaam, unagusa Tanga, unagusa Mwanza, unagusa Kigoma na *Lake Tanganyika* ipo na *Lake Nyasa, Lake Victoria* ipo kwa nini lisizungumzwe kwa mapana yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili kuna hiki kitu kinaitwa *Exclusive Economic Zones,*kwa taarifa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, nilikuwa najishawishi kukuongeza muda lakini sasa namna unavyosema mkataba huu unahusisha hizo bandari na kifungu huna, unasema unawaza baadaye kwa kweli kengele ya pili imeishagonga sekunde thelathini malizia sentensi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ulisema unanilindia muda wangu...

**SPIKA:** Nimeshaulinda.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nasema hivi mkataba huu hili suala *serious* sana, na nilisema wakati ninaanza tukipitisha leo tuna nafasi ya kubadilisha, lakini hatutabadilisha, tukipitisha leo maana yake huu unaenda kuwa mkataba ama makubaliano ya Kimataifa ambayo yako *legally binded*. Kwa hiyo, chochote kilichotajwa humu kiujumla jumla kwa sababu kimetajwa kiujumla jumla, kinachohusu *ports* zetu zote kinahusika…

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, muda wako umekwisha, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi

Mwanaisha Ulenge na Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye jambo hili zito na kubwa kwa manufaa ya nchi yetu.

Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutuwezesha kukaa na kujadili jambo hili, lakini nitumie nafasi hii kwanza kabisa kusema kwamba wakati tunajadili jambo hili Watanzania wenzetu walio wengi wapo wanatusikiliza na wanatusikiliza ili kupata ukweli wa mambo mengi yaliyopotoshwa kabla ya sisi Wabunge wao hatujakaa hapa kujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii kuwaambia wananchi wa Tanzania kwamba walituamini wakatuchagua ili tuje tufanye kazi ya kuisimamia Serikali, kutunga sheria na kupitisha bajeti. Wapo Watanzania wengi kama alivyotoka kusema Dada yangu Halima Mdee huko nje anasema wapo wenye akili nyingi wengine kuliko sisi, hao wenye akili nyingi kuliko sisi, wenye akili za kati na wenye akili za chini hawakuja humu wakatuleta sisi ili tuwawakilishe wote wenye akili nyingi, akili za kati na akili za chini.

Ndugu Watanzania leo tunazungumza kwa niaba yenu, tukiwa na kiapo tulichoapa mbele ya Spika, kulinda Katiba na sheria za nchi. Lakini tukiwa na dua ambayo huwa tunaiomba kila siku ya kuliombea Bunge na kumuombea Rais wetu ili Mungu atupe hekima na busara za kufanya kazi zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini si hilo tu ninyi kila siku mmekuwa mkituombea, mashehe, mapadri, wachungaji na viongozi mbalimbali na wananchi mbalimbali ili tuweze kuifanya kazi yenu vizuri. Kama mlimsikiliza mtu yeyote kuhusu jambo hili, sasa tusikilizeni sisi mliotuamini, naona upotoshaji ni mwingi sana huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyotangulia kusema msemaji wa kwanza Profesa Kitila Mkumbo, Rais wetu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na chama kinachotawala Chama cha Mapinduzi haviwezi kuja hapa na mkataba wa kutokomeza nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais kwa wajibu wake ndiyo msimamizi wa shughuli zote za nchi, lakini ni mfariji na mlinzi wa haki za raia na watu wengine wote ambao wako kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Anafanya kazi ya kuhakikisha kwamba anapo ongoza nchi yake anaangalia kila fursa ya kuvutia uwekezaji kwa manufaa ya Watanzania na tumekuwa tukimwamini hivyo, amefanya kazi kubwa kwenye *Royal Tour* kwa ubunifu wake na leo tunapokea watalii kwa wingi na wamekwenda kwenye maonesho Dubai, amefanya mazungumzo na Mfalme na leo sasa tunaiona nyota ya kusaidia kupata ufumbuzi wa matatizo ya bandari zetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwanza mimi natumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefanya jambo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya ubia huu ambao tunataka kuingia kwa njia ya uwekezaji tulikuwa na ubia huu na Kampuni ya *TICTS* na hao *TICTS* pamoja na kwamba mkataba wao tulikuwa tunautazama kila wakati tunauangalia, tunafanya maboresho lakini bado waliweza kufanya kazi nzuri kuliko tulipokuwa tunaendesha wenyewe bandari asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zinaonesha hapa magati yote haya 11 yalipokuwa yanasimamiwa na *TPA* tulikuwa tunapata gawio la kama bilioni 180; lakini walipoingia *TICTS* wakachukua magati nane tu; gati namba 8, namba 9, namba 10 na namba 11 tukawa tunapata bilioni 345. Huku tunakokwenda sasa nataka niwaarifu Watanzania kwamba tunakwenda sasa kufanya makubwa zaidi ya yale tuliyokuwa tunayapata kwa *TICTS* maana ingekuwa tunataka yale tungebaki pale pale, tungeongeza mkataba lakini tumeona hapana huku tunakokwenda tutapata zaidi na tutafanikiwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo tunaliona amelisema mtoa hoja, kwamba tumekuwa na tatizo la meli zinazokuja kupakua kwa wakati, wakati mwingine zinakaa mpaka siku tano na kila meli inapokaa siku moja tunakuwa-*charged* dola 25,000 kama shilingi milioni 60 za Kitanzania. Ikikaa siku tano ni milioni 300 za Kitanzania, hizi gharama zote mwisho wa yote zitakwenda kuingia kwenye gharama za mlaji wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka kupata mwarobaini wa tatizo hili na mwarobaini wa tatizo hili ni mkataba huu ambao Serikali yetu na Serikali ya Dubai inaweka *framework* ya kutengeneza mikataba ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kutumia nafasi hii kuipongeza sana Serikali na kusema kwa kweli tupige ndiyo, twende haraka tuweze kufikia hatua hii, na katika yote haya masuala yanayohusu ajira za Watanzania yamezingatiwa, masuala yanayohusu usalama wa Taifa letu yamezingatiwa, masuala yanayohusu kodi yamezingatiwa tunataka nini zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi uliniteua miongoni mwa kundi la Wabunge kushirikiana na Serikali kwenda kuangalia sekta binafsi inavyowekeza kwenye bandari. Mimi nilikwenda India, tukaenda *Adani Port,* tukaangalia kazi kubwa inayofanywa na wale *Adani Port* kule Jimbo la Gujarat tulikwenda kule Gujarat tukaangalia ile *port* yao wanavyoendesha. Kazi kubwa sana inafanywa na mimi nilidhani wale ndiyo watafika mahala watapata, lakini katika uchambuzi Serikali imeweka makampuni mengi ikaona hawa *DP World* wa Dubai ndiyo ambao kwa kweli kupitia Serikali ya Dubai wanaweza wakafika mahala huko mbele wakatusaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema Serikali imefanya vizuri kuwa na makubaliano na Serikali ya Dubai ili makubaliano haya sasa yakatupe mikataba ya uwekezaji kwenye bandari zetu na maeneo mengine hatua kwa hatua na kila mkataba uwekezaji wake utakuwa na uwekezaji wake, utakuwa na gharama zake, utakuwa na malipo yake, utakuwa na faida zake na utakuwa na

muda wake. Haiwezekani leo mtu awekeze katika bandari kama hivyo walivyokuwa yanasemwa hapa tumeishawekeza trilioni moja, inaweza ikawa na kazi yake Serikali ikaona huyu nikuendesha tu kwa sababu sisi tumeishawekeza na kama huyu ni kuendesha utatulipa kiasi hiki kule ambako wanawekeza, wanaleta mitambo, anatengeneza sijui hivi unajua gharama ni hii, kwa hiyo, atapaswa kulipa kiasi hiki haya yote Serikali yetu imesheheni wataalamu wa fani mbalimbali ambao tunawaamini chini ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema kwamba tumechelewa, tupige hatua haraka, tuweze kufika mahala tupate mwarubaini. Tukiweza kumaliza tatizo la baadhi ya bandari zetu huku tutaweza kumaliza hata matatizo ya bandari za kwetu kule Kigoma kwenye *Lake Tanganyika*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia katika jambo hili tukufu kabisa lenye mustakabali mpana wa maendeleo ya Taifa letu. I(Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kupata fursa ya kuchangia katika makubaliano ya kukubaliana na nchi ya Dubai katika kuendesha baadhi ya maeneo katika bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba naomba ni–*declare interest,* niliyesimama mbele yenu niliwahi kuwa *Manager* wa Usimamizi wa Mradi katika Bandari ya Dar es Salaam upanuzi kutoka gati…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, ngoja tuliweke vizuri hili.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Ndiyo.

**SPIKA:** Tunapojadili mkataba wa namna hii, ukasema unataka kuweka maslahi yako wazi na ni mkataba unaohusu uwekezaji, maana yake una maslahi ya kifedha kwenye hawa wawekezaji moja wapo.

Sasa kama ni hoja ya kusema umeshawahi kufanya kazi mahali, ama unamfahamu fulani nenda moja kwa moja, ondoa hayo maneno yako unataka kuonesha maslahi yako kuwa wazi kwenye jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Dhamira yangu ni kutaka kusema kwamba ni nina uzoefu na bandari na yale upanuzi uliofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam na katika kitu ambacho ninakikumbuka mpaka leo ni kwamba Bandari ya Dar es Salaam imepanuliwa kutoka gati *zero* mpaka gati namba 7 na bado tunakwenda kupanua gati namba 8 mpaka gati namba 11. Haya yanayokwenda kufanyika sasa hivi ya kutafuta mbia kuendesha Bandari ya Dar es Salaam katika baadhi ya maeneo ninasema Mama Samia anaendelea kuwa mtekelezaji wa yale aliyokwishatangulia akiwa kama Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Mama Samia amefanya mengi katika *SGR* na katika mengine yote ambayo ameshirikiana na mtangulizi wake yeye akiwa Makamu wa Rais, naomba niwaambie Watanzania popote mlipo na hili la uwekezaji wa kumpata mbia katika Bandari ya Dar es Salaam ni sehemu ya muendelezo ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu gani? Makubaliano na liyetupa fedha ambaye ilikuwa ni Benki ya Dunia mwaka 2017 alipotupa mkopo wa dola za milioni 305 katika Bandari ya Dar es Salaam kutengeneza ile jumla ya milioni 421 ambayo ndiyo trilioni moja ya Tanzania ambayo imetumika

kuwekeza katika Bandari ya Dar es Salaam miongoni mwa *loan agreement* iliyoingiwa na ile Benki ya Dunia ni kuhakikisha kwamba tunaweza kurudisha fedha ile tuliyowekeza pale kwa haraka na Benki ya Dunia katika makubaliano yale imezungumza na sisi tukayakubali kwamba bandari ile itaendeshwa kwa ubia, imesema wazi kwenye *loan agreement* mwaka 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kwamba Serikali haikukurupuka wala Mama Samia hakukurupuka kama ambavyo wengi walidhani wamefikiri. Mama Samia anafanyakazi kwa mujibu wa maandiko ambayo ameyakuta muda mrefu katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba uwekezaji wote mkubwa unaofanyika katika Taifa letu na katika nchi zozote duniani hauwezi kufanyika kwa kukurupuka tu, ni lazima tafiti, ni lazima stadi zifanyike, ni lazima tutafute *traffic forecasting,* haiwezekani tufikirie mwekezaji leo kama hatujaangalia Bandari ya Dar es Salaam mwaka 2045 itakuwa na mzigo gani? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie Watanzania, *Port Master Plan* ya mwaka 2008 ambayo imefanyiwa mapitio mwaka 2018 na Mhandisi mshauri anayeitwa *Anova Consult* ambaye wala si Mtanzania, katika taarifa yake ya mwisho yote yanayofanyika sasa hivi katika Taifa letu kuanzia upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara, *SGR* yote yako katika maandiko yaliyofanyiwa tafiti. Serikali haikurupuki, Serikali inafanya mambo kwa maandiko, Watanzania tujifunze kusoma, Watanzania tujifunze kutafuta taarifa, Watanzania tusiishi kwa hofu, tujifunze zaidi hii ni *summary report* hii ni taarifa fupi ya *Port Master Plan* ya mwaka 2008 inazungumza yote hayo na *page* ya 31 mpaka 34 inazungumza suala zima la mzigo utakaokuja Bandari ya Dar es Salaam mpaka mwaka 2045. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile limezungumzwa kwenye *page* ya 32 suala zima la upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na vilevile

katika *page* ya 34 imezungumza suala zima la Bandari ya Dar es Salaam kuendeshwa *under PPP. (Makofi)*

Sasa niwaambie ndugu zangu, Serikali yetu haiongozwi na watu wasiokuwa na akili timamu, Serikali yetu inaongozwa na watu wenye akili madhubuti. Watanzania sisi tusiyumbishwe na kupelekwa pelekwa haya mambo yako kwenye maandishi, tujifunzeni kusoma Watanzania. Inavyoonekana ni kama vile Mheshimiwa Rais amekwenda Dubai, akatekwa tu, akasaini tu yaliyosaniwa, siyo kweli. Ni kumkosea heshima Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mama yule ni mama makini, mama yule ni mama mwenye kuipenda Tanznaia kwa mapenzi makubwa sana. Ni fedheha huku kuendelea kusema kama sisi tunaweza kununuliwa bahasha hii ninunuliwe mimi Mwanaisha Ulenge? Bahasha hii nyepesi namna hii ininunue mimi? *I see,* Watanzania naomba muwe na imani kubwa na Serikali yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ina masikio na Serikali hii ina macho, Serikali hii ina wataalam, Serikali hii inafanya tafiti. Kwa hiyo, naomba niwaambie Mama Samia ndiyo kidedea wa kutekeleza hata yaliyokuwa yamefichamana. Haya anayoyatekeleza mama Samia yalikuwa kwenye maandishi tangu mwaka 2008, Mama Samia leo anakuja kutekeleza. Mama huyu ni kichwa mwanamama wa Kizimkazi, Mungu anedelee kumsimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tabia Watanzania ya kujilinganisha na Singapore kwamba mwaka 1960 Singapore ilikuwa masikini kama sisi. Tumekuwa na tabia ya kujilinganisha na *South Korea* kwamba mwaka 1960 ilikuwa kama sisi, lakini tumekuwa na tabia ya kujilinganisha na Malaysia kwamba walikuwa kama sisi.

Sasa katika kitabu hiki nilichokishika mkononi hapa ambacho kimeandikwa na Mtanzania mwenzetu aliyefanya tafiti za Afrika nzima...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**Spika:** Malizia kwa sekunde 30.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** ...ambacho kinaitwa *Poverty within, not in the skin* kinaeleza kwamba Malaysia, Singapore *and South Korea* walitoka katika umaskini ule kufikia walipofikia sasa kwa sababu waliamua kuingia katika *advancement in technology*.

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, na mimi pia nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia maoni yangu kwenye Azimio hili la Bunge ambalo tunategemea kulipitisha muda mchache unaokuja.

Mheshimiwa Spika, labda mimi nianze pia kama wengine waliochnagia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanaya ya uwekezaji. Nakumbuka mwaka jana kwenye *Dubai Expo* ilisainiwa *Memorandum of Understanding* takribani 35 yenye thamani ya trilioni 17.5. Zimesaini Wizara nyingi tu, Wizara ya Nishati ilisaini na Wizara nyinyine. Sasa tunapoona mikataba hii inatekelezwa na ilisainiwa Watanzania tukajulishwa tukafurahi halafu wananyanyuka wengine wanaanza kusema imekosewa nadhani iko haja ya kuelimishana vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nichukue nafasi hii kuomba sana Watanzania, hili Bunge ni Bunge lao, wametutuma humu kwa ajili ya kuwawakilisha, yapo mambo mengi sana yamesemwa huko nje tumeyasikia na wamesikilizwa kwenye

mitandao na sehemu nyingine. Tuwasihi watupe nafasi na sisi pia, maana kama wametuamini kama wawakilishi wao kwenye kupitisha miradi ya maendeleo, kwenye kufanya uwakilishi ambao wamekuwa wanategemea tunaufanya vuizuri na kwenye hili pia watupe nafasi ya kutusikiliza na kutuamini. Siyo pale tunapochangia mitandao iko macho, Bunge la CCM, Bunge la hivi hapana, Bunge la CCM hili limejenga madarasa, limefanya shughuli nyingine zote ambazo zinaendelea watupe nafasi tutoe ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, mimi kwa upande wangu ni *engineer* kwa hiyo nitaenda zaidi kwenye vitu vyangu vya kihandisi ambavyo vinahusu bandari, mambo haya mengine ya mikataba wengi mmeongea sana kwa kiasi kikubwa mimi nataka nuiongelee *stage* hii ya *engineering* na hasa mambo haya ya uhandisi ambayo yanafanyika pale.

Mheshimiwa Spika, wengi kwanza wameuliza kile kiambatanisho au *appendix number one*. Naielezea *appendix number one* tu kwa haraka ya maeneo yale ya kimkakati ambayo uki–*refer article* namba tano *right to develop, manage or operate*. Kwa hiyo, kuna mojawapo kati ya hao yanaweza yakafanyika. Wameelezea *appendix* namba moja na *specifically phase one*. Kwa hiyo, ukiangalia *scope* ilitaja *appendix* yote, lakini *development* inataja *phase one* ya *appendix* ile. Kwa hiyo, *phase two* ukija kuisoma ni pale *TPA* atakapoamua ndio maana kule mwisho ukisoma *phase two* kwa mwisho, mambo ya maziwa mambo ya nini endapo *TPA* mwenyewe ataamua atawashirikisha. Kwa hiyo, siyo sehemu ya *scope*.

Kwa hiyo, tukienda namba tano hii ndiyo inayoelezea maeneo ambayo tutashirikiana ambayo amepewa haki yeye ya kwamba amepewa ile *exclusive* kwa *phase one for twelve months*, sasa wengi walikuwa wanauliza hapa.

Mheshimiwa Spika, kwanza ukiongelea *phase one* ni sehemu ambayo nchi hii tumewekeza kwa kiasi kikubwa pale, lakini ukweli uliopo ni kwamba hatukuwa na vifaa kwenye bandari hii. Tumechimba kina cha bandari yetu imefika mita 15 leo kina kilipo

unaweza ukashindana na Mombasa. Mombasa nao wana mita 15, tulikuwa na mita 11 sasa tumeenda mita 15. Gati Namba 8 mapaka 11bado lina mita 11. Mwekezaji huyu Gati Namba 8 mpaka 11 kuna vifaa vilivyokuwa na mwekezaji yule aliyepita, huwezi kumleta mtu ukamuweka kwenye sehemu ambayo tayari una vifaa, lakini kwa sababu sisi upande wa kwetu pamoja na kwamba tulikuwa na kina cha mita 11 tulikuwa tuna-*miss* vifaa vingi sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nikiongea hapa sehemu hii tunahitaji tuwe na *ship to shore gantry crane* sita, lakini tulikuwepo nayo moja na *gantry crane* moja inauzwa shilingi bilioni 42 za Kitanzania. Tulitakiwa tuwe na *rubber tag*, *gantry crane* ziko 20 tulizotakiwa tuwe nazo, tunazo mbili tu. Vifaa vyote nilikuwa nimepiga hapa hesabu na moja inauzwa bilioni saba. Ukienda kwenye *mobile harbor crane* zinatakiwa ziwe 11 tulikuwa nazo sita, moja inauzwa shilingi bilioni 15 kwa haraka na hesabu za kawaida tu za haraka haraka tunahitahji uwekezaji wa vifaa vya shilingi bilioni 435 sehemu hii tu ambayo mmempa huyu mtu aje kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sehemu hii ilikuwa muhimu mpe yeye aje na vifaa aje awekeze. Hatuwezi kwenda benki kuchukua shilingi bilioni 435 unaenda kuweka pale halafu unampa mtu aende kwenye kina kifupi. Kina hiki cha mita 15 leo tuko kwenye *position* ya kushindana na Bandari ya Mombasa. Meli kubwa zilizokuwa haziwezi kuja hapa zinashusha Mombasa zitaanza kuja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo cha kwanza *efficiency* ya bandari yetu inakwenda kuongezeka kwa hili tu. Nadhani niliweke sawa hilo ndio maana nikasema ile *exclusivity* tunayosema kwanza ni ya *twelve months* ndugu zangu. Tangu kusainiwa mkataba huu, tuliposimama hapa *exclusivity* ya *phase one* kwao imebaki ikifika tarehe 28 Oktoba ule uhalali wa kwao wa kutoa *phase one* walioi-*operate* wao utakuwa umeisha endapo hatujakubaliana. Kwa hiyo itakuwa wazi kwa *TPA* kuweza kutafuta wawekezaji wengine au yeye mwenyewe aombe, lakini bila *exclusivity,* liko wazi hili.

Mheshimiwa Spika, sasa sielewe wanasheria wanakwama wapi wanatafsiri vitu vingine ambavyo havipo. Kwa hiyo mimi niombe Watanzania wanaotusikiliza huko nje muelewe Bunge hili lina wanasheria, Bunge hili lina wahandisi, Bunge hili lina madaktari, hatuwezi kwenda kupeleka nchi sehemu ambayo sisi wengine bado ni vijana wadogo tunataka tuone Taifa hili likisonga huku tuki-*enjoy* na watoto wetu na vizazi vyetu vikiwa vinaenda mbele. *(Makofi)*

Kwa hiyo tuombe hili tuwe na imani na Bunge hili tuwe na imani na Serikali yetu, kuna wengine wamenda mbali zaidi anasema mkataba huu huwezi kujitoa, lakini vifungu hivi viko wazi.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu umeelezewa kabisa kwamba *duration and determination* iko hapa namba 23 imeeleza; *subject to paragraph two* ukienda namba *two* hii *the expiration of all HGAs and all projects agreements subject to any additional or extension,* ikisha-*expire* hii mikataba midogo tunayosaini huu mkataba mkubwa, hii *agreement* hii kubwa haina kazi tena *it is obvious* na iko hapa, sasa hatuelewi hawa watu haya mambo wanayatoa wapi na tumeenda mbali zaidi mtu anasema huu mkataba huwezi kujitoa mkataba mpaka umekupa *room* ya kufanya *amendment article 22* kwamba kama kuna jambo hata leo kama limeshapita bado *states* wanaweza wakakaa wakafanya *amendments* ya baadhi ya mambo, ipo hapa.

Mheshimiwa Spika, tukienda *article 23* namba nne ambayo imeongelewa sana na watu wengi, mimi siyo mwanasheria lakini usisome ukaishia hapa tu, kulikuwa na kipengele kimeendelea; *notwithstanding the foregoing, any dispute between State Parties in respect of such circumstances shall be dealt with in accordance with the requirements of Article 20 of this Agreement.* Unarudi nyuma *article 20* inasemaje; kutakuwa na mazungumzo kati ya viongozi wetu endapo tutashindwana kwenye hiyo *article 20* ndio twende kwenye *arbitration.* Sasa kwa nini mtu anasema mkataba huu ni kifungo hauwezi kutoka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi tu sasa niongee *with experience* pia. Kwa nini tumeenda Dubai? Hilo ndiyo jambo la muhimu pia wananchi wajue *why Dubai today*?

Mheshimiwa Spika, wote mnajua mizigo inayokuja kwenye Bandari ya Dar es Salaam, wafanyabiashara wanajua, sehemu kubwa ya mizigo yetu unapoongelea kutoa kontena moja Shanghai, China kuja Dar es Salaam, *20 feet* kontena inaenda dola 2,500 mpaka dola 2,800 na kontena la *40 feet* mpaka inaenda dola 4,500. Unapoongelea kutoa mzigo ule ule kuja Mombasa *20 feet* dola 1,200 wao kati ya *20 feet* na *40 feet* kontena, zinatofautiana kati ya dola 300 na dola 400; hawafikishi kontena hata la *40 feet* kwa dola 2,000; utashindana vipi mtu anayepeleka mzigo Congo atakubali kuleta Dar es Salaam hapa?

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu kama tunaipenda hii nchi tuache siasa, mimi siyo mwanasiasa, mimi ni mhandisi mambo yangu yamenyooka hivi. Mbili jumlisha mbili ni nne haibadiliki. Tukitaka kwenda mbele tuache siasa, tukileta siasa kwenye masuala makubwa kama ya Taifa hili, ndugu zangu Taifa hili tunaliangamiza, unapoenda mbele kwa nini mizigo yetu imekuwa inachelewa kwa sababu cha kwanza mfanyabiashara anachotaka *other than saving cost* anachotaka na mzigo aupate kwa uharaka zaidi. Wote ni mashahidi *trans-shipment* ya mizigo ya Tanznaia ni Jebel Ali Dubai. Mizigo mingi inayotoka Bara la Asia, inayotoka Ulaya mingi inapita Dubai Jebel Ali, ikishafika Jebel Ali ndio wanai–*consolidate* kutafuta meli ya kuileta huku kwetu. Mizigo imekuwa ikichelewa Jebel Ali *not less than three to two weeks sometimes*. Mfanyabiashara ambaye ameagiza mgigo mwenzake ameshapokea Kenya yeye yuko Congo anasubiira mzigo umekaa Dubai wiki mbili unauleta Dar es Salaam, utoke Dar es Salaam uje huku, nani atapitishia mizigo kwenye bandari hii?

Mheshimiwa Spika, *no wonder* ukisema wenzetu wale majirani zetu kwenye nchi wanazozihudumia mpaka wameweka kwamba na Tanzania wanaihudumia, sasa unaposoma *profile* ya mwenzetu mwenye bandari kama sisi, *competitor* wetu, anasema anatuhudumia na sisi kama Taifa na sisi ndiyo tuna bandari

maana yake ni nini? Anatuondolea baishara, *sometimes* tusiingie kwneye mkumbo.

Mheshimiwa Spika, ameongea vizuri sana Mheshimiwa Jerry pale, sisi tunaowakilisha hii nchi kwenye Mabunge ya nje tunajua upinzani tulionao na wenzetu wa jirani. Ni lazima kama Taifa ifikie *stage* tusimame, hawezi kuja mtu anayeongea lafudhi ya nchi jirani, mnamuita mmbobezi na mtaalamu wa sheria, mlitaka Bunge tujadili kitu kabla ya kuja humu? Leo kimekuja, Serikali imesema, Wabunge tumeona kazi imeishia hapa leo, tusingeweza kwenda kwenye mitandao Wabunge na Serikali tukaanza kujibu kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi kwa kuomba tunapoenda kumalizia hasa kwenye utekelezaji, nimefika katika bandari ya Suez nchini Misri mwaka 2019 pale kwenye *Suez Special Economic Zone*. Wale watu wamefanya uwekezaji mkubwa sana, pale kazi anayofanya anafanya *APM,* hii kazi anakuja kufanya *DP World* hapa Suez anafanya *APM*. *APM* ni kampuni ya Uholanzi kutoka *Maersk Group,* wao walichokifanya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kw Amuda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, namalizia; wao wamekodisha miaka 45 kwenye upande ule wa makubaliano, sasa mimi nilikuwa nataka niweke maoni. Maoni yangu ni mawili; cha kwanza, kwenye *contracts* ambazo mnaenda kuingia kati ya *TPA* na *DP World* tunaomba tupate *specific time,* nilikuwa na *suggest not more than 25 years* kwa kuanzia na mikataba iwe *revisited after every five years.*

**SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umeisha, ahsante sana. Muda wako umekwisha nimekupa sekunde 30 na zenyewe umeshamaliza sasa naona unaanza tena maelezo badala ya kusema kwa *point.*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Cecil Mwambe ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niungane na wenzangu, lakini kabla nataka na mimi niweke msingi kama ambavyo makubaliano haya yanaweka msingi na msingi wangu nitauweka kutoka kwenye vitabu vya Mwenyezi Mungu, nita-*refer* Biblia.

Mheshimiwa Spika, Hosea 4:6 inasema; "Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa, kwa kuwa wameyakataa maarifa." Mathayo 22:29 inasema; "Yesu akajibu akawaambia mwapotea kwa kuwa hamyajui maandiko." Yohana 8:32 inasema; "Tena mtaifahamu kweli na hiyo kweli itawaweka huru." Methali 11:9 inasema; "Asiyemcha Mungu, humpoteza jirani yake kwa kinywa chake, bali wenye haki watapona kwa maarifa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanzia hapo, hofu zetu zote ni kutokuwa na maarifa na Serikali inachokifanya sasa hapa leo imetupa maarifa ya kutosha, tuondoe sasa ile dhana yetu tuliyokuwa nayo kwenye vichwa, tukubali kuingiza vitu vipya, ili tusiendelee kudanganywa na kuangamia.

Mimi kwa kuwa somo la sheria na mimi pia nilipata kidogo ukakasi, lakini sikutaka kuangamia kwa kukosa maarifa. Nilijipa muda wa kusema nitafute maarifa. Kwenye huu mkataba kwanza kitu cha kwanza unachotakiwa kujua unakwenda kwanza malengo yake ni nini.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi tusio wanasheria, watu wa biashara tunapoandika *research* huwa kuna *general objectives* na kuna *specific objectives. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la jumla la mkataba huu ni kati ya nchi na nchi na hawa nchi na nchi wanaingia makubaliano ya kushirikiana kwenye masuala ya biashara kwenye maeneo ya bandari, *automatic* bandari zinakuwa kwenye maziwa, kwenye

bahari, kwenye mito, hiyo ni ya ujumla na hii utaipata kwenye ibara ya pili; malengo ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, ukija Ibara ya nne ya mkataba ambayo inaeleza mawanda au upana ndiyo hiyo tulikuwa tunasema *scope*, hii imejaribu kuelezea mawanda ya huu mkataba lakini imekwenda *specific* kwamba hawa nchi wameshaingia makubaliano na wenzetu wale wanafikiri kwamba kampuni ambayo labda inaweza tukaanza nayo ni ya kwao ya uwekezaji kwenye bandari ambayo ni *DP World*.

Mheshimiwa Spika, wakai-*bind* kabisa kwa *specific objective* kwamba ninyi mkienda Tanzania mtaingia mkataba baada ya kuwa hatua zote zimefikiwa pamoja na Bunge kuridhia, mkataba wenu mtakwenda kuingia kwenye maeneo haya. Ndio hiyo *appendix* moja tuliyoisema imeeleza kwa undani, lakini kilichonifurahisha katika kujua malengo, siyo kwamba bandari zote au maziwa yote au Tanga sijui huko Mtwara wapi zimeingia, hapana. Kwenye hiyo hiyo *article four* namba mbili inasema; *Tanzania will inform Dubai of any other opportunities relating to ports, freezones and logistics sectors in Tanzania to allow Dubai or Dubai entities to express interest and submit proposals for consideration in respect of such other opportunities.*

Mheshimiwa Spika, kwamba sisi Tanzanaia ndiyo tutakuwa na mamlaka ya kuwaambia wale Dubai tuna fursa nyingine huku labda kuna Bandari ya Mtwara tunaomba kwa sababu hapa mmefanya vizuri, tunaomba basi na Mtwara mkafanye kitu kama hiki. Wao watakuwa na *responsibility* ya kutafuta mtaji na kwenda kuendeleza, kusiamia na kuhakikisha wanaboresha. Hivyo ndivyo mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wanasheria wakisoma wanatudanganya kwamba maziwa yote yamechukuliwa, bahari zote zimechukuliwa, mbona namba mbili hamuiangalii kwamba *consideration* ni sisi ndio tutakao-*inform* hawa kwamba tuna *opportunities* nyingine katika hizi *water bodies* za uwekezaji wa bandari, hapo mimi nikajiridhisha, nikaondoka na kuangamizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mwanasiasa kuna hoja nyingine utaifikiria kwamba je, ardhi ya Watanzania inachukiliwa? Maana ardhi ikishachukuliwa Tanzania maana mimi watu wangu watakaa wapi? Wapiga kura wangu Iringa watakaa wapi au wataenda wapi? Nikaenda Ibara ya nane inaeleza ukurasa wa 18 haki ya ardhi, lakini hapa Ibara hii inaitaka Serikali ya Tanzania kuhakikisha hatua muhimu zinachukuliwa ili kuwezesha *DP World* kupata haki ya matumizi ya ardhi. *Yes,* lazima sisi kama Watanzania tuwa-*guarantee* wale matumizi ya ardhi yetu. Wanaleta mitambo, sawa, watawekeza pale. Sasa kama hatutawalinda kwa sheria zetu tukaendelea kuwa na urasimu, tukaendelea kuwa-*disturb,* unategemea wawekezaji wataendelea kuwepo?

Mheshimiwa Spika, sisi tumepewa jukumu la kuwalinda hawa wawekezaji na ni jukumu la msingi, sio kumiliki ardhi. Katika hii ukurasa wa tisa inaeleza tafsiri, hakuna mtu anakuja kumiliki na kuchukua ardhi ya Watanzania. Ukurasa wa tisa, *Land Rights* inavyoeleza *interpretation* inasema; "*Land Rights shall mean all those rights (excluding rights of ownership of the land in Tanzania.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imeondoa hilo suala la umiliki wa ardhi, kwa hiyo wao watakuwepo kwenye matumizi ya ardhi. Sisi tunasoma hivi, ili tusiangamie hata kama sio wanasiasa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, manufaa kwa Watanzania...

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba huu mkataba na anavyozungumza vizuri sana

Mheshimiwa wetu, jina lake gumu sana, Mheshimiwa Jesca, ni kwamba wanaangalia *logistic* ya *from* Dar es Salaam na kufikisha mzigo Burundi, Rwanda kote na Uganda. Kwa hiyo, lazima wafikirie kwamba ili iwe ni *efficient* lazima waweze kuboresha bandari za Ziwa Victoria, kama itakuwa hivyo na pia waweze kuweka maeneo ya bandari kavu sawasawa na kadhalika na pia kuwezesha hizi *export … (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru sana kwa Taarifa; fahari ya wazee ni mvi kichwani, hiyo ndio hekima ya mzee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwamba wewe huwezi kumpa mtu atoe makontena pale usimpe sehemu ya kuweka makontena. Huyu *DP World* ana bandari kavu Rwanda, usimpe *access* ya treni kwenda Rwanda kupeleka makontena yake; ana-*supply* na *South Africa,* sijui na wapi huko na Djibouti huko ana mikataba inaendelea, usimpe *access* kwamba atakwenda hadi huko kupeleka makontena, haiwezekani. Kwa hiyo, ndio maana kuna *appendix II* kwamba, badae tutakuja kuendelea kuongea sisi tutakapokubali tutamshirikisha yeye.

Mheshimiwa Spika, kama mwanasiasa manufaa hayo mengine ya ushirikishaji, tatizo kubwa tulilonalo saa hizi ni ajira. Mimi nikaangalia changamoto, hivi mimi watu wangu wa Iringa wanaosoma pale Chuo cha Bandari, Dar es Salaam watapata kazi au ndio zinakwisha au wanafukuzwa?

Mheshimiwa Spika, nikaangalia Ibara ya 13 - ushirikishwaji wa wazawa, ajira na majukumu kwa jamii. Tunahangaika hapa kutoa ajira, tunaleta wawekezaji ili tupate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anasema ibara hii, inaelekeza kuwa mikataba itakayosainiwa ya utekelezaji wa mradi lazima iainishe mpango wa ushirikishwaji wa wazawa katika utekelezaji wa mradi

husika, unaona? Na maeneo yafuatayo yatapewa kipaumbele kwenye hii *article*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo inasema kutoa kipaumbele kwa kampuni za ndani katika zabuni na ushauri pale ambapo makampuni hayo yatakidhi vigezo. Baadhi ya miradi inayokwenda kutekelezwa iwe imetolewa kwa kampuni za ndani na raia wa Tanzania; kutekeleza mpango wa mafunzo ya uendelezaji wa raia wa Tanzania; kusaidia kujenga uwezo wa vyuo/mafunzo katika tasnia ya usafiri majini na usafirishaji; na kuwezesha tafiti na uhamasishaji wa teknolojia kwa wazawa.

Mheshimiwa Spika, hii tayari msingi umewekwa wazawa wetu sisi…

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, wazawa watapata ajira, lakini na wale waliokuwepo wataboreshwa kwa kupewa mafunzo. Maana asije akasema nimeweka kitu cha kisasa hapa Mtanzania hawezi, tunataka ampe mafunzo aweze kuki-*operate* kile kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka nini?

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na kwamba atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana, lakini nikiri kwamba una Wabunge wazuri sana, tangu asubuhi saa 3:00 mpaka saa hizi nafikiri asilimia kubwa ya Watanzania wameelewa azimio lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme ukweli, nitazungumza kidogo wala sitachukua muda wangu mrefu. Ni kweli nimemsikiliza mtoa hoja Mheshimiwa Waziri, nimemsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu wamezungumza jambo kubwa, lakini mimi nafikiri nitaliongeza kidogo kwamba huu sio mkataba, huu sio mkataba wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, haya ni makubaliano kati ya nchi na nchi. Tumepata Uhuru mwaka 1961 Waheshimiwa Wabunge, nina uhakika Serikali zote zote zimeingia makubaliano kama haya, ni kwa sababu tu tulikuwa hatuletewi hapa kuridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano, Serikali ilishawahi kuingia makubaliano na nchi ya Marekani kama haya haya upande wa afya; Serikali ilishawahi kuingia makubaliano kama haya na Canada upande wa elimu, hakuna kitu kipya Waheshimiwa Watanzania; na Serikali ilishawahi kuingia makubaliano kama haya na China upande wa biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Watanzania wanachanganywa, lakini hili jambo la makubaliano ni jambo la kawaida kabisa na ninaomba Watanzania muone kwamba kipindi hiki linaleta hekaheka kwa sababu imepitishwa hapa turidhie. Hii ni mara ya pili tunaridhia.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Issa Mtemvu.

**TAARIFA**

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, mchangiaji anachangia vizuri sana, eneo la historia kwa makubaliano kama hayo unayoyasema, hata juzi tu tunayo makubaliano kama haya ya bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Ohima, Tanga. Kwa hiyo, ni makubaliano yanayofanana kabisa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naipokea Taarifa hiyo na tena ninakumbuka vizuri tuliridhia.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Watanzania wetu, wapiga kura wetu msichanganywe, hakuna kitu kipya hapa. Hapa kitu kinachosumbua watu Awamu ya Sita inakwenda kushika nchi tena, hakuna kitu kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge Serikali ya Chama cha Mapinduzi sio wajinga, wanaingia uchaguzi mwaka ujao, wana uchaguzi mwaka 2025, walete bomu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawawezi kuleta bomu, hiki kitu ni kitu kinakwenda kutuimarisha, na Waheshimiwa Wabunge mkakitumie vizuri mtakapoomba kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongee jambo la pili; mimi nimewafurahia Watanzania sana, nimewapenda Watanzania sana kwa sababu Watanzania wameonesha hofu yao, wameonesha hofu yao kubwa, wakamfanya na Rais amefurahi sana, wameifanya na Serikali imejua Watanzania wanataka nini. Kama mmegundua, mimi nimewasikiliza kwa siku zote nikitika nikirudi nyumbani nawasikiliza kwenye njia nyingi, Watanzania wanaipenda nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanafahamu kama bandari ndio lango kubwa la mapato ya nchi yao. Kwa hiyo, wameona aah, bora tuseme, mimi ambao nawaweka kando ni wale wapotoshaji wale siwasifu, lakini Watanzania nimewapenda mno, mlitumia haki yenu ya Kikatiba, mmezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Watanzania kilichowasumbua ni hofu; ahh hii bandari yetu, hiyo mikataba itakayoingiwa itakuwa mikataba mibovu, itamaliza nchi yetu, ndio kimewasumbua Watanzania, lakini naomba niwatoe hofu Watanzania kwa kitu kimoja kikubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nimetulia kwenye mitandao nikasema hivi Rais hajasema kitu chochote kuhusu mikataba?

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nimnukuu Mheshimiwa Rais. Naomba nimnukuu Mheshimiwa Rais na kwa sababu yeye anazungumza kwa sauti ndogo na mimi nizungumze kwa sauti ndogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza Mheshimiwa Rais jana *ITV* wamemleta kwenye kipindi cha mubashara, Rais anasema hivi; "Jamani mikataba hii ina aina zake, unajua kabisa mkataba wa aina hii hauwezi kuwa na vifungu hivi vikawa ndani ya huo mkataba, lakini unaukuta mkataba wa aina hiyo na kuna kifungu cha ajabu ajabu kimo ndani ya huo mkataba ambacho hakipaswi kuwa ndani ya huo mkataba, lakini umepita kote, njia zote na mkataba ukaenda ukafanya kazi na sasa waliofanya wanadai ni kimkataba, ni kimkataba, kwenye mkataba ipo. Sasa unawapa watu wengine, hebu someni huu mkataba, wanasema huo mkataba mama haukupaswa kuwa na vifungu hivi. Sasa unawauliza ilikuwaje vikaingia? Wanaangaliana machoni. Dhambi zetu sisi wenyewe, sisi wenyewe tunauwa nchi yetu, sisi wenyewe. Unaruhusu vifungu vya ajabu vinaingia kwenye mikataba isiyopaswa, kwa hiyo, huku kwenye mikataba kuangalieni vizuri," mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais ameshawaonesha Watanzania kwamba hataki mikataba mibovu, alilizungumza hili kabla hatujafikia kujadili hili azimio hapa. Naomba Watanzania wawe na uhakika kwamba huyu siye, hatakubali mikataba mibovu. Wawe na uhakika kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inakwenda kuleta ufanisi ndani ya bandari zetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na n awaomba na Waheshimiwa Wabunge tusimameni imara tuipe nafasi Serikali ifanye kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, watu wasije wakapata wasiwasi nimesimama wakajua wanakatwa.

Wako wageni wetu ambao wamefika hapa, nataka niwatangaze, ili kama wana ratiba waweze kuendelea.

Kwanza nimeambiwa kuna mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambaye sikumtangaza, Mwanasheria wa Wizara, Mohamed Salum, sijui kama ameshaenda kukaa huko, lakini tunakukaribisha sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni hawa wanatoka *IPU - Inter Parliamentary Union* ambao ni Umoja wa Mabunge Duniani.

Yupo Ms. Cynthia Lopez Castro ambaye ndio Rais wa Wabunge Wanawake huko kwenye Umoja wa Mabunge Duniani, karibu sana. Haya, asanteni sana. *(Makofi)*

*Okey, that is a sign that they approve your coming but also they appreciate your visit. So Ms. Cynthia Castro you are very welcome to the House. (Applauses)*

*Okey, she is also a member of the Congress of the Union of Mexico. So she is also a Member of Parliament. She has come together with a Right Honorable Anna Bake who is the Former Speaker of the Australian Parliament. Thank you for coming. (Applauses)*

*They also have Mr. Masheke Masinjila, Gender Expert,* ahsante sana. *(Makofi)*

*There is also Ms. Graca Sanchez staff from the IPU Secretariats, thank you so much. (Makofi)*

*Ms. Caren Shika Gomes staff from the IPU Secretariats. You are all welcome to the Parliament of Tanzania and thank you for the program that you have for the women. I think you have seen some of them already contributing in the House and I believe the*

*training that they are going to receive they are even going to be more vibrant than you have seen them now. (Makofi)*

Asanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na uchangiaji.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Cecil Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Jaqueline Msongozi Ngonyani ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, na mimi kama Wabunge wengine wote tuliopata nafasi ya kuchangia leo kwanza nikushukuru sana, lakini jambo la pili, kama ambavyo unetuongoza kwamba tuna wajibu sasa wa sisi jambo la kwanza kabisa kuisaidia Serikali yetu kutoa tafsiri sahihi kwa watu wanaofuatilia jambo hili ambalo liko mbele yetu kwa sababu kwa bahati mbaya kabisa lilianza kwenda mitaani ama duniani pasipo sisi Wabunge kupata tafsiri sahihi ama kuelewesha kinachoendelea, na kwa bahati mbaya mikataba hii na hasa zaidi huu mkataba wa makubaliano ulioko mbele yetu kati ya nchi ya Dubai na Tanzania wa kushirikiana katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi ulipata kwenda mtaani kabla sisi wengine hatujauona.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kidogo kwanza kuhusu mimi mwenyewe binafsi. Mimi nilipata nafasi ya kuwa *opposition* kabla sijarudi tena kwenye chama chetu, chama tawala, Chama cha Mapinduzi na bado niko kwenye ma-*group* ambayo kuna mchanganyiko wa watu, kuna watu wa Chama cha Mapinduzi, lakini pia kuna watu wa *opposition*.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza na mimi nilipopata kusikia ama kuona kwenye ma-*group* haya watu wakivutana kuhusiana na masuala haya ya makubaliano kati ya nchi ya Tanzania na Dubai hata mimi nilishtuka kwa sababu nilikuwa sijui nini kinaendelea. Nikajipa nafasi ya kusoma na kujifunza, tukakutana na wataalam wakatuelewesha.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana watu wachache waliamua kuchukua vipengele vinavyowafurahisha wao au vile wanavyoamini kwamba vina *controversy* na kuvipeleka kwenye *public* badala ya kusoma tafsiri sahihi ya kila jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajaribu kusema tu kwenye mambo machache na nitajikita kwenye *article 21* ya mkataba huu pamoja na *article* ya 22; na niwaombe Watanzania wenzangu, hasa tuliopo kwenye yale ma-*group* tuliyobishania haya mambo na wenyewe wakaangalie halafu baadae tupate tafsiri ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo nataka niliweke sawa ni hili ambalo limekuwa likipotoshwa mitaani kwamba mkataba huu utatekelezwa kwa kutumia Sheria za Uingereza. Mimi sio mwanasheria, lakini walau Kiingereza ninakifahamu, ukisoma *article* ya 21 ambayo iko kwenye ukurasa wa 28 kwa Kiingereza na wewe ni mwanasheria, utaniongoza. Inasema hivi;"*The governing law of this agreement shall be English Law whereas the governing law of each HGA* kwa maana ya *Host Government Agreement and the relevant project agreement shall be in the laws of Tanzania. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri isiyo sahihi sana ni kwamba makubaliano haya kati ya nchi ya Tanzania…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe ngoja. Sasa hapo usiseme kwa tafsiri isiyo sahihi, sema kwa tafsiri isiyo rasmi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri isiyo rasmi, nashukuru kwa kunirejebisha.

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri isiyo rasmi sana kipengele hiki kinataka kusema kwamba makubaliano haya yaliyofanywa kati ya nchi ya Dubai na Tanzania yatakuwa kwa kutumia *English Law,* lakini wanachokisema hapa ni *common law* kwa sababu Dubai wana sheria zao na Tanzania tuna sheria zetu, kwa hiyo, itatumika *common law* itakayoweza kuziongoza nchi zote mbili kwenda

kutekeleza majukumu waliyokubaliana hapa. Hiyo ni sehemu ya kwanza, kwa hiyo, ule upotishaji, yale maneno kwamba mikataba hii itafanywa kwa kutumia lugha ya Kiingereza, sio sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipengele hicho hicho tafsiri yake ni kwamba sasa ndio maana pale wanasema kuna *Host Government Agreement,* tutakapofanya utekelezaji wa vile vipengele vidogovidogo kati ya Bandari ya Tanzania na Bandari ya Dubai au wale waendeshaji kutoka Dubai itatumika Sheria ya Tanzania kwa sababu mwekezaji atakapokuja Tanzania hatua ya kwanza atakayoifanya ni kusajili kampuni yake *BRELA*. *BRELA* inatumia sheria za Tanzania kwa hiyo, hili nalo lazima likae sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo halikuwekwa vizuri sana lilikuwa…

**SPIKA:** Sasa kwa sababu umesema pia, nikusaidie…

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ndio, naomba unisaidie.

**SPIKA:** Hicho kifungu chako kiunganishe na kifungu cha tano, ukurasa wa 16. Kifungu cha 5(2) na chenyewe soma.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, Ukurasa wa 16. Kama ulivyoniongoza, *article 5* inayosema kuhusu *Rights to Develop, Manage or Operate.*

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa 16, kifungu kidogo cha pili, kama ulivyoniongoza kinasema hivi, *"The State Parties agree the implementation of plans for development of the projects by DPW is subject to the conclusion of definitive Project Agreements, Land Rights and HGAs for each relevant project."* *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa mikataba hii ndio inaendana na kile kifungu, itakayoingiwa hapa. Sheria zitakazotumika ni za Tanzania. Haya ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kuniongoza.

Mheshimiwa Spika, na jambo la pili ambalo limekuwa linaleta sintofahamu ni kuhusu suala la *exclusivity*. Kuna wanaodai kwamba *DPW* wamepewa haki ya kutokuingiliwa milele, yaani kwamba pasitokee mtu mwingine yeyote katikati atakayetaka kufanya kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye mkataba huu kwa uelewa wangu, na ilivyo huku ndani ni kwamba kipindi hiki cha majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusiana na uwekezaji unaotakiwa ukafanyike bandarini, kipindi cha miezi 12 pasitokee nchi nyingine hapa katikati kutaka kuonesha *interest* au kutangaza kwamba anaweza akaja na yeye kutaka kuwekeza kwenye eneo hili ambalo ni eneo la *phase one*. Hii nayo naomba ikae hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na baada ya hapo sasa naomba nitoe ushauri wangu kwa Serikali; kama ambavyo umetuongoza, lakini pia nilisema nitasoma kifungu cha 22, hiki ni cha *subsequent amendment,* na yenyewe imekuwa inapotoshwa na utaniongoza kwenye mambo ya kisheria, mimi nakwenda tu kwenye mambo ya Kiingereza, kinasema hivi; *This agreement may be amended at any time in writing, by the mutual agreement of the State Parties. No amendment to this agreement will have effect without agreement by the signature and the ratification and/or adoption of the appropriate documentation by the State Parties. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hakuna sehemu inayosema mkataba huu ukiingiwa hakutafanyika makubaliano yoyote, makubaliano haya. Kwa hiyo wajibu wetu Bunge kama ulivyosema kutokana na Kanuni zilizopo, tuna wajibu sasa wa kutaka kuishauri Serikali mambo ambayo yakaingiwe kwenye mkataba.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa ambalo napenda kushauri ni kuhusiana na suala la muda. Tutakapoletewa mikataba hiyo midogo midogo lazima ku-*define* muda ili tuweze

kupata uhakika wa tunachokifanya, na ninapendekeza kipindi cha mkataba kiwe ni miaka 25, *renewable* kila baada ya miaka mitano ili kuona sasa kama *performance* inayopatikana ni nzuri, basi tuendelee kwa vipindi hivyo vitano mfululizo kwa miaka mitano mitano. Isiwe ni *open goal.*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, huyu mtu anakuja kuwekeza fedha nyingi sana, na fedha zile nazo ziwe *recouped* kwa muda fulani, *payback period* itakuwepo, kwa hiyo huwezi kusema ni miaka 25, inaweza ikawa hata miaka 30 kutegemea na aina ya mradi na kutegemea kwamba tija ya uzalishaji faida itakuaje.

**SPIKA:** Hapo hiyo taarifa inabidi nimlinde. Yeye kwa mawazo yake kasema tunaweza kuanza na miaka 25, ni mawazo yake. Kwa maana ya kwamba Serikali inavyokwenda kuzungumza na huyu mtu hoja ya muda ni muhimu na yeye anapendekeza miaka 25, wewe umetaja 30, labda ni 50, labda ni 10. Kwa hiyo, wote hatujui, tuniambia tu Serikali ikatazame hoja ya muda.

Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, na ninaamini muda wangu unalindwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ninapenda kupendekeza tunapoelekea kwenye hiyo mikataba midogo midogo ya utekelezaji, suala hili la eneo la bandari, ukisoma kwenye haya makubaliano imetaja eneo kubwa sana, na hata ukienda kwenye *appendix I* na yenyewe imetaja maeneo yaliyopo pale. Sasa wasiwasi uliopo ni kuhusu bandari ambazo

zitakwenda kusimamiwa. Kwa hiyo, mimi napendekeza, kwa kuanzia…

**SPIKA:** Ngoja, eneo kubwa sana ukimaamisha nini?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwenye *cover* ya huu mkataba hapa inasema *concerning,* naangalia tu kile kipengele cha mwisho; *economic and social partnership to the development…*

**SPIKA:** Unasoma wapi, twende pamoja.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwenye *cover* ya makubaliano *(agreement)*.

**SPIKA:** Yaani unasoma jina hapa juu?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, chini kabisa sasa, hizo *lines* mbili za chini.

**SPIKA:** Sawa, enhe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, *improving performance of sea and lake ports in Tanzania.* Sasa unaposema *sea and lake ports in Tanzania,* linaweza likawa eneo kubwa sana kwa maana…

**SPIKA:** Hapana, sasa ngoja, ndiyo twende vizuri.

Hili ni jina la mkataba, huku mbele umewekewa hizo *appendix I,* kama ulivyosema na ukaenda kwenye *phase one,* ukaenda kwenye *phase two;* maana yake huu mkataba humu ndani umetaja mambo ambayo yanahusika. Kwa hiyo, hatuwezi kuweka ile namna ambavyo wale watu wameiweka kule nje. Kwa nini, nimesema Bunge la leo lina kazi mbili, hii hapa na kuuelimisha umma kuhusu mkataba huu.

Sasa mkataba huu pamoja na hilo jina la mkataba huku ndani kumetajwa ni mambo gani yanayohusika, na kichwa cha

habari cha hiyo *appendix I* kinaeleza nini hapo Mheshimiwa Mwambe? Kichwa cha habari cha *appendix I* kinasemaje? Kichwa cha habari tu pale juu. Ukurasa wa 35 hapo juu kabisa, *appendix I.*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa 35 *appendix I* inasema; *Areas of Cooperation.*

**SPIKA:** Ambayo ndiyo maana nikakupeleka kule.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya yote lazima moja moja wakae mezani wakubaliane, ambalo hawakubaliani linakaa pembeni. Ahsante sana.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Kwa hiyo, na mimi nataka kusisitiza kwenye hili, sasa tutakapotoka nje maana yake lazima tuwe *specific* kwa haya mambo, kwamba kuna *areas of cooperation* ambazo zipo na zitakubaliwa kutokana na *appendix I* badala ya ile tunayoambiwa kwamba iko *very general,* tutakwenda kila bandari ya Tanzania, tutakwenda mitoni, kwenye maziwa na maeneo mengine. Jambo hili siyo sahihi, lakini lilikuwa likitembea huko mitaani, kwa hiyo tukasome hii *appendix I* tunaweza tukapata uelewa wa pamoja kwa maana ya sasa bandari zitakazokusudiwa, lakini pamoja na *area* tutakayo-*cover.*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda pia kuliweka sawa ni faida zitakazopatikana kwenye utekelezaji wa makubaliano haya kwa maana ya mikataba. Ukisoma taarifa ya Mheshimiwa Mbarawa kwa maana ya Mheshimiwa Waziri kwenye mikataba hii wakati wa utekelezaji kuna mambo mengi tunakwenda kunufaika na sisi kama nchi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza kabisa ni kupunguza muda wa meli kukaa bandarini ambayo itakwenda kuongeza *efficiency;* lakini suala la pili ni la kuongezeka kwa ajira kwa

Watanzania kutoka ajira 1,500 lakini tutakwenda mpaka ajira 2,950. Jambo lingine inategemea kuongeza mapato ya Serikali kutoka pesa inayokusanywa sasa hivi bandarini ambayo ni trilioni 7.76 mpaka mwaka 2031 kufikia trilioni 26.70.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya ndiyo mambo ambayo sisi kama Watanzania tuna haja ya kuyaweka sawa na ndugu zetu waliopo nje wanaotusikiliza waamini, na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamekuwa wakielezea kuhusu sisi sasa, wananchi watuamini kwamba hatutaweza kwenda kuwaingiza kwenye kitu ambacho siyo kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna Mkataba wa *TICTS* ulikuwa unatekelezwa, sasa hivi tunakwenda na wengine kama watakuwa *DP World* au mtu mwingine atakuwa na *interest* ya kutaka kuja pale, lakini kimsingi hatuwezi kurudia makosa yaliyofanyika huku nyuma.

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles John Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Jaqueline Ngonyani Msongozi, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada iliyopo mezani. Kwanza, niunge mkono wasilisho la Mheshimiwa Waziri, lakini niungane kabisa na mapendekezo ya Kamati mbili zilizotuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya makabrasha na mikataba nimeyasoma sana, na nimshukuru sana *consultant* wangu Mheshimiwa *Advocate* Lujwahuka aliyeniongoza kipengele kwa kipengele. Kwa hiyo mambo ya mikataba sitayazungumza ila nitaunga mkono kwa kupitia *transport and transportation economics,* mambo ambayo mimi nina uzoefu nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la bandari au usafiri na usafirishaji kuna wadau wawili wana maslahi, mmoja ni mwenye mzigo.

Maslahi ya mwenye mzigo ni mzigo wake ufike haraka sana na ufike salama. Mdau wa pili ni mwenye rasilimali au mwendeshaji, yeye ni kupata chumo alilowekeza *return on investment* na faida, na apate faida *justifiable,* siyo awanyonye wale wanaomtegemea. Kwa hiyo, utendaji wa bandari unakwenda namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumze suala lingine kuhusu ushindani wa bandari *(the competitiveness of a port);* hii inategemea namna gani bandari inaweza kupokea meli, inaitwa *vessel turn around,* ikaipokea haraka na kuiondoa ikaondoka haraka, yaani kama mtu anakuja, *captain* anaingia maji ya Dar es Salaam, anaiita Dar es Salaam, Dar es Salaam mnakuja, wanamwambia karibu. Aingie aende bandarini, ashushe, apakie aondoke; hicho no kipimo moja wapo cha *competitiveness of a port. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine linaloleta ushindani wa bandari ni muunganiko wa sekta au miundombinu inayofanya hiyo bandari ifanye vizuri, hapo tuna barabara na reli au mfumo mzima wa *logistics.*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja, Bandari ya Dar es Salaam tumekuwa tukishindwa kuuza matunda na chai itokayo mikoa ya Kusini kwa sababu ya udhaifu wa *logistics,* yaani matunda wanayapeleka Mombasa na chai wanapeleka Mombasa kwa sababu ya *competitiveness* hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa *competitiveness, indicators* nilizozungumza ni *vessel turn around,* lakini kitu kingine ni ukubwa wa mzigo. Bandari inashika mzigo kiasi gani. Kama mzigo ukipakiliwa China au Singapore meli ikajaa, isisimame popote, ina maana mzigo wetu utakuja haraka, kwa hiyo bandari yetu itakuwa *competitive.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama walivyozungumza Wabunge, unakusanya mzigo mzigo kwa sababu huwezi kuwa na mzigo mkubwa na hapo ndipo inapokuja utafute mshirika mwenye uwezo. Siyo siri, *DP World* anakuja; kwa nini? *DP World*

ameshashika mzigo ulipo, ameshashika Rwanda, ameshashika DR Congo, lakini yeye ni mkusanyaji mzuri wa mizigo huko inakotoka.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunamchukua? Ni ili tupate mzigo mkubwa meli ije moja kwa moja Dar es Salaam, na Dar es Salaam iwe *trans-shipment center* ndogo. Kama mizigo inafika hapa basi ipakuliwe hapa na kwenda kwenye nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, *competitiveness* namba tatu ni *speed*. Basi kama meli imepakia kutoka itokako moja kwa moja Dar es Salaam itakuja kwa *speed* kubwa, hakutakuwa na *trans-shipment* ya suala hilo, ilibidi niliseme hivyo.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumza hapa, limezungumzwa suala la TEHAMA. Nadhani Mheshimiwa Mwakyembe atakuwa anasikia, katika watu ambao wamehangaika kuweka mifumo katika Bandari ya Dar es Salaam alikuwa ni Mheshimiwa Mwakyembe. Hata kulazimisha watu walipe kuingiza benki watu walipe kwenye benki watu walikuwa wanakataa. Lakini kwa kuweka TEHAMA, mwekezaji anayekuja anakuja kuweka TEHAMA. Maana yake ni nini? Maana yake anapokuja, kontena likifika mteja ataweza kujua kontena lake limefika, lakini na wenye *interests* zao wataweza kujua kwamba kontena limefika.

Mheshimiwa Spika, sasa niichambue kwa misingi ya kiuwekezaji. Katika uwekezaji tunaangalia suala la kwanza ni ajira, niwatoe hofu na wote walionipigia simu na walionitumia *messages*. Ukisoma kifungu namba 13 uwekezaji huu utaongeza shughuli, lakini kifungu namba 13 kinasema ajira za Watanzania waliopo kazini zitalindwa, lakini na Watanzania zaidi watafundishwa ili waweze kupata kazi pale. Kwa hiyo, kiuwekezaji mimi sina tatizo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili katika uwekezaji, tunakwenda kuzaa bidhaa. Kimsingi katika hii sekta ya uwezeshaji ni *service,* huduma zitaongezeka kwa sababu meli zitakuwa zinakuja kwa haraka zinachukua muda kidogo, kutakuwepo *big volume, the service will improve* kwa sababu una-*order* mzigo

wako, mzigo unafika, unaondoa mzigo wako, unakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuchangamsha uchumi. Hakuna haja ya kuzunguka, tumezungumza kutengeneza *industrial zone,* tumezungumza kutengeneza *logistics center*. Zikitengenezwa watakazi-*manage* ni wananchi, kwa hiyo uchumi utachangamka.

Mheshimiwa Spika, kipengele namba 18 kimezungumza wazi, uwekezaji lazima utupeleke kwenye kulipa kodi. Kutakuwepo na kukusanya kodi. Sasa makusanyo ya kodi yale tunakusanya kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengine wamezungumza, haya ya *disputes.* Lakini niwaeleze wasafiri na wasafirishaji kwamba ukisafirisha mzigo kutoka Dar es Salaam, *transporter,* ukifika kwenye mpaka wa Congo utakwama. Lakini magari yanayotoka Durban hayakwami kwa sababu gani? Ni kwa sababu anayesimamia mizigo kutoka Durban anawasiiana na yule anayekusanya mzingo ndani ya Lubumbashi, mzigo unakusanywa moja kwa moja unaweza kupita. Sisi madereva wetu wanakaa siku 30, hata siku 40 kwenye mpaka wa Tanzania na DRC.

Mheshimiwa Spika, lakini niwambejambo moja, na hili nakuomba Mheshimiwa Waziri unisikilize; mimi katika Ziwa Victoria nina bandari 13, huyo mtu kwenye *phase two*, usisubiri *phase two,* mlete kwenye bandari 13 za kwangu, aende Goziba, aende Rwangamile**,** aende Kyamkwikwi atengeneze bandari ili *marine seaport* aweze kusafiri na kusafirisha watu. *Songoro Marine* anashindwa kusafiri kwa sababu hana *port* nzuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nilisema mwanzoni naunga mkono hoja, lakini Mheshimiwa Waziri

umenisikia, mlete huyo mtu atengeneze bandari kwetu, atengeneze bandari Goziba tusafiri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaqueline Ngonyani Msongozi, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa leo.

Mheshimiwa Spika, nami naomba niwe miongoni mwa wachangiaji kwenye hoja hii ya kuridhia kuanzisha mahusiano ya nchi hizi mbili; Tanzania na Dubai kwa ajili ya suala la uwekezaji kwenye bandari yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi naona kwamba jambo hili limechelewa, yaani kwamba mchakato huu umechelewa kuanzishwa. Nilikuwa nategemea jambo hili lingekuja mapema sana, mara tu baada ya kuanza ujenzi wa *Standard Gauge Railway*. Naomba tu niseme kwamba katika bandari yetu ya Tanzania mpaka sasa hivi, pamoja na kuwa bandari yetu hii imezungukwa na nchi mbalimbali ambazo kimsingi ndio wateja wetu; Uganda, Congo, Zambia, Malawi, Mozambique, Rwanda na Burundi, tuna bahati sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niseme mpaka sasa hivi katika bandari yetu ya Tanzania, uwezo wa bandari yetu kuleta makontena kwa mwaka mmoja, mwaka 2021/2022 makontena ni 820 tu ambayo yaliweza kupakuliwa kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam, ukilinganisha na nchi ya Dubai ambako ndiko mwekezaji huyu tunayemzungumzia *DP World* yeye yupo na anafanya kazi, Bandari ya Dubai sasa hivi inatoa makontena 24,000,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba wenzetu wako mbali sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa tayari tumeshawekeza fedha nyingi sana kwenye *Standard Gauge Railway,* zaidi ya trilioni sita ambazo zinakwenda kuwekezwa kwenye *SGR*. Kwa

hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuona kwamba iko haja ya kufanya maandalizi mazuri ili kutengeneza mnyororo mzuri kwamba bandari yetu ya Dar es Salaam iweze kuongezewa uwezo na hatimaye sasa *Standard Gauge Railway* itakapokuwa tayari imeunganishwa vipande vyote sasa iweze kupokea mzigo kutoka kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam na kusafirisha kwenye nchi hizo nilizozitaja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo mimi nataka niseme kumekuwa na upotoshaji mkubwa sana. Wenzangu wamesema, lakini na mimi naomba niseme kidogo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upotoshaji kwamba kwenye huu mkataba ambao tunauzungumzia leo hakutakuwa na marekebisho yoyote. Mimi naomba wapotoshaji hao wasifanye jambo hilo kwa sababu wanafanya kwa makusudi na wanatambua kwamba kwenye ule mkataba kuna Ibara ya 22 ambayo imejipambanua vizuri, imewekwa wazi kwamba marekebisho yoyote yanaweza yakafanyika wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwenye suala la TEHAMA; kwenye suala hili ni sehemu nyeti sana, kwa hiyo, ninashauri kwenye eneo la TEHAMA hawa wenzetu *eGA* wawepo, lakini pia *TCRA* wawepo kwa sababu mifumo hii tukiiacha iwe *free* kwa mwekezaji itakuwa ni hatari sana kwa usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine naomba niseme, Watanzania wenzangu, Watanzania sisi kama ambavyo mnatambua mmetupa ridhaa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tuko hapa kwa niaba yenu kuhakikisha kwamba mambo yote yanakwenda vizuri na hakuna jambo litakaloharibika, kama ambavyo mlituamini tunaomba muendelee kutuamini. Lakini kama ambavyo mnamwamini Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan tunaomba pia muendelee kumwamini kwa sababu anasimamia misingi ya sheria na misingi ya utawala bora, hakuna kitu chochote kitakachokwenda tofauti.

Mheshimiwa Spika, lakini pia umoja wetu ni lazima tuuzingatie sana, tusigawike eti kwa sababu ya suala hili la

bandari hii ambayo inakwenda kupata mwekezaji baada ya michakato hii yote kwenda.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuombe sana Mheshimiwa Rais wangu, kwa kweli asitolewe kweli reli ya maandalizi na mchakato huu wa kuelekea uwekezaji mkubwa kwa Taifa hili. Wapo wanasiasa uchwara ambao wanapita kila maeneo huko kupotosha na wana kazi maalum ya kuhakikisha kwamba wanamtoa Mheshimiwa Rais wetu kwenye reli ili asiweze kusimama imara katika suala hili la uwekezaji wa bandari kama ambavyo nimezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika wapo madalali; hawa madalali wamekuwa wakitusumbua sana katika nchi yetu na wengine ni majirani zetu tuwaombe watuachie nchi yetu tufanye shughuli zetu kwa usalama na amani kwa sababu hata wakati tulipokuwa tuna mchakato wa *Ngorongoro Conservation* kuhamisha wananchi kule kuwapeleka kule Tanga napo ambao waliingilia, wakaanza kuleta kelele, wakaanza kuleta vurugu. Hatuhitaji mtu yeyote aje atuingilie kwenye nchi yetu, mwacheni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan afanye kazi yake vizuri ipasavyo na kwa vyovyote vile wanatuonea wivu kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu yuko imara, anafanya kazi vizuri sana, amesimama vizuri sana katika kufungua masuala yote ya kiuchumi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaaminim kabisa uwekezaji huu ukifanyika katika nchi yetu ya Tanzania maana yake tunaenda kuingiza pesa nyingi sana. Kwa hiyo, ni lazima wawe na wivu katika masuala mazima ya kiuchumi na hawa madalali wa kisiasa tunawaomba sana kama wamechukuliwa, wamelipwa fedha basi waangalie mambo yao wasiingilie masuala haya ambayo ni masuala yenye afya katika uchumi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo machache naomba nichukue nafasi hii kukushukuru na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mheshimiwa Tarimo ajiandae.

Mheshimiwa Miraji, kisemeo kimegoma. Waheshimiwa Wabunge kama kuna mtu amewasha kisemeo akizime tafadhali.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, washindwe kabisa kwa jina la Yesu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, haya ni majaribu katika dunia, tunamwomba Mwenyezi Mungu atupitishe salama.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi hii, lakini pili kabla sijapongeza kiongozi wetu wa nchi, nianze kwa kueleza kwamba uchumi duniani unaendeshwa kwa misingi mliyokubaliana kama Taifa na uchumi unazingatia maandiko na sera mlizokubaliana wenyewe, na nchi yetu imekubali sekta binafsi kufanya kazi na Serikali, kwa hiyo sekta binafsi kama tulivyosikia wengine inabeba shughuli za uchumi kwa asilimia 90 na ndio Serikali inawaalika sekta binafsi, lakini Ilani ya Chama cha Mapinduzi na hili lieleweke Ilani ya CCM sio kadi ya CCM, ieleweke ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi, sera na ndio ahadi tulizoahidi mwaka 2020, kwa hiyo tunaponukuu kitabu hiki tunaenda kwenye reli tuliyokubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani hii kwenye Ibara ya 9(b) pamoja na Ibara ya 14 zinaeleza wazi na kwa sababu ya msingi wa maelezo yangu, nisome maneno machache tu, inasema; "kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani, kwa kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukuwa na kustawi pamoja na kuvutia wawekezaji ili kuleta mchango stahiki katika maendeleo ya nchi yetu; lakini pili yake inasema CCM inatambua na kuthamini nafasi ya sekta binafsi hivyo itaendelea kusimamia Serikali katika kuhakikisha kuwa inalinda sekta binafsi pamoja na kuweka mazingira ya kiuchumi na kibiashara yanayo vutia wawekezaji nje na ndani ya nchi yetu."

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(3)(e) inaeleza wazi mikataba yote itakayokuwa inakutana kati ya nchi na nchi italetwa Bungeni. Ninapoenda kumpongeza Mheshimiwa Rais ni kwa mara ya kwanza ninaweza kusema tunapata mkataba wa nchi na nchi unaletwa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo hili ni jambo tunatakiwa tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya dhati ya kuweka mambo hadharani katika mambo makubwa yenye maslahi ya Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzania kwamba, maslahi mapana ya Tanzania yanalindwa kwa sababu sisi tunawawakilisha Watanzania wote ambao ni zaidi ya milioni 61. Kwa hiyo nikisema hivyo nielekee sasa kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nimeusoma huu mkataba, nimeusoma mkataba kwa maana ya makubaliano hayo, lakini sina haja ya kwenda *details* za huko nyuma, naomba nieleze tu kwamba pale nyuma..., naomba hiyo, kwa sababu nimehama kiti.

Mheshimiwa Spika, mimi sio mwanasheria nimesoma *engineering,* kwa hiyo nintaka tu niseme kwamba ile *appendix I* imejibu hofu ya watanzania. Imeeleza kwamba *areas of cooperation,* imeeleza kwa maana ya *phase one* na imeeleza *phase two* tutakazoenda kushirikiana katika jambo hili. Kwa hiyo, nataka niwaombe Watanzania kwamba wanasheria wetu wamesimamiwa na Serikali na kwa sababu na namna ambavyo tumejiandaa vizuri kwenye uwekezaji na kwa historia mbalimbali za huko nyuma ninaamini kabisa makubaliano haya yatakuwa na maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachotaka kusema hapa katika msingi ule ule wa kufungamanisha biashara za wananchi na katika biashara na wananchi wetu ni kwamba sisi tunayo Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Dar es Salaam wanakwmbia inaendeshwa chini ya kiwango kwa maana ya jiografia tuliyonayo, lakini tumekuwa tukishauri hapa Bungeni kwamba tumekuwa tunaendesha chini ya kiwango, tumekuwa na malalamiko mengi ya bandari yetu, tumekuwa hatuwapati

wateja wote ambao tunatakiwa kuwapata, lakini meli nyingi zimekuwa zikichelewa hata kushushwa maana yake ni kwamba kuna mambo hatufanyi vizuri ndio maana Serikali ilipofanya tathmini ikajiridhisha kwamba inapaswa iingie sasa utaratibu wa uwekezaji wa ubia ili kuhakikisha kwamba bandari yetu inafanya kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini leo tunavyoongea tumeweza kujenga reli yetu ya *SGR*. Reli hii ni reli ambayo tumewekeza fedha zaidi ya trilioni 17; ni fedha nyingi sana. Tusipoangalia reli hii au treni hii itakuwa kama toroli kama matoroli mengine, haitakuwa na faida yoyote katika nchi yetu kwa sababu reli inataka mzigo, reli inataka mzigo, kama hatuna mzigo mzuri kutoka Congo na maeneo mengine, reli hii haitarudisha fedha tuliyowekeza pale. Kwa hiyo, ndio maana tukasema kwamba lazima bandari yetu ambayo ni *hab* iweze kuwa na mzigo wa kutosha na mzigo wa kutosha hauwezi kuja bila kuboresha huduma za kibandari.

Mheshimiwa Spika, tukiboresha huduma za kibandari itasaidia kuchachua uchumi wa nchi yetu wamesema wengine hapa. Kwa hiyo, hoja ni kwamba tunachoangalia hapa ni matokeo yatakayotokea pale mbele yetu, lakini *SGR* hii itakwenda kuwa na tija kama tutakuwa na mzigo kama nilivyoeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee zaidi niseme mapato yetu ya nchi yetu yanategemea sana pale kwenye bandari yetu. Leo hii soko lile la pale Kariakoo linategemea kwa asilimia kubwa namna mzigo unavyoingia katika bandari yetu. Maana yake ni kwamba leo bandari isipofanya vizuri *automatic* Kariakoo haitafanya vizuri. Kwa hiyo, nilitaka niseme huu uwekezaji unapokwenda kuwekwa utaenda kuwa na tija kwenye maslahi ya Taifa letu, lakini kama haitoshi tumeambiwa mapato yataongezeka kutoka trilioni saba mpaka trilioni 26 maana yake nini? Sisi bajeti yetu ya mwaka ni trilioni 42 tukiweza kukusanya kwenye bandari peke yake trilioni 26 maana yake tutakuwa na asilimia 62 ya mapato yetu yote yataenda ku-*cover* kwenye Bajeti Kuu ya Serikali, maana yake tutaondoka kwenye utegemezi wa misaada kutoka nje kwa wale washirika wa maendeleo, maana

yake sasa hivi tunategemea asilimia 20 kutoka nje. Maana yake tukiweza kupata trilioni 26 hizi zitaenda kuondoa lile *gap* tulilokuwa nalo kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hoja yangu nilitaka niseme azimio hili tunapoenda kulipitisha, linaenda kuanzisha safari nzuri ya maendeleo ya uchumi wa Tanzania. Wale ambao wanapotosha wanaweza wakawa wana nia mbaya kwa sababu wengine hawapendi tuendelee kupiga hatua, lakini kama haitoshi Mheshimiwa Rais anataka aone nchi yake inakwenda. Tumekuwa hapa na kelele kwenye Mradi wa Mwalimu Nyerere, tumekuwa tunataka kuwa na umeme wetu wa uhakika, tunaenda kuzalisha zaidi ya *megawatts* 2115, tutaenda kujibu kiu ya Watanzania ya kupata umeme vijijini lakini mradi ule tungekuwa tumesikiliza kelele leo tumefikia asilimia 87. Mheshimiwa Rais ameusimamia vizuri, tungesikiliza watu hawa leo tungerudi tunaendelea kuwa na matatizo ya umeme nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana mradi huu twende mbele matokeo watayaona Tanzania tunayo itamani inakuja kupitia uboreshaji wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini maneno mawili ya kuzingatia maombi yangu makubwa ni kuomba sana tutakapomaliza hii *IGA* kupitisha leo niwaombe kwenye *HGAs* wataalam wetu na Serikali wasimamie mikataba ya miradi itakayoenda iweze kuwa na maslahi kwa ajili ya Watanzania, ile hofu ya watanzania ambayo ipo iondolewe kupitia mikataba midogo midogo itakayoenda kuwekezwa, lakini kama haitoshi tumeambiwa *TPA* ndio watakaoendelea kuwa msimamizi wa bandari yetu kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naamini kabisa tutasimamia vizuri mambo ya kiusalama, tutasimamia vizuri sana mambo yote yanayoelekea huko.

Mheshimiwa Spika, nimalizie…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** La mwisho ni kulinda ajira za Watanzania ili waweze kuwa na faida na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo ninaunga mkono na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono azimio hili ili Serikali iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi.

Mheshimiwa Spika, leo Waheshimiwa Wabunge wanafanya kazi ya Kikatiba, lakini vilevile nimepata meseji nyingi kutoka kwa watu wa Tarime na Mkoa wa Mara naomba sasa wasikilize maelezo ya chifu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kwamba haya ni makubaliano kati ya Tanzania na Dubai kwenye mambo ya kiuchumi na mambo ya kijamii, jambo la pili kutakuwa na nafasi ya Serikali kutengeneza mikataba midogo midogo kulingana na eneo mahsusi na masharti yake, hili ni vizuri likaeleweka sana, lakini waswahili wanasema wasiwasi ndio akili. Kitendo cha Watanzania kuwa na wasiwasi na hofu ni jambo la kawaida. Mheshimiwa Rais amesikia, Serikali imesikia, Wabunge wamesikia, chama kimesikia, wataalam wamesikiana, watazingatia yote ili katika utekelezaji wa mikataba hiyo hofu ya Watanzania ikapate matibabu ya kudumu na mwisho wa siku nchi iweze kupata manufaa ambayo tunatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile yako mambo ya msingi tu, mtu mmoja akaniambia mnauza bandari, hata ardhi watachukua. Kwenye Ibara ya 8 imezungumza namna ambavyo ardhi itatumika, imejibiwa hiyo hoja, lakini pia amezungumza

habari ya ajira, imezungumzwa kwenye Ibara ya 13, *local content*, wazawa watapata ajira, maboresho, mafundisho na huyu mwekezaji akitoka lazima aache utaalam katika nchi yetu, lakini pia wamezungumza hoja ya kwamba mikataba haivunjwi, Ibara ya 23(4) unarudi Ibara ya 20 inaeleza utaratibu utakaotumika namna ya kuondoa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi hii ni awamu ya pili Bungeni hapa sijawahi kujadili azimio lolote hapa likiwa na mkataba wa wazi kama hivi. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Leo kila Mbunge anasimama hapa anachangia akiwa na mkataba kifungu kwa kifungu tunajiridhisha haikuwahi kutokea, sasa nauliza ambao wanalalamika hapa, hivi nani amewahi kuona mkataba wa ujenzi wa *SGR* kutoka Dar es Salaam - Morogoro mmeona? Kutoka Morogoro - Dodoma, mmeona? Kwa nini hamjaona? Nani ameona mkataba ule wa Daraja la Tanzanite, Dar es Salaam, mmeona? Mmeona mkataba wa Kigongo – Busisi mmeona? Mmeona mkataba wa Bwawa la Mwalimu Nyerere? Maana yake Mheshimiwa Rais anataka uwazi katika jambo hili, ameruhusu Watanzania wajadili, watoe maoni na yupo tayari kufanya maboresho hata hapa tulipo anaangalia mijadala ya Wabunge wake, anasoma kwenye mitandao ataifanyia kazi vizuri ili Watanzania waweze kunufaika kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa mara ya kwanza kupata nafasi nzuri sana ya kujadiliana, lakini mimi nimekuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi hakuna Mtanzania mwenye akili timamu ambaye atapinga uwekezaji katika bandari zetu zote hakuna atakayepinga, cha muhimu ni kwamba kama tunawekeza tunawekeza wapi, kitu gani, tunapata nini, maslahi mapana ya nchi yetu? Hiyo ni muhimu sana na ni ukweli kwamba tumezidiwa sana na wenzetu kwenye taaluma na teknolojia. Tunataka wenye uwezo waje kuwekeza ili sisi Watanzania na wataalam wenye nafasi wahakikishe kwamba maslahi ya nchi yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye kitabu chetu cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania ukurasa wa tatu, tarehe 26 Aprili, 1964 Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Watu wa

Tanganyika waliungana na kuwa nchi moja na kwa hiyo, ni Taifa moja, lakini pia kwenye kitabu cha historia, sisi ni wajukuu wa Mwalimu Nyerere hebu tuwakumbushe watu mambo haya.

Mheshimiwa Spika, ukisoma kitabu cha Mwalimu Nyerere historia yake, wakati anazungumza anataja misingi ya Chama cha Mapinduzi, CCM ni chama cha wanyonge chenye kupigania vita ya ubepari na unyonyaji, lakini binadamu ni sawa, hakuna ubaguzi wa kidini, kikabila na kijinsia, lakini pia kudumisha na kutetea Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na Mwalimu alisema kwamba yeyote atakayetaka kuvunja Muungano hatakomea hapo, ataendaelea kuwagawanya watu kwa misingi ya Ubara na Uzanzibari; Uzanzibari na Upemba na kuendelea unaweza ukasema Ukurya na Uchaga; Umakonde na Umatengo na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Mheshimiwa Rais Mama Samia, ni Rais wa kwanza mwanamke katika nchi hii. Tulimpa heshima Baba wa Taifa akaitwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ninapendekeza huyu aitwe Mama wa Taifa kama ambavyo tulimpa Mwalimu Nyerere hiyo heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ni mama ambaye alipoingia madarakani aliahidi kwamba kazi itaendelea na kazi inaendelea; lakini Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba hakuna kitakachosimama na hakuna kilichosimama, lakini Mheshimiwa Rais huyu kwa huruma yake alimkuta mtu yuko gerezani akamtoa, akaenda akala pale Ikulu akakaa naye, lakini huyu ameruhusu mikutano ya vyama vya siasa, mama huyu pia ametoa hata ruzuku wanafanya siasa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningekubaliana na ndugu yangu yule kama angekosoa vifungu kwenye muswada huo au kwenye makubaliano hayo. Kitendo cha kusema kwamba Mheshimiwa Rais kwa sababu ni Mzanzibari anauza Bandari ya Dar es Salaam na Ndugu Profesa Makame Mnyaa Mbarawa kwa sababu ni Mpemba, ni Mzanzibari anauza Bandari ya Watanganyika, Mheshimiwa Mbowe amemkosea sana Mheshimiwa Rais, amewakosea sana Watanzania na Mheshimiwa Mbowe

anapaswa kumwomba radhi Mheshimiwa Rais kwa kumdhalilisha, lakini kuleta dalili mbaya za kuligawa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kujadili hoja za msingi za Watanzania kwa misingi ya tulipotokea. Profesa Kitila amesema amekuwa Mbunge wa Ubungo, mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Mtaa pale Kivule, Dar es Salaam, nimekuwa Mbunge wa Dar es Salaam hata Mlimani nilikuwa Rais wa Serikali ya Wanafunzi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina Watanzania wote na watu kutoka nje wangeniuliza mimi ni Mkurya kutoka Kanganiani nisingepata fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie kitendo hiki viongozi wa nchi hii lazima tukichukulie hatua. Kwenye Vyama vya Siasa, kwenye sheria yetu *Political Parties,* inataja mahsusi kwamba Chama cha Siasa lazima kioneshe Ibara mahsusi ambayo italinda Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tutaruhusu mijadala ya *design* hii ya kuanza kubagua ukimsema Rais wa nchi umemsema Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, nataka niwambie Watanzania, wanachama, viongozi, wafuasi wa Chama cha Mapinduzi hatuwezi kukaa kimya kwa mambo kama haya. Tunataka watu walete hoja za msingi, watujengee hoja, watukosoe na Rais mwenyewe amekwishasema akosolewe kwa hoja. Tena amesema wakifanya vikao vyao wakisema ya kwao, Rais ametuzuia amesemea tutoe hoja tusitukane. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nataka niwaombe Wabunge wa Chama cha Mapinduzi hii ni dalili nzuri kwamba watu hawa hawawezi kupewa nchi, wametuonesha wenyewe. Mheshimiwa Rais ajiandae 2025/2030 njia iko wazi, abebe msalaba huu, sisi tumemuamini na wanawake wanaweza na chenji inabaki. Tunataka tumpe heshima Mheshimiwa Rais ili atoe nafasi kwa wakina mama wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni mwanamama Watanzania tunakuamini, Wabunge tunakuamini, hauwezi kuleta hapa mkataba ambao ni wa hovyo. Wewe ni Wakili Msomi, Daktari wa Falsafam *PhD* ya Sheria, haiwezekani. Kwa hiyo, wasituone kwamba sisi Wabunge wa CCM hatuna akili sio kweli, tunajua sana. Hiyo kazi ambayo wanafanya kwenye mitandao, hayo mambo ambayo wanapotosha tuna uwezo mkubwa kuliko wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais katika jambo hili atuache tushughulike na watu kidogo, tulikuwa tumepoa. Tunaweza kufanya ambayo wanafanya zaidi yao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, sekunde 30 malizia.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nataka niwambie watu wa Tarime, huyu mama Mheshimiwa Rais ndiye aliyesema mgogoro wa hifadhi kule utakwisha; fidia ya Nyamongo; mama huyu ndiye amesema; kulikuwa na viongozi wa ajabu ajabu ametuondolea; mama huyu ameahidi miradi mikubwa ya nchi; mama huyu ndiye amepeleka *VETA* Nyamongo; na mama huyu ndio ameahidi zile *ambulance*. Tunapoongeza mapato ya bandati maana yake madarasa yatajengwa, vijana watapata ajira na mradi wa maji kutoka Rorya – Tarime – Nyamwaga – Nyamongo utakamilika, hizi ndizo fedha ambazo zimekuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo watu wa Tarime, watu wa Mara na Watanzania waelewe Wabunge wa CCM wanaunga mkono mambo ya msingi na hapa tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka niwambie Watanzania...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, ahsante sana.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, haiwezekani Mbunge wa Chama cha Mapinduzi uje ukae humu ndani uje upinge hoja ya Mama Samia utakuwa hujitaki. Ukitaka kutupinga toka nje, tafuta chama kingine, hii ni hoja ya Chama cha Mapinduzi, ni hoja ya Mama Samia lazima tumuunge mkono iwe jua, iwe mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono azimio kwa nguvu zote na Watanzania watuelewe, watuunge mkono, tukachape kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sasa. *(Makofi)*

Sasa nilikuwa najiuliza baada ya mchango huo na nimeona watu wote tumepiga makofi, michango kutoka kwenu si tuishie hapo? *(Makofi)*

**WABUNGE ULANI:** Ndio. *(Makofi)*

**SPIKA:** Leo mambo yalikuwa mengi kidogo, lakini naona hoja imeungwa mkono?

**WABUNGE FULANI:** Ndio. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsanteni sana. Sasa, ni kweli hoja imeungwa mkono lakini wale Wabunge ambao nilikuwa nimekwishawataja kwamba watachangia tumalize na hao halafu niipe nafasi Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia azimio hili muhimu na kipekee kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, niliomba kuchangia kwa sababu wakati wa bajeti hii ambayo tunaendelea nayo tarehe 23 Juni, 2022

nikiwa nachangia hapa niliiomba Serikali ifikirie namna ya kutafuta wabia wa uendeshaji wa bandari hii na kwa bahati nzuri niliwataja hawa hawa ambao wamekuja kubahatika kuwa wabia wetu ambao *DP World*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwajuaje *DP World* nikawataja kwenye mchango wangu mwaka jana, mwezi wa sita? Mwaka 2006 nilikuwa nafuatilia mwenendo wa mijadala ya Bunge la Marekani. Alipokuwepo Rais George W. Bush alileta muswada kwenye Bunge la Marekani waridhie *DP World* wachukue *management* ya bandari zao sita za Marekani (USA). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala ukawa mkali sana na ulienda ukagusa kila eneo na mjadala ulikuja kusimama kwa sababu waliokuwa wanaendesha bandari za Marekani walikuwa ni *P&O* wa Uingereza, lakini walinunuliwa na *DP World* ambapo *DP World* walikuwa na kila kigezo cha kuendesha, isipokuwa mjadala ule ulikwama Bungeni Marekani kwa sababu za kiusalama kwa upande wao.

Mheshimiwa Spika, hawa *DP World* ambao Serikali yetu imewachagua uwezo wao sio wa kutilia mashaka hata kidogo. Hata hivyo, tunarudi ni nini tufanye kwa upande wetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Priscus, amekwenda vizuri ila hakumalizia vizuri. Baada ya pale kilichotokea; baada ya *DP World* kukataliwa na *Congress* ya Marekani, kilichoendelea pale ilichukua kampuni nyingine ambayo sio ya Marekani na ilikuwa ni kampuni ya

Uingereza ambayo ndiyo inaendesha zile bandari sita mpaka sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naendela kusema jambo moja, kuna kipindi katika nchi yetu tulikwama kwenye mambo ya msingi kwa sababu ya baadhi ya viongozi kushindwa kufanya maamuzi. Leo hatuwezi kuacha Mheshimiwa Rais ametuongoza kwenye kufanya maamuzi ya busara, sisi tuikwamishe Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uamuzi ambao tumekwishaanza kuufanyia kazi, azimio lililopo mbele yetu ni azimio la ukombozi kwa kila namna unavyolitazama. Mikutano ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea mambo wanayotuhoji juu ya maamuzi yetu ya ndani ni kwa sababu ya uwezo wetu wa kibajeti, ni kwa sababu tunaendelea kuwa tegemezi.

Mheshimiwa Spika, huu mpango kwa kila *angle* unayoiangalia unakwenda kutukwamua kwenye bajeti tegemezi. Kama tunakwenda kuitoa bandari kwenye mchango wa trilioni saba kwenda kwenye mchango wa trilioni 26 mpaka 30 kwenye pato letu, tunakwenda kupata uhuru wa kiuchumi na tunakwenda kuyasimamia mambo yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima kwa pamoja tumuunge mkono Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha azimio hili linapita. Tunapokwenda kumuunga mkono Mheshimiwa Rais ni lazima pia tuwasikilize hao wanaotukosoa, ni wananchi wetu, wana hoja, lakini ningeomba sana Kitengo cha Mawasiliano cha Serikali kiwe kimetangulia mbele, kwa sababu kwenye hoja hizo, kuna hoja za kuzifanyia kazi, lakini kuna hoja zinahitaji ufafanuzi tu. Kwa nini tuache upotofu utangulie, baadae tuje tufanye kazi ya kusafisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sisi tuwatangulie katika kutoa ufafanuzi kwenye zile hoja ambazo zimpotoshwa. Hata hivyo, kwenye hoja ambazo ni za msingi zipo ambazo tumezichukua tutazifanyia kazi kwenye hatua zinazofuata, kwenye *HGA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukirudi kwenye hadithi za Biblia katika busara za Mzee Suleiman, tunakumbuka hoja za wanawake wawili waliokuwa wanagombania mtoto. Busara za Mfalme Suleiman ilikuja pale ili kujua ni yupi mzazi kweli wa yule mtoto aliposema mtoto huyu akatwe nusu wagawanywe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaopinga hili azimio hawaongelei hizi ajira 72,000 watazipata wapi kama tusipopitia hili suala? Hawaongelei haya mapato tutakayoenda kuyapata tutayapata wapi kwa ajili ya Watanzania na maendeleo ya yetu? Hawaongelei kabisa kukua kwa uchumi wetu kutokana na haya. Maana yake wanataka kulizuia na hawana mbadala wa kututoa hapa tulipo kutupeleka mbele. Tukiangalia kiuhalisia namna halisi ni sisi ambao tunaona ni namna gani tunakwenda kusimamia hili azimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ushauri wa Kamati katika kila *angle* wamepita mle mle ambapo wananchi ndipo wanapolilia. Ni kwa nini watu wengine waendelee kupotosha wakati uhalisia uko mbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwashawishi Wabunge wenzangu tuliunge mkono kama ambavyo tumkwishaonesha ili tuweze kupata manufaa haya yanayokuja na hili na mimi siku zote nilikuwa ninasema tunajenga reli ya kisasa hivi reli hiyo itabeba abiria tu? Hiyo hela ambayo tumewekeza au huo mkopo utarudi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuja hawa *DP World,* wakaweza kuongeza mizigo kwenye bandari yetu kama inavyoonekana hapa kutoka tani milioni 18 mpaka tani milioni 48 maana yake bandari zetu, reli yetu na bandari za kwenye maziwa zitafanya kazi na tutarudisha mikopo na hela tutapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ahsante sana nimesema nigusie maeneo hayo na ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata ushauri hapa kwamba kuna Wabunge ambao waliomba kuchangia azimio hili lakini wao hawajawahi kuchangia kabisa Bungeni. Kwa hiyo, na mimi ni mtu wa haki, kwa hiyo sipendi mtu aonewe. Kama hawajawahi kuzungumza kabisa basi tutampa nafasi ili awe amechangia angalau kwenye hoja hii.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Aida Khenani, sasa changamoto ni kwamba hapa huwa nakuwa na orodha ya Wabunge wale waliochangia ila leo sina. Kwa hiyo, nitaangalia kwenye huu ushauri niliopewa. Kuna Wabunge ambao nimetajiwa hapa ambao hawajapata nafasi za kuchangia. Mheshimiwa Dkt. Leornard Chamuriho, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa ndio nimeambiwa hawajawahi kuchangia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama kuna ambae amechangia katyi ya hawa nipeni taarifa lakini tutakaomaliza nao ni hawa ambao hawajawahi kuchangia.

Mheshimiwa Aida Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Leornard Chamuriho, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie azimio hili ambalo liko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema hakuna mtu anapinga uwekezaji kwenye Taifa letu. Hakuna mtu ambaye haoni umuhimu wa kuwekeza leo kwenye Taifa letu hasa kwenye bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa niwakumbushe Wabunge wenzangu, kipindi tuna Kambi Rasmi ya Upinzani hapa Bungeni ushauri wetu miaka yote tulisema bandari yetu inaendeshwa kwa hasara na tukashauri kwamba ni vizuri tukaona utaratibu mwingine wa kuruhusu sekta binafsi. Leo tunapotaka kushauri hatusemi shida ni uwekezaji, tunachotaka kujua masharti ya kwenye huo uwekezaji yana faida gani kwa Taifa letu, yana faida gani kwa Watanzania, na yana athari zipi kwa Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sio mwanasheria kama wewe na vifungu vilivyopo inawezekana ni suala la kutoelewa hivyo hivyo huko nje. Ilikuwa ni suala la elimu lifanyike kwanza kabla ya kuleta hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitazama malalamiko ya Watanzania ndio waliotufanya sisi tuko hapa leo. Bandari tunayoizungumzia ni bandari yao. Tunaofanya maamuzi leo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, samahani kidogo. Waheshimiwa Wabunge naongeza nusu saa ili tuweze kukamilisha kazi hii. *(Makofi)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, jambo lolote lenye nia njema linakwenda na dhamira njema. Inawezekana wengi walioko huko ambao wanalalamika ni kwa sababu aidha kama tunavyosema hapa mtu akikiona Ibara ya 23(4) kwa hali ya kawaida Ibara hii ya 23 ya Mkataba wetu na hapa ndani tumeona Wabunge wanavyochangia wapo wanaosema si mkataba bado wanazungumzia makubaliano. Huko nje unaweza ukaona pia na wao wanaelewa nini kuhusu jambo hili linalozungumzwa leo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nia ni njema ya hili jambo, yale maeneo ambayo tunasema yanahitaji kutolewa ufafanuzi, yatolewe ufafanuzi kwa nia hiyo hiyo njema.

Mheshimiwa Spika, ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida, kwa nia hiyo hiyo njema hicho kifungu ulichokitaja kifungu kidogo cha (4) ulichokitaja, huko nje wanakisema kana kwamba ni Tanzania pakee ndio inayobanwa na ndio haiwezi kutoka, lakini kifungu hiki hapa kinasema; "*The State Parties is shall...*" maana yake Dubai pamoja na Tanzania kila mmojawapo haruhusiwi, ukikisoma chenyewe tu peke yake, lakini wao wanakiweka kana kwamba ni Tanzania peke yake ndiyo haiwezekani. Kwa hiyo, nadhani na wewe unacho hapo, kinazungumzia pande zote mbili.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, eneo linalowekezwa ni Tanzania na wanaoumia ni Watanzania kwa sababu wanajua athari zitakzotokea sio kwao, yaani endapo kama itatokea wao labda wamechukua muda mrefu, kwa sababu ni suala la uelewa kama ninavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, unaposema hawatoruhusiwa kujitoa iwe Dubai au Tanzania, wakati huo jambo la kwanza ambalo Watanzania walitamani kuliona ni kwamba wanakuja kuwekeza wapi na kwa muda gani? Hayo mambo kama yangetolewa ufafanuzi mapema yasingetufikisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nia hiyo hiyo njema ninaishauri Serikali, wananchi wanapotoa mawazo yao wachukuliwe kwa nafasi yao kama Watanzania wajibiwe kikamilifu ili waweze kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hiyo hiyo kwamba kwa muda ambao mimi nimekuwepo kwenye Kamati hii iliyoundwa…

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Naisubiri

**SPIKA:** Inatokea wapi? Mheshimiwa Aida Khenani, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kumpa taarifa dada yangu Mheshimiwa Khenani ambaye ninamheshimu sana. Bunge hili halipingani na Watanzania wanachokisema, Bunge hili linasema tunamuonya muhuni mmoja ambaye yeye mwenyewe anamjua ambaye wanawake wa hapa, akina mama wametengenezwa kwa miaka 30 kwa sababu ya maslahi yake binafsi leo kila siku wako mahakamani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Bunge hili linamzungumzia huyo, lakini mawazo ya Watanzania Bunge hili limeyapokea na wakati wote umewasikia Wabunge hawa, lakini huyu muhuni mmoja ni lazima tushughulike naye. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, kulingana na uzito wa jambo lililopo mbele yetu naomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kuwapongeza Watanzania waliotoa maoni yao na wakasema hofu zao na ndio hofu ambayo mimi Mbunge ninayezungumza hapa ni kubwa sana kwangu.

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia hii Ibara ya 23 kama kweli kuna *loophole* ambayo sisi tunaweza tukafanya *negotiation* kulikuwa na haja gani ya msisitizo huu kwenye hii Ibara ya 23(4)? Hiyo ndiyo hofu ya Watanzania wengi, msisitizo ule ulikuwa ni wa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tuna haki ya kutoa maoni yetu kwa mujibu wa Katiba yetu ambayo ndio msingi, leo tunasema kutakuwa mikataba mingine, sawa tunakubali hiyo mikataba mingine ambayo itaendelea labda mkataba wa pili au wa tatu, lakini msingi wake ndio huu tunaoujadili leo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilichokuwa nataka kufahamu, kama ndio kuna eneo ambalo tunaweza tukaruhusu mazungumzo yaani tumeona kwenye mkataba hawa *DP World* kwamba kuna shida fulani ambayo sisi tunaona labda upande wa makusanyo au eneo ambalo tumewapa. kama tunaweza kukutana nao tena kuzungumza, Watanzania wanataka kujua ni vizuri sasa Serikali iseme eneo hili pamoja na kuandikwa hii ibara, ibara hii inatupa nafasi nyingine. Ni Watanzania wangapi wanajua kuhusu hilo jambo?

**SPIKA:** Sawa na ahsante sana, eneo la makusanyo ni mikataba ijayo. Kwa hiyo, sisi hatujui.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ndilo hilo ninalizungumzia.

**SPIKA:** Kulikuwa kuna taarifa nyingine kutoka kule nyuma, Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nimpe tu taarifa mzungumzaji rafiki yangu Mheshimiwa Aida kwamba kifungu hiki cha 23 ukikisoma vizuri usiposoma cha (4) tu ukaanza kusoma kile cha (1) mpaka cha (4) hakina shida yoyote, na kifungu hiki kinachosomeka hapa ndivyo kinavyosomeka hivyo hivyo kwenye makubaliano ya aina hii ya Mkataba wa Bomba la Mafuta na ni kifungu cha 24(4) hivyo hivyo, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana, Mheshimiwa Aida Khenani unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa yake, tunawezaje kusaini kitu ambacho hatukijui? Ndio hofu yangu mimi hiyo, na Watanzania wengine waondolewe hii hofu.

Mheshimiwa Spika, wakati tuna...

**SPIKA:** Kwa sababu wewe upo hapa ndani, mimi nataka kuindoa hiyo hofu yako, wewe una hofu gani?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, na muda wangu bado upo?

**SPIKA:** Unalindwa, ukizungumza na mimi unalindwa ambao haulindwi ni ule kule. Hofu yako mimi nataka niiondoe wewe una hofu gani Mheshimiwa Aida?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, hofu kubwa iliyopo kwanza kuna mikataba ya hovyo mingi kama Taifa ambayo tumewahi kuingia huko nyuma, mingi sana. Kwa hiyo unapokuja mkataba mwingine mkubwa kama huu, lazima hofu iwepo, lakini Watanzania leo tunapotaka kupitisha hili azimio wanayo historia na kauli ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano aliyoizungumza, leo tulikuwa na haki ya kuwaambia Watanzania alichokizungumza Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kina utofauti gani na hiki ambacho leo tunakwenda kukiingia? Lazima watu wajue, wana kitu gani leo tunapokwenda kupitisha kitu kama hiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida, mimi nakusiliza ili hofu ile ya Watanzania natamani kwa sababu mwishoni ile Kanuni zetu ya 111 inatupa nafasi kama Bunge kupitisha mkataba huu, kupitisha baadhi ya vifungu au kuukataa kabisa. Sisi kama Bunge tunaruhusiwa vyote vitatu. Ninavyotaka mimi nielewe hofu yako ili na Watanzania tukitoka hapa tuwe tumeelewana. Ukiiweka kwa ujumla mimi nina nafasi ya kufafanua hofu yako, ya kwao naweza nisipate, nafasi lakini na wewe ukiweka jumla basi nitakuacha na wewe utatoka hapa ndani ukiwa na hofu wakati kura utapiga wewe hapa ndani. Karibu Mheshimiwa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba kura yangu ni ya hapana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haya mazingira tunapoyaweka hapa hawa ambao wanatamani kuelewa ni Watanzania, maamuzi yanayokwenda kufanyika yanafanyika kwa niaba ya Watanzania na ndio maana nasema hili jambo lilihitaji mjadala mpana sana kwa maslahi ya Taifa, mpana sana ili watu ambao wanaweza kutoa ushauri wao, watu ambao wanatakiwa kuondolewa hofu zao waondolewe.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hata kwenye wadau tukiwa tu kwenye Kamati, namna ambavyo hili tangazo lilitolewa la hawa wadau, wadau tuliowapata ni wachache sana kiasi kwamba tulipaswa tupate mawazo ya watu wengi ili kama Bunge tujue tunasimama wapi. Ni kweli sisi hatuhusiki na kusaini mkataba, lakini kama Bunge ni wajibu wetu kuisimamia Serikali na kuikosoa Serikali ndio maana yale maeneo ambayo tunaona kwetu bado yana hofu, ambayo bado yana changamoto lazima tuyaseme.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, si utaratibu wa mimi kusimama, lakini nilitaka nimsaidie tu Mheshimiwa Aida.

Mheshimiwa Spika, hiyo hofu aliyokuwa kwenye *article 23(4)* alitakiwa akisome mpaka mwisho. Anakisoma maeneo yale ambayo anayaona ni magumu, lakini akija mpaka mwisho kinaeleza vizuri tu; *Notwithstanding the foregoing, any dispute between State Parties in respect of such circumstances shall be dealt with accordance with the requirements of Article 20 of this agreement.*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kifungu hiki kinasomwa pamoja na *article 20* ambacho ni *dispute* ya *settlement,* kwa hiyo hofu hiyo dada yangu itoe. Tatizo lolote litamalizwa na *article 20.*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na taarifa zinazoendelea na kwa sababu kiongozi wangu pia namheshimu sana nimepokea taarifa yako, lakini nataka kusema kama umesema sheria zitakazotumika kusuluhisha migogoro ni za

Tanzania kwa nini tunakwenda kusuluhisha *South Africa?* Hayo ndio maeneo ambayo Watanzania wa kawaida wanataka kujua mambo kama hayo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, jamani *too much*.

**MBUNGE FULANI:** Mnaogopa nini?

**SPIKA:** Taarifa zimeshaisha tatu, kwa hiyo, sasa hivi mimi ndio naruhusiwa kuongea naye.

Mheshimiwa Aida wacha nikufafanulie kwenye hilo eneo ni hivi, huu mkataba kwa sababu ni kati ya nchi mbili; nchi mbili huwezi kuchagua sheria za nchi mojawapo, unachagua wewe nchi ipi duniani huko ama sheria zipi huko duniani mtazitumia, kwa hiyo hofu hiyo nikuondoe kwa namna hiyo kwa sababu mkataba huu ndio unaozungumzia mtakwenda Afrika ya Kusini, ile mikataba mingine ile humu nako kumeshatajwa kwamba tutatumia sheria zetu, wala hatutoki popote. Hata kama tutaenda huko tutatumia zetu.

Nimeona nikufafanulie hapo si umesema una hofu kwa hiyo na mimi nataka nikutoe kabisa hofu yako hata kama utapiga kura ya hapana ni haki yako, lakini hofu iwe imekuondoka.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na niendelee kusema kwamba kwa sababu ni haki yetu kusema, kushauri, maamuzi najua tutafanya kwa wingi mtaamua, lakini lazima tutaelekeza kwenye yale maeneo ambayo tunaona kwetu yana changamoto. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mwenyekiti wangu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kutoa maoni kama Mtanzania, kwa kuonesha kwamba mambo haya lazima mbele tuangalie kuna mambo yanaweza kutokea, ni haki yake kama Mtanzania, kama kiongozi wa chama na sisi tunasema tusipotoshwe kama inavyosema

hukio nje wanapotosha. Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe hakuzungumza juu ya mgawanyo wa Tanganyika na Zanzibar, tusipotoshe mambo haya.

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia.

**MHE. AIDA J. KHENAN:** Mheshimiwa Spika, watu wana *clip* walisikia, wasipotoshe kwa makusudi yule ni kiongozi wa chama anastahili heshima yake kama mnavyoheshimu viongozi wengine na siyo lugha zinazotumika humu ndani.

**SPIKA:** Ngoja jamani mimi namlinda mchangiaji, Mheshimiwa Aida hawa wamepotosha, wewe unaujua ukweli hebu sema alichosema ili na wewe iingie kwenye *record* kwamba ndicho alichosema.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana alichozungumzia kwamba kwenye maamuzi haya, kwenye mkataba huu ni vizuri kuchukua tahadhari, ni vizuri kuchukua tahadhari na tahadhari ni jambo la kawaida kabla hujafanya maamuzi, lazima uchukue tahadhari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida ngoja, Waheshimiwa Wabunge mimi namlinda.

Mheshimiwa Aida mchango uliokuwa unasema watu wamepotosha Wabunge wengine ni kuhusu hoja ya Mheshimiwa Rais kutoka Zanzibar na Mheshimiwa Waziri kutoka Zanzibar, pale wewe umemsikia nini akisema Mheshimiwa Mbowe? Rekebisha hiyo kwa sababu umesema wapepotosha, sasa mimi nataka kuelewa kutoka kwako wewe ulivyomsikia kasemaje hoja hiyo ili Taarifa zetu za Bunge zikae sawa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, alisema inaweza kuleta hisia na *clip* hapa ninayo.

**SPIKA:** Basi wako sahihi, amesema yeye...

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, hapana.

**SPIKA:** Inaweza kuleta hisia, ni kama wewe ulivyosema hofu zao kwani tumebishia za wananchi.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Aah! Mheshimiwa Aida umesema amesema zinaweza kuleta hisia maana yake amesema inaweza kuleta hisia, hisia zinaweza kuwa zake au za watu wengine. Kwa hiyo, yeye ndio kazisema, kwa hiyo wako sahihi hawajapotosha alichokisema.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, jambo hili likienda hivyo, siyo sawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida ujue unaposisitiza nitakwambia ufungue kwenye simu tumsikie alichosema.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kufungua.

**SPIKA:** Fungua. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati anaendelea kutafuta... kaa tu Mheshimiwa tafuta taratibu wala hatuna haraka.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi tu ipo tu hapa.

**SPIKA:** Eeh, wakati tunasubiri ili tusipoteze muda nimeletewa wale waliochangia kama nilivyokuwa nimesema nataka kutenda haki, Mheshimiwa Chamuriho amechangia mara moja, Mheshimiwa Mnyeti mara tatu, Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa mara mbili, Mheshimiwa Kigwangalla hajachangia kabisa.

Kwa hiyo, katika orodha hii tunaweza kuchangiwa na Mheshimiwa Chamuriho na Mheshimiwa Kigwangwalla Mheshimiwa Dkt. Leonard Chamuriho au umeipata?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ipo tayari.

**SPIKA:** Haya tuwekee.

Shusha hiyo *microphone* halafu weka. Weka sehemu hapo ya *microphone* kama mimi ninavyozungumza tutaisikia, siyo hapo unapoweka *microphone* unakozungumzia wewe huko.

*(Hapa sauti iliyorekodiwa ya Mhe. Freeman Aikael Mbowe ilisikilizwa Bungeni)*

*"Tunawaletea uchambuzi wa awali wa mkataba wa ushirikiano kwa ajili ya uendeshaji na uboreshaji wa bandari Tanzania kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dubai"*

**SPIKA:** Sasa tupeleke kwenye hoja yake kuhusu Rais kutoka Zanzibar, usituwekee yote hatuwezi kuwa na huo muda wewe tutafutie kwenye hoja yako uliyosema Wabunge wamepotosha kwenye hoja yake ya kuhusu Rais kutoka Zanzibar na Waziri kutoka Zanzibar, itafute tu taratibu mimi nimekupa muda. Itafute tu taratibu.

Mheshimiwa Dkt. Leonard Chamuriho.

**MHE. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hoja hii muhimu ambayo imewekwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na *preamble* ya haya makubaliano tukiangalia ile ya kwanza kabisa chimbuko ni ziara ya Mheshimiwa Rais alipokwenda kule Dubai. Kwa hiyo, kwa ziara hilo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kututafutia rasilimali za kuweza kuendeleza miundombinu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika *preamble* hiyo hiyo kifungu cha pili kinaongelea chimbuko lingine ambalo ni maombi ya *TPA* na *DP World*. Ningependa kuwapongeza Wizara pamoja na *TPA* kwa kuweza kufahamu udhaifu uliokuwepo *TPA* na kutafutia changamoto cha kuweza kutatua.

Mheshimiwa Spika, kwa wengi wanaweza kuwa hawafahamu kwa nini hawa waliweza kumtafuta mwekezaji mahiri. Nitatoa mifano mitatu ambayo itaonesha ni kwa nini unahitaji mtu mahiri ili uweze ku-*dea*l na hivi vitu vikubwa vikubwa.

Mheshimiwa Spika, mfano wa kwanza tulitaka kununua *spare* za *engine* za *TAZARA* zinaitwa *tracks and motors,* tulipotoa ile *order* tuliambiwa tunaweza tukaipata baada ya miaka mitatu na kosa letu lilikuwa ni moja tu kwamba sisi tulikuwa niwaagizaji wadogo, hatuwezi kuweza kuitoa *design team* ya wale *manufacturer* wahame watutengenezee sisi kitu kidogo, kwa hiyo tutakwenda baada ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ambao nitautoa kwa nini tunahitaji wawekezaji mahiri, ni pale tulipoagiza vichwa vya treni. Tulipoagiza vichwa vya treni tulipata changamoto moja kubwa, klila ukiagiza unaambiwa kwamba *order* yako ni ndogo mno kuweza kuhamisha *design team* yetu ikafanya kazi yako ili upate hiyo *order* yako. Kwa hiyo, unajikuta unawekwa kwenye foleni ya miaka mitatu au minne mbele na ikitokea changamoto yoyote unasukumwa mbele zadi? Ni kwa sababu ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, mfano wa tatu ambao ningependa kuutoa utahusu bandari wenyewe. Katika hayo maendelezo ya bandari yaliyofanywa sasa hivi tuliagiza hizo *sea to shore gantry* ambazo ni *crane* ambazo zinatumika pale. Tulipata muda ambao ni wa miaka mitatu mbele, kosa letu moja tu ninyi ni wadogo mno kuweza kutoa hiyo *order* mkapata moja kwa moja. Kwa hiyo, inabidi uwe una mwekezaji mahiri ambaye akiagiza *order* yake ni *order* kubwa ambayo itasababisha uweze kupata hiyo *order*. *(Makofi)*

Sasa huyu mwekezaji mahiri kama tulivyoambiwa amewekeza kwenye bandari nyingi sana. Kwa hiyo, hata kama akitoa *order* yake ni kubwa, kwa hiyo uwekezaji wake unakwenda moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika uendeshaji huu vifaa hivi huharibika, vinapoharibika tunapambana na changamoto hiyo

hiyo kwamba unapoagiza vipuri na wewe ni mtu mdogo unaingia kwenye foleni ndefu sana, imeharibika *crane* yako moja unataka upate hicho kipuri unaambiwa kipuri chako utakipata baada ya miaka mitatu. Sasa huwezi kuwa unasubiri hapo na wenzako wanapata vipuri kwa sifa moja tu, kwamba wao *order* zao ni kubwa kwani ni wakubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka kuchukua fursa hii kuwapongeza Wizara kupitia *TPA* kwamba kwa kutafuta mwekezaji mahiri ili aweze kutuboreshea bandari zetu ili tuweze kupata uendelezaji wa haraka.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa tatu utaenda kwa wale waliojadili huu mkataba. Kama ilivyojieleza katika *preamble* pale, sisi tulikwenda kuomba kusaidiwa. Sasa unapoenda kuomba katika majadiliano huwa uko kwenye *weaker position,* lakini unaona kwamba katika majadiliano haya hawa waliojadiliana wameweza kabisa kutuletea mfumo mzuri kabisa ambao unaweza kutuondolea changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, mfumo waliouweka ambao unaanzia *IGA* unatoka kwenye *IGA* unakuja kwenye *Host Government Agreement* ambayo ni kwamba mnajadiliana Serikali itampa nini mwekezaji, lakini wa tatu tutakwenda kwenye *land lease* ambayo utampangisha mwekezaji ili apate sehemu ya kufanyia biashara na mwisho ni hiyo *concession agreement,* ni mfumo ambao ni mzuri ambao unaweka hatua mbalimbali ambazo zinaweka. Kwa hiyo, ningependa kuchukua hatua hiyo kuwapongeza hao ambao waliweza kufanya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile pongezi ambazo ninawapa hao ni kuweza kuweka mikataba ijadiliwe wakati ule ambapo inapotakiwa. Hili litawezesha hawa watakaojadili hiyo mikataba inayokuja kuweza kuangalia changamoto za nyuma ambazo tulikuwa nazo na kuweza kuzichukulia katika mukhtadha wakati uliopo. huu nao ni mtindo mzuri sana ambao inabidi tuwapongeze katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukiangalia kifungu cha nane ambacho kinaongelea ardhi, maana yake ni kwamba wameweka kwamba kwa sababu kitajadiliwa kwa sheria za kwetu kitajadiliwa kwa mukhtadha wa sheria zilizopo. Ukiangalia kwenye kifungu cha tisa, vivutio; vivutio wamesema vitawekwa kulingana na sheria za kwetu, kwa hiyo kwa sababu wameviweka vitajadiliwa kule mbele, jukumu letu ni kuangalia hizi hofu za Watanzania na kuziingiza katika ile mikataba kama vizuizi hatarishi ambavyo tunavilania. Kwa hiyo, hizi hoja ambazo zinatolewa na hofu za wananchi nashauri tu kwamba Serikali izichukue ili ziweze kuingia katika majadiliano hayo tuweze kupata kilicho bora ambacho Watanzania wote wanakitaka.

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kuwapongeza kwa kuweza kulinda ajira za Watanzania. Katika miradi hii mikubwa huwa kuna mvutano mkubwa sana katika kulinda hizi ajira. Ukichukulia mfano wa mkataba wa *SGR* kwa wafanyakazi wa kawaida asilimia 80 wanatakiwa wawe Watanzania na asilimia 20 ndio wawe wageni. Hiyo ni *ratio* nzuri tu na kwa wale kwa upande wa *management* asilimia 20 wanakuwa Watanzania, asilimia 80 watakuwa wa kwao.

Kwa hiyo, hii ni mifano ambayo imeangaliwa huko nyuma na sasa hivi inaweza ikaangaliwa vizuri zaidi katika mikataba inayokuja. Kwa hiyo, tuwapongeze hawa kwa kutuwezesha kuruhusu tujadili mikataba hii mbele ili tuangalie huko nyuma tulivyofanya na tuweze kuboresha kwa kadri ambavyo tutaona inafaa.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa nimetenda haki bila kuongelea machache ya hofu. Napenda kujadili hofu ambayo imejitokeza katika majadilano huko nje.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana.

**MHE. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mheshimiwa Nape Nnauye ajiandae.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nitoe maoni yangu kwenye hoja hii muhimu sana iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha mchakato huu wa mageuzi makubwa ya kiutendaji kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam na bandari nyingine hapa nchini. Haya ni mambo ambayo yalikuwa yamekwama kwa muda mrefu yalihitaji mtu mwenye uthubutu, mtu ambaye atakuwa tayari kutupiwa mawe ilimradi mambo makubwa kama haya yaweze kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimpe moyo Mheshimiwa Rais wetu na Mheshimiwa Waziri na timu nzima iliyolifikisha jambo hili hapa tulipofika kwamba wasikatishwe tamaa na watu ambao wanakusudia kutukwamisha, kwa sababu miongoni mwa wanao tukwamisha wengine siyo raia wa nchi yetu. Nilisikia *clip* moja inazunguka mtu ambaye alikuwa anajaribu kutaka kutukwamisha siyo hata Mtanzania, lakini pia wengine wanaotaka kutukwamisha ni wanasiasa kutoka upande wa upinzani, badala ya kuchangia hoja ambayo ni mkataba wanaleta hoja nyingine za ajabu ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme hapa kwamba Mheshimiwa Rais Samia hawezi kuwa mtu wa kwanza kupigwa mawe pale ambapo alithubutu kufanya jambo kubwa. Mambo haya yalianza toka Awamu ya Kwanza walisemwa viongozi wakuu. Mzee Mwinyi alisemwa miaka ile ya 1990 alipokuwa anaamua kuikwamua nchi kutoka kwenye mfumo wa *centrally planned economy* uliokuwepo wakati huo na kutuleta kwenye mfumo wa soko huria,

aliambiwa amelikanyaga na kulichana Azimio la Arusha, aliziba masikio akasonga mbele. *(Makofi)*

Mzee Mkapa alipokuwa anaamua kutekeleza yale ambayo yaliamuliwa na Rais aliyemtangulia ambaye ni mzee wetu Mzee Mwinyi naye aliambiwa anauza mashirika ya umma, kelele zilikuwa nyingi lakini aliziba masikio akasonga mbele hakurudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Mzee Magufuli hapa juzi alipokuwa anataka kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere alipigwa vita sana, walikuwepo wenzetu upande wa upinzani, lakini naye aliamua kuziba masikio na akasonga mbele. Leo hii karibu tuanze kupata umeme megawati zaidi ya 2,150. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mtu yeyote yule siku yoyote ile atakayoamua kufanya jambo zuri lenye manufaa atarajie atapingwa, atarajie atapigwa vita, hakuna watu ambao watakuwa tayari kumuunga mkono moja kwa moja kwa sababu nyingi mbalimbali mojawapo ni woga wa mabadiliko na nyingine ni woga wa kitu ambacho hawakijui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kupingwa, kukosolewa sio mambo ya ajabu ni mambo ya kawaida, kwa hiyo napenda kumtia moyo Mheshimiwa Rais, lakini pia Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi ninapenda nijikite moja kwa moja kwenye kile kifungu cha 23 ili kujaribu kujibu hofu mbalimbali ambazo ziliIetwa, lakini kabla ya kifungu cha 22 labda nianzie kile cha nane ambacho kinahusu haki za ardhi *(land rights)*. Kifungu hiki hakiendi kummilikisha ardhi huyu mwekezaji anayekuja, kinaenda kumpa haki za kutumia ardhi na sisi katika sheria zetu za ardhi hapa nchini, haturuhusiwi hata sisi wenyewe tuliozaliwa hapa haturuhusiwi kumiliki ardhi, tunapewa tu haki ya kutumia ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata huyu mwekezaji anapokuja atapewa haki ya kutumia ardhi na haki atakayopewa

yeye itapitia *TIC* kwa sababu sio mzawa. Kwa hiyo, atapata *derivative rights,* atapewa masharti ya namna ya kutumia ardhi atakayoitaka na ndio ataishia pale, lakini sio kumilikishwa ardhi.

Kwa hiyo, wanaowadanganya Watanzania huko nje kwamba ardhi yetu inauzwa na anapewa mwarabu wa Dubai waache tabia hiyo kwa sababu ni upotoshaji ambao haujengi Taifa, ila unaenda kutukwamisha kufanya mambo yetu ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo napenda kulisema linahusu upotoshaji ambao umewekwa kwenye eneo la kipindi cha mkataba na *termination*. Walikuwa wanasema kwamba tunauza kipande cha ardhi ya Tanzania kwa miaka 100, kwanza hakuna hicho kitu kwenye mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia mkataba huu unaweka ukoma kwenye hicho hicho kifungu cha 23; wengi wanatia mashaka kwenye kile kifungu kidogo cha (4) ambacho bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Spika amekifafanua vizuri sintokirudia, lakini mimi napenda kutia msisitizo kwenye kile kifungu cha kwanza kwamba kifungu 23(1) inasema kwamba mkataba huu utaendelea kufanya kazi mpaka pale mambo kadhaa yatakapojitokeza. Moja ni shughuli za mradi zitakapoisha, lakini la pili ni mikataba ile midogo midogo ya utekelezaji itakapomaliza muda wake. *(Makofi)*

Sasa kama ile itamaliza muda wake na shughuli za mradi zitakuwa zimeisha *automatically* huu mkataba mama utakuwa hauna kazi, utakuwa umekufa, hautokuwepo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kusema kwamba mkataba huu hauna mkomo sio sahihi, kwa sababu sisi tuwe makini tu kwenye ile mikataba midogo midogo ambayo Serikali wataenda kusaini huko mbele kwa maana ya *Hosting Government Agreement* ama *Concession Agreement* na hapo mimi na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba Serikali watakapoenda kujadili na hatimaye kupatana juu ya *HGAs* pamoja na *Concession Agreements* wawe makini kwenye kipindi kwenye mkataba. Wasizidishe miaka 30, naona imekuwa kama *consensus* hapa Wabunge wengi wamejadili hivyo na mimi napenda kuungana na wanaopendekeza miaka kati ya 25 ama 30. Kwa maana ya kwamba ikipita hicho kipindi cha miaka hiyo 30 maana yake kama hatujasaini mkataba mwingine na wala hakuna mkataba mwingine ambao uko hai maana yake hii *IGA* inakuwa imekuwa imekufa *automatically*. Hata kama itakuwepo haijafutwa lakini itakuwa imekufa kwa sababu ya hichi kifungu cha 23(1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kupendekeza kwamba watakapoenda kusaini ile mikataba ya utekelezaji hizo *Hosting Government Agreement* pamoja na *Concession Agreement*, wawe makini wasije wakasaini mikataba ya kumpangisha kutumia ardhi, wasaini mikataba zaidi zaidi inayojielekeza kwenye kumpa haki ya usimamizi wa miradi husika, kwa maana ya kwamba sisi tubaki na haki za kumiliki ili mitambo, kumiliki hizo *facilities* ambazo watakuwa wamejenga, lakini tumpe tu mikataba ya *operations,* usimamizi, marekebisho kwa miaka hiyo atakayotaka na hapo tutakuwa tumelinda sana maslahi ya Tanzania kwenye mikataba hiyo, kuliko tukisema tunaenda kumpa aidha mikataba ya upangishaji kama *tenant agreements* ama *CMS agreement*.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ninalopenda kupendeza wakawenalo makini kwenye Bandari ya Dar es Salaam ukiangalia miradi iliyopo kwenye *appendix I, phase one* unaona pale kuna shughuli ambazo Serikali yetu imeshakopa pesa nyingi na zimekwishafanyika sema kuna mapungufu ya hapa na pale ambayo yanaenda kutekelezwa na mkataba huu. Sasa pale maana yake kuna uwekezaji wa Serikali. Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kwamba iundwe kampuni ya pamoja kati ya *DP World* na *TPA* ambayo Serikali itakuwa ina hisa zake na mwisho wa siku kabla ya kuunda hiyo kampuni utakuwa tumeshafanya *valuation,* tutakuwa tumefanya uthamini wa mali iliyoko pale. Kwa hiyo tutakapoenda kufunga naye mkataba tutapata *share* za kutosha kwa hiyo *DP World* ataendesha ndio, lakini na sisi tutakuwa wabia

kwenye mkataba wa kuendesha Bandari ya Dar es Salaam kuliko kusema tunamwachia moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hiyo naweza nikapendekeza pia hio kampuni mpya itakayoundwa baina ya *DP World* na *TPA* iweze kuwa *listed* kwenye Soko la Hisa, ili katika ile *local content* Watanzania wengi zaidi waweze kununua hisa na waweze kupata matunda yanayotokana nan uwekezaji wa kimkakati katika Taifa letu. *(Makofi)*

*(Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagongwa, shukrani sana.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Nape Nnauye ajiandae.

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa fursa niweze kuchangia kwenye hoja iliyowekwa mezani na Mheshimiwa Profesa Mbarawa kuhusu azimio hili.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametufikisha hapa tulipo kuanzia pale safari yetu ilipoanzia kwenye jambo hili. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake njema anayoifanya kwenye eneo la uwekezaji. Mheshimiwa Rais yeye ameamua kulifungua Taifa letu na tumeona uwekezaji tunaoupokea na wawekezaji tunaowapokea ndani ya Taifa letu sasa ni zaidi ya asilimia 100 ya miaka ya nyuma ambayo ilikuwepo. Kwa hiyo, kwa kweli Mheshimiwa Rais tunampongeza sana, hata jambo hili lilikoanzia ni kwenye maonesho ya *Dubai Expo 2020* ambayo yalifanyika mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Mheshimiwa Rais alipoamua kwenda kwenye maonesho yale wapo waliosema kwa nini anakwenda. Kwa hiyo, hili ya kuongea huko nje wala Mheshimiwa Rais naamini halimpi shida kwa sababu ameyazoea, cha muhimu ni kuona anatekeleza malengo yale aliyoapa kuyakeleza kwa niaba ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye siku ya kilele cha maonesho ya *Expo* siku ya Tanzania tarehe 28 Februari, 2022 Mheshimiwa Rais aliona mikataba 37 ikisainiwa yenye thamani ya shilingi za Kitanzania trilioni 20.5 ambayo kwenye mikataba hiyo 37 tunataraji kutengeneza ajira za vijana wa Kitanzania 205,500. Moja ya mikataba ile 37 ni huu ambao umepelekea kuja na azimio hili, ndio maana nimeanza kwa kumpongeza sana, sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi njema anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Wabunge mmesema vyema kama kuna Mtanzania hajatuelewa basi huyu ameamua mwenyewe kutokuelewa, lakini elimu iliyotolewa hapa kuanzia alipoanza Profesa Kitila Mkumbo mpaka wa mwisho Mheshimiwa Kigwangalla elimu imefika kwa Watanzania, cha muhimu hapa ni kuunga mkono twende tukatekeleze mkataba huu. *(Makofi)*

Naomba pia kuongeze pale kwenye hizo hofu ambazo zinasemwa huko nje, bandari yetu imeuzwa, bandari yetu imebinafsishwa, naomba niwaambie Watanzania kuwa bandari yetu iko salama, haijauzwa na haijabinafsishwa; kilichofanyika ni kutafuta mwekezaji kati ya wawekezaji wengi tunaowahitaji kwenye Bandari ya Dar es Salaam, huyu ni mmoja kati ya wawekezaji wengi tunaowahitaji kwenye Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwakumbushe Watanzania tulipofanya kongamano kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya tarehe 3 Februari, 2023, tulisaini hati za makubaliano nyingine sita na wawekezaji mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji kwenye Taifa letu. Moja ya mkataba tuliosaini siku ile ni hati ya makubaliano kati ya Mamlaka ya Bandari ya Tanzania na Bandari ya Antwerp ya nchini Ubelgiji na lengo lake lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano katika

uboreshaji wa utoaji huduma wa Bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, kama bandari imeuzwa Serikali imeingia hati ya makubaliano nyingine na mwekezaji mwingine ni jambo sio kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bandari yetu ni salama, bado ipo mikoni mwa Watanzania na bado tunawahitaji wawekezaji wengine waje wawekeze kwenye Bandari ya Dar es Salaam na bandari nyingine zote tulizonazo ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitamani sana hilo niwaambie Watanzania kwamba bandari yetu ni salama na bado tunahitaji wawekezaji wengine. Profesa Mbarawa na timu yako endelea kututafutia wawekezaji na kuwapokea wawekezaji wetu kwa ajili ya bandari zetu zote na tuweze kufanya vizuri ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mezani ya kuridhia azimio la makubaliano ya nchi mbili Tanzania na wenzetu wa Dubai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kumbukumbu sikumbuki kama kuna makubaliano yamewahi kuhusisha Watanzania wengi kuyajadili kama haya. Watanzania wengi wamejadili kwenye *platform* mbalimbali, kwenye mitandao ya kijamii ndani na nje ya nchi yetu, kwenye vyombo vya habari, barabara na kwingine kote na hapa inathibitisha namna ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amejenga mazingira bora, mazuri na salama ya Watanzania kutoa maoni yao bila uoga wala hofu. Wengi sana wamechangia kwa uwazi bila hofu, mijadala ilikuwa inakwenda mpaka saa nane usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mijadala ya hii Watanzania wana haki ya kujadili kwa sababu hii nchi yao na wala haina shida, wamejadili na wana haki. Wapo walioonesha hofu na kazi nzuri iliyofanywa na Bunge lako sina mashaka kwamba hofu imeondoka kwa mtu aliyetaka kuelewa hofu imeondoka. Kama kuna watu walikuwa na mashaka na uzalendo na uimara na uthabiti wa Bunge hili bila shaka leo tumethibitisha hili Bunge imara sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana upepo ulivyokuwa unapulizwa walidhani watu watayumba hapa. Waheshimiwa Wabunge mmethibitisha ninyi ni wazalendo, ninyi ni imara, ninyi ni thabiti na hampo hapa kwa bahati mbaya, mko kulinda maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais Samia, kama kulikuwa na watu wana mashaka na uzalendo wake na uimara wake na uthabiti wake bila shaka katika jambo hili tumethibitisha na Rais amethibitisha ni mzalendo, ni imara, ni thabiti anayestahili kuendelea kuaminiwa kuliongoza Taifa letu. Ameonesha ujemedari mkubwa, kelele zimepigwa nyingi, kasimama imara akasema tusonge mbele na kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiacha watu wengi ambao kwa kweli walikuwa wana maswali ya hapa na pale na yamejibiwa, wako wachache ambao walitaka kutumia hofu hii kujaribu kulikoroga Taifa letu na hawa vizuri tukashughulika nao vizuri. Kwa sababu mbegu hata kama ni ndogo namna gani ikipuuzwa iko siku itaota, itaathiri Taifa letu na kweli vizuri tusiyumbishe maneno, tusimumunye maneno, hawa tuwakabili usoni mchana kweupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia 90 ya Watanzania tulizaliwa baada ya Muungano, hizo tofauti hizo huko, hatukuzikuta wala hatuzijui, zilishazikwa baada ya Muungano, sasa bahati mbaya sana anatokea mtu mzima, anaaminika, anakwenda, tumempa heshima na katika watu waliompa heshima ni pamoja na Rais Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais huyu kwa uungwana wake ndiye aliyeamua twende kwenye maridhiano, kwa uungwana kabisa. Hatukubadili sheria, hatukubadili Katiba, Katiba ile ile iliyowafungia, muungwana amewafungulia; sheria zilezile zilizowafungia, muungwana amewafungulia; leo kwa kulewa tu mtu mmoja anataka kusimama kuutumia vibaya uungwana wa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lilianza taratibu, taratibu, tunaanza kuona wanyoosha nyoosha vidole, unasema aah hivi haya maridhiano ndio yanataka kutumika hivi. Hapana, sisi Wana-CCM ndio waasisi wa maridhiano, hatukulazimishwa na mtu, tunayaamini lakini maridhiano yasitumike kuligawa Taifa letu, hilo hatutakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi leo Profesa Mbarawa, uzalendo wake, uungwana wake unaenda kutwezwa kijinga, kilevi; hapana, na kwenye hili lazima tulaani kwa nguvu zote na bahati nzuri mwanzoni watu walikuwa wanaongea pembeni, dada yangu kamleta mwenyewe mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili haliwezi kukubalika, tukianza kuhoji maamuzi ya nchi hii kwa vigezo vya wapi nani anatoka, si sawa. Tunaligawa Taifa letu, tunaharibu nchi yetu na hili lazima lilaaniwe na kila Mtanzania anayetaka haki katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wametoa mifano hapa mimi nilikuwa naagalia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika mbili malizia Mheshimiwa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia nimesoma makubaliano ya Tanzania na Uganda imeandikwa *Intergovernmental Agreement between* Uganda na Tanzania

nikaangalia hii hapa na hii imesainiwa tarehe 25 Mei, 2017 ya bomba la mafuta. Huu hapa na wenyewe unasema hivyo hivyo *Intergovernmental Agreement between The United Republic of Tanzania* na *Emirates of Dubai.* Hapa kuna mmoja umesainiwa 2017 kati ya Tanzania na Uganda hakuna maneno, hakuna hofu na haukuletwa hapa, tumesaini, hakuna kelele na vifungu vinafanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hapa kwa sababu tumekuwa waungwana, tukasema wacha turidhiane ndiyo midomo inapanuka hivi! Hapana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusisitiza wasituharibie nchi yetu kwa sababu ya uungwana wetu, hili hatutalikubali, hili tutalinda kwa nguvu zote, uungwana wa Rais lazima ulindwe. Hivyo ninawaomba Wabunge, nawaomba Wabunge wenzangu tupeleke salamu, tupitishe kwa kishindo makubaliano haya na Watanzania watuunge mkono tuwaadhibu wote wanaotaka kuligawa Taifa hili wajifunze na wasirudie tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, subirini kidogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, subirini kidogo. Mheshimiwa Nape kuna mahali kidogo penye huo mkataba kati ya Uganda na Tanzania ni kweli una vifungu vinavyofanana mpaka pale tuko sawa sawa, changamoto tu ni pale kwamba haukuletwa, uliletwa Bungeni. Eeh, uliletwa kama huu labda hofu ndiyo hazikuwepo. Ahsante sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa maono yake na jinsi anavyojitoa katika kuwahudumia Watanzania. *(Makofi)*

Napenda pia kutoa pongezi na shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais. Pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kukushukuru sana kwa kunipa tena nafasi hii na mimi kuchangia kwenye hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa ninaomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kipekee nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso na Waheshimiwa Wabunge wote, Wajumbe wote wa Kamati kwa hoja nzuri walizozitoa za Kamati. Aidha, ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mitaji ya Umma - Mheshimiwa Jerry Silaa na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya *PIC* kwa michango yao mizuri. Kamati hizi mbili zilifanya kazi kubwa ya kuchambua azimio hili, ninaomba kuwahakikishia maoni yao yote pamoja na maoni ya wadau wote waliopitisha maoni yao kwenye Kamati hizo mbili tumeyapokea na tunakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado muda tunao, fursa kubwa ya kuyafanyia kazi ipo na tunawahakikishia kwamba tutayafanyia kazi maoni yote na ya Watanzania wote kwenye mikataba ya miradi na mkataba wa nchi mwenyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hoja hii. Naomba sasa nianze kuhitimisha hoja yangu kwa kutoa ufafanuzi wa kijumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa hisia kali kuhusu azimio la makubaliano haya kuhusu uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi katika bandari

Tanzania na Waheshimiwa Wabunge wanakubaliana wote na azimio la makubaliano lililoko mbele yetu. Ninaomba kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni yenu na maelezo yenu na tunawaambia kwamba tunaenda kuyafanyia kazi, tunao muda na tutayafanyia kazi kama mlivyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamefanya hivyo kwa kuchangia kwa hisia kali kwa sababu wanafahamu kwamba Bandari ya Dar es Salaam ndiyo lango kuu la uchumi wetu kwa sasa. Kama walivyosema wengi 37% sawa na shilingi trilioni 7.78 ya makusanyo ya mapato ya kiforodha ya *TRA* yanakusanywa kwenye bandari zetu hasa Bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, bandari zetu ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu mikataba kwa kila mradi itakayoandaliwa itapewa bayana kipindi cha utekelezaji wake na ukomo kila mradi tukianzia mradi wa uendeshaji utapewa muda wake, tukianzia kama kuna mradi wa ujenzi pengine gati la abiria tutaupa muda wake na ninaomba nichukue fursa hii hili jambo la muda tuwaachie wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwekezaji anayendesha bandari na mwekezaji anayejenga bandari wanapewa muda tofauti. Huwezi mtu anayeendesha bandari ukampa miaka kumi, anayejenga bandari ukampe miaka kumi; siyo sahihi hata kidogo, kwa sababu mmoja anawekeza sana, mmoja anafanya *operation,* kwa kweli naomba hili ni jambo la kitaalamu, sisi tutalichukua na tuna wataalamu wazuri ambao watalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba tutaweka muda wa marejeo. Tutaweka *time* ya kufanya *review* kwa kila mradi. Miradi mingine tutafanya *review* kila baada ya mwaka mmoja, na miradi mingine tutafanya *review* kila baada ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tutaweka viashiria muhimu vya ufanisi wa kiutendaji yaani *key performance indicators* kwa kila mradi na ninaomba Waheshimiwa Wabunge niwaeleze *key performance indicators* hizi ndiyo zilizomtoa *TICTS*. *TICTS* alikuwa asitoke, lakini *TICTS* alishindwa kufikia vigezo tulivyomuwekea na ikawa hana njia lazima aondoke tu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana muwaamini wataalamu wetu tunaamini wataalamu wazuri na ninaamini kwa kila mradi wataweka hizo *key performance indicators* na mkandarasi yoyote ama muwekezaji yoyote kama atashindwa kutekeleza tutaachana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba tuwahakikishie kwamba uandaaji wa mikataba ya miradi utafanywa na timu chini ya usimamizi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narejea tena, tuna vijana wazuri ambao wana uwezo mkubwa wa kutengeneza miradi kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliopata kuona ule mkataba wa *TICTS,* ule mkataba ulikuwa *non-starter,* ilikuwa hatuwezi kutoka lakini vijana wale wale tuliokuwa nao jana waliupitia mradi ule na *TICTS* mwezi wa Desemba aliondoka bila matatizo yoyote, bila mgogoro wowote kwa vile tunao vijana wazuri wana uwezo mkubwa na watafanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Wabunge wengi wameongea hapa kwamba Tanzania imeelekeza au Tanzania imewekeza takribani shilingi trilioni moja. Serikali imeelekeza ama iliwekeza karibuni shilingi trilioni moja kwenye Bandari ya Dar es Salaam, lakini ufanisi kwenye bandari yetu bado ni changamoto kubwa. Nitawapa mfano, kwa mfano kitengo chetu cha makasha kuanzia gati namba tano mpaka namba saba ambayo inahudumiwa na *TICTS* mwaka uliopita iliweza kuhudumia makasha 150,000 tu wakati pale malengo ilikuwa tuhudumia

takribani makasha 600,000. Hii haiwezekani, hatuwezi tukafanya hivyo kuwaachia watu ambao uwezo wao siyo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna sababu za msingi ambazo zimefanya utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam hasa kwenye kitengo kama cha makasha uwe ni dhaifu. Sababu ya kwanza kabisa tumeshindwa kuwekeza kwenye mitambo mikubwa ya kushushia makontena au makasha kwenye meli. Mheshimiwa Ezra amesema hapa ukitaka kununua *ship to shore crane* moja unahitaji takribani shilingi za Kitanzania bilioni 45 mpaka 50 na kwa meli moja unahitaji *ship to shore cranes* nne kwa wakati mmoja ndiyo utaweza kufanya hiyo kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine tuliyonayo pale sote tunafahamu, tumekuwa na changamoto kubwa sana la mifumo ya TEHAMA na kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama hapa amezungumzia mambo ya TEHAMA. Sasa tunakwenda kupata mwarobaini kwa ajili ya changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, pia Bandari yetu ya Dar es Salaam tumekuwa na changamoto kubwa ya utafutaji masoko. Haya makontena hayaji tu hivi hivi kama watu wanavyofikiria, lazima uwe na mtu ambaye ana uwezo mkubwa, ana *network* kubwa aweze kwenda nje kuleta mizigo mingi zaidi. Kwa vile tuna amini kwa mtazamo tunaokwenda nao wa *DP World,* sasa tunaweza kwena kupata mwekezaji ambaye atatutoa hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema majibu ya changamoto hii ni kuleta mwekezaji mahiri na sisi tunaamini kwamba *DP World* ni mwekezaji mahiri na anaweza kututoa hapa tulipo. *(Makofi)*

Ninaomba nieleze machache tu kuhusu bandari tunazoshindana nazo. Sisi sote katika ukanda huu tunapambania soko la Zambia, Malawi, Rwanda na Uganda pamoja na DRC. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mshindani wetu mkubwa namba moja kwa sasa kwa hapa karibu ni *port* au Bandari ya Mombasa.

Bandari ya Mombasa ina gati 19 wakati sisi Dar es Salaam tuna gati 12 tu. Magati ya kawaida wanayo 13 na magati sita ni kwa kuhudumia makasha. Sisi tunazo gati sita, lakini zote ni ndogo kulinganisha na Mombasa.

Mheshimiwa Spika, lakini wenzetu Mombasa sasa na wao wameshaanza kwenda kutafuta *private sector* kuendesha bandari hiyo hasa sehemu ya makasha. *Container Terminal Number Two* kwa sasa ambao wameijenga kwa mkopo na wao kutoka *JICA* kwa gharama ya dola za Kimarekani 280 tayari sasa hivi inaendeshwa na Kampuni ya *Mediterranean Shipping Company* ya Italy. Kampuni hii inamilikiwa na familia tajiri ya Kiitaliano Bwana Aponte ambaye yeye ni tajiri mkubwa kwenye mambo ya meli.

Mheshimiwa Spika, bandari hii vilevile ina gati ambayo inaendeshwa na *private sector* ambayo kazi yake kubwa ni kuhudumia nafaka.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Durban; Bandari ya Durban inamilikiwa na *Transnet National Port* ya *South Africa* ina magati 50; magati 31 ni ya kawaida ya kuhudumia makontena ni magati 10 na magati ya mafuta na chuma ni magati tisa. Magati 31 ya kawaida na magati 10 yanahudumiwa na *Transnet Port Terminal* siyo *Transnet National Port Authority* ni mtu tofauti ni kampuni ya *South Africa* lakini tofauti. Magati tisa yaliyobaki ya mafuta na mawe na chuma yanahudumiwa na *private sector.*

Mheshimiwa Spika, mshindani wetu mwingine ni Beira kutoka Msumbiji. Bandari ya Beira yenyewe ina magati 11; magati ya shehena za mchanganyiko pamoja na magati ya kuhudumia makontena yanahudumiwa na *private sector (Conal Eda Mozambique)* ni kampuni ambayo inatoka huko Uholanzi.

Mheshimiwa Spika, mshindani wetu mwingine ni Bandari ya Vizag...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri dakika tatu malizia.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu niseme bandari zote sasa hivi hasa kwenye maeneo ya kontena zinahudumiwa kwa asilimia mia moja na *private sector*. Ukichukua Angola, ukichukua Egypt, ukichukua Ghana, ukichukua Nigeria kila mahali wanafanya *private sector* kwa sababu wanafahamu *private sector* ina uwezo mkubwa wa kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tuliamua kuleta *private sector* na tukaamua tulete *private sector* ambaye ana uwezo wa kufikia viwango vya kimataifa pamoja na awe na ufanisi katika utekelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, sifa ya pili ambayo *private sector* tunataka tumlete awe na uwezo wa kutoa ufumbuzi katika mnyororo mzima wa usafirishaji; sifa ya tatu awe na mtandao mpana wa kupata mizigo kutoka soko la usafirishaji duniani; na sifa ya nne awe na uwezo wa kimataifa katika kuendeleza na kuendesha shughuli za kibandari.

Mheshimiwa Spika, majibu yote yako kwa *DP World*. Kampuni ya *DP World* ina uwezo mkubwa katika uendeshaji wa shughuli za bandari duniani kuanzia Afrika, Asia, Ulaya, Marekani ya Kaskazini na Kusini, kwa ufupi anao mtandao mkubwa sana duniani.

Pili, *DP World* ina uzoefu na utaalamu wa kuchagiza mnyororo mzima wa usafirishaji kutoka maeneo ambayo bidhaa zinatoka mpaka kufikia kwa walaji. Kampuni ya *DP World* inamiliki kampuni kubwa ya meli *(P&O)* ambayo ina takribani meli 100 na zinafanya kazi biashara duniani kote. Tunaamini kwa kwenda na *DP World* tutaweza kufanikiwa kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *DP World* inaendesha maeneo mengi maalum ya kiuchumi karibu na bandari, inasafirisha usafirishaji baharini na inafanya kazi kwenye nchi kavu nyingi na hivi sasa tunavyozungumza kule Rwanda wana *logistic park* kubwa ambayo tunaamini *DP World* ikija Tanzania mizigo yote ya Rwanda itakuja au itapitia Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema leo kwamba baada ya kazi hii ya kumleta *DP World* kuna matokeo makubwa tutayapata kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam. Ninaomba nimalizie haya mawili.

Kwanza tunaamini tutapunguza muda wa meli kukaa nangani kutoka masaa manne mpaka matano mpaka kufikia saa 24 kwa siku. Meli inaingia sasa hivi jioni, kesho inaondoka.

**SPIKA:** Ngoja, ngoja, hapo mwanzoni nadhani ulikusudia kusema siku umesema masaa sasa nadhani tutakuwa tuna…

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimesema siku nne mpaka tano za sasa mpaka masaa 24 kwa siku. *(Makofi)*

Pili, kama tutafanikiwa, na naamini tutafanikiwa kumleta *DP World* tutapunguza muda wa ushushaji wa makasha yaani kutoka siku nne kwa sasa mpaka kufikia siku moja na nusu yaani meli itaingia pale baada ya siku mbili inaondoka. Pia tunasema kama tutamleta *DP World* tunaweza kuongeza mzigo kutoka tani milioni 20.8 za sasa mpaka kufikia tani milioni 47.57 ifikapo mwaka 2032/2033.

Mheshimiwa Spika, jambo muhimu ambalo tutafanikiwa nalo ni kuweza kuongeza mapato yanayotokana na kodi ya forodha. Kwa sasa tunakusanya takribani shilingi trilioni 7.756 kupitia *TRA* kama tutaweza kumleta mwekezaji *DP World* tutaweza kwenda mpaka shilingi trilioni 26.709 sawa na 62% ya bajeti ya nchi yetu, pia tutaweza kuongeza kwa kiasi kikubwa ujaji wa meli katika bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niaomba mwisho kabisa niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wabunge mtuamini sana kama tunaenda kuifanya kazi hii kwa uadilifu mkubwa na ninyi wenyewe matokeo mtayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono na kwa utaratibu wetu sasa nitawahoji. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie nafasi hii kutangaza rasmi kwamba Bunge limepitisha Azimio kuhusu pendekezo la kuridhiwa kkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ma Serikali ya Dubai kwa lengo la kuanzisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii katika uendeshaji wa maeneo ya bandari nchini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea azimio hili pia kumpongeza yeye pamoja na Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri iliyofanyika. Tunaamini kwa namna ambavyo Wabunge wamechangia, lakini Wabunge wataendelea kuchangia na wananchi wataendelea kutoa maoni. Naamini mawazo waliyoyatoa Wabunge ndio ambayo yanatakiwa kuweka msingi wa ile mikataba mingine inayokuja huko baadaye ili kuweza kuweka ule uwazi ambao mmeuweka na ambao siku zote mnajitahidi kufanya ili wananchi waendelee kujua kwamba nchi yao inakwenda vizuri katika hilo eneo la uwekezaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni dhahiri sisi wote tumetafatilia maoni ya wananchi kutoka sehemu mbalimbali, wengine kwa maandishi, wengine kwa kuzungumza. Ni muhimu kila mmoja wetu yale ambayo anaona yana tija waliyoyasema wananchi, basi waendelee kuyafUatilia na kuyakusanya kwa

sababu bajeti kuu iko mbele yetu na kipindi chetu hiki cha kuishauri Serikali na kwa sababu eneo hili la uwekezaji linakusudia kuongeza mapato ya nchi yetu. Basi tutapata pia nafasi katika zile siku saba za mijadala kuendelea kuishauri Serikali kwenye uwekezaji kwenye maeneo ya bandari.

Waheshimiwa Wabunge, pia nitambue katika hiyo hiyo michango ambayo wako wananchi wametoa michango mizuri ambayo kwa kweli itatusaidia hata sisi huko mbele na itaisaidia Serikali wakati ikiingia kwenye makubaliano, lakini pia wako wananchi ambao wametoa maoni yao kwa namna ya kumfedhehesha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haipendezi, yeye ni kiongozi wetu, ni nembo yetu kama Taifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ikifika mahali raia unataka kumtweza kiongozi wako mkuu wewe sijui unakuwa uko sehemu gani, maana yeye ndio nembo yetu kwa sasa. Hata kama watu tunatofautiana kisiasa usifike sehemu ya kumkosea heshima kiongozi wa nchi, mpe heshima yake anayostahili na kama unabishana naye bishana naye kwa hoja, usiende kwenye mambo binafsi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeona wako wengine hata wanamtusi utu wake, haipendezi na si jambo ambalo Watanzania tumelizoea. Wakati mwingine kwa sababu ipo mitandao wako watu wengine hata hawapo hapa nchini lakini wapo wengine hata sio wananchi wa Tanzania, lakini wanamtukana Rais wetu na wewe Mtanzania unaambatana nao kana kwamba una Rais mwingine. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Daktari Samia Suluhu Hassan na kama wewe unajiita Mtanzania popote pale ulipo huyo ndio Rais wako. *(Makofi)*

Sasa unataka ama hutaki hilo ni suala lako, lakini sasa yeye ndio Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ataendelea kuheshimiwa kwa sura hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mambo machache japokuwa muda wetu umekwenda sana; la kwanza na kwa kifupi kabisa

makubaliano haya yanaruhusu mabadiliko ama marekebisho, fungu la 22 ama Ibara ya 22 wale wenye mikataba wasome. Makubaliano haya yanaweza kusitishwa, asikwambie mtu tumeingia miguu yote miwili, sijui tumefanya nini, kifungu cha 23 kinaruhusu upande wowote kusitisha, huu huu tunaojadili wacha yale ya baadaye huu huu tunaojadili unaweza kurekebishwa na unaweza kusitishwa. Kwa hiyo, watu wasome vizuri wasiwasikilize wapotoshaji wanasoma robo halafu wanaendelea yeye na maneno yake kama ni sehemu ya huu mkataba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni kuhusu muda, muda lazima utakuwa nje ya hapa kwa sababu mikataba itakayoingiwa ni mingi, tumeshasoma sana vifungu hivyo leo hapa sina haja ya kuvirejea. Mikataba ipo itakayoingiwa ya uendelezaji, ipo ya uendeshaji, haiwezi kulingana muda kwa hiyo hiyo yale mawazo yenu kuhusu muda yatawekwa huko. Lakini mtu anaibuka na heshima zake zote anasema miaka 100 ameisoma wapi kwenye huu mkataba? Hakuna miaka 100 wala hakuna mwezi mmoja, wacha miaka 100. Kama hayo yote hayapo yeye sijui kayatoa wapi na niungane na Wabunge ambao wamependekeza Watanzania tujifunze kufanya utafiti ili unapozungumza usiwe sehemu ya wapotoshaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni kwamba mkataba huu umeshasainiwa, halafu ndio unapelekwa Bungeni sasa itakuwaje? Eeh na kuna shughuli ambazo zimeshaanza na hapa na pale. Zile shughuli wale wapotoshaji hawajazisoma hata kwamba ni shughuli gani, ni shughuli ambazo hata Wabunge humu ndani leo mmesema na mmependekeza kwamba Serikali yetu kabla haijaikabidhi nchi ya Dubai ama kampuni itakayoletwa na Dubai hapa imetajwa jina kwa *DP World* wao wawe wamefanya utafiti ule wa kawaida kabisa ili wanapoenda waseme sisi tulikuwa tumefika hapa, ninyi mchango wenu ni huu, tunautarajia huu, msipofanya huu tutakatisha. Sasa kama sisi wenyewe tunasema hivyo na hizo ndio shughuli zilizotajwa kwenye mkataba kwa sababu zimetajwa ni zipi. Sasa watu wanaenda huko nje ooh mkataba ulishaanza kutekelezwa kabla hata Bunge, ooh mkataba ulishaingiwa kabla hata Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Katiba imeweka utaratibu mzuri lazima Serikali iwe imemaliza kwa sehemu yake ndio ituletee. Hauwezi kuitwa mkataba kama hizo nchi hazijaingia bado hayo makubaliano. Kwa hiyo, lazima wasaini kwanza ndio unakuja hapa Bungeni. Kwa hiyo kwamba wao wametangulia kusaini halafu wametuletea ndio utaratibu hata mikataba yote ya kimataifa ambayo nchi yetu husaini ndio inaletwa hapa, siyo huu peke yake wa uwekezaji. Kwa hiyo, ni vizuri sana wananchi tuendelee kujielimisha kuhusu hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, la mwisho wapo Wabunge ambao wamechangia hapa kuhusu umuhimu wa mikataba ile ambayo sasa itatokana na makubaliano haya kwamba pengine iletwe hapa Bungeni na sisi tuweze kuitazama halafu tuwe na uhakika na mambo yanayofanyika.

Waheshimiwa Wabunge, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(2) inasema; "Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii."

Waheshimiwa Wabunge, sasa hata kama ni kweli tutataka kuona hiyo mikataba sheria yetu ile ambayo tunaitumia kwamba itatupa hayo mamlaka ni hii Sheria Namba 5 ya mwaka 2017 ambayo ni *The National Wealth and Resources Permanent Sovereign Act*. Kifungu cha 12 kinasema; *"All arrangements or agreements entailing extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources may be reviewed by the National Assembly."* Maana yake Serikali lazima iwe imeshaingia hiyo mikataba, lazima hiyo mikataba iwe imeshaanza kutekelezwa, ndio tunakuja hapa kuitazama, sio tunataka kuanza kuitazama kabla hawajaingia, halafu sasa wakiingia mambo yasipokuwa tutatimizaje majukumu yetu ya Ibara ya 63(2). Hatuweza kufanya kazi ya kuisimamia Serikali kwa sababu na sisi tutakuwa sehemu ya huo mkataba maana tulishatoa maoni yetu, sasa tutaisimamiaje. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuipe nafasi Serikali ikaingie hiyo mikataba na sisi tukishaona kuna shida pahala tutaiitisha hiyo mikataba kwa sababu sheria inaturuhusu, lakini sio kwamba tuletewe hapa mikataba tuanze kutoa maoni yetu karekebisheni hapa na pale halafu baadaye mambo yasipoenda huko hatutaweza kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, tufanye kazi yetu ya kikatiba ambayo tumepewa hapo, nadhani hilo litakuwa limeeleweka na kwa kweli nawatakia kila la heri katika hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, la mwisho katika hoja hii hii ni kifungu cha 11 cha sheria hii inayolinda rasilimali zetu inazungumzia kuhusu...; wapo watu wanasema sheria hiyo kifungu cha 11 tumekosea kwa sababu kinakataza kwenda kupeleka kesi nje ya hapa na kutumia sheria na mambo kama hayo.

Waheshimiwa Wabunge, hakuna lililokosewa kwa mkataba huu, kwa mikataba inayokuja mawazo mliyoyatoa na vifungu hivi vilivyotajwa hapa Serikali inapaswa kuvizingatia kwa sababu ndio sheria yetu. Lakini kwa mkataba huu nilishasema wakati nazungumza na baadhi ya Wabunge hapa haiwezekani kutumia sheria za upande mmoja kwa sababu hizi ni nchi mbili zenye uhuru wake na zenye mamlaka yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wale wanaozungumza kwa namna isiyostahili sisi wengine unaweza kutuzungumzia sawa, lakini usimtusi Mheshimiwa Rais, sio heshima huyo kiongozi wa nchi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo niwakumbushe tena kesho kuna semina ile inayohusu elimu, msikose ili mtoe mawazo yenu huko elimu yetu iwe bora kabisa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 9.08 Alasiri Bunge Lilihairishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 12 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*